Nipashe
Jumanne Agosti 13, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579995
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Vifo ajali gari la mafuta, amani vyatawala ibada ya Iddi el Haji

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mikopo elimu ya juu yageuka kaa la moto

• **Hoja** mahsusi sasa kutinga bungeni, Wizara yakubali kupokea malalamiko, yataja hatua kuchukua... *Endelea ukurasa wa 2*



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu Mkoa wa Dodoma, wakishiriki Swala ya Eid El Haji, katika Uwanja wa Jamhuri, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Dk. Bashiru awashukia waliochoma nyumba

UKURASA 3

## Walipozikwa marehemu Moro sasa kujengwa mnara, uzio

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YAITIA HOFU TOWNSHIP ROLLERS** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mikopo elimu ya juu kaa la moto

**Na Waandishi Wetu**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imesema itawasilisha hoja mahsusi bungeni wakati wa mkutano ujao wa Bunge kupinga ongezeko la asilimia sita kila mwaka katika deni la wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

Mkutano ujao wa Bunge la 11 unatarajiwa kuanza Septemba 3, mwaka huu ukitanguliwa na vikao vya kamati za kudumu za chombo hicho cha kutunga sheria.

Vilevile, kambi hiyo imesema katika hoja yake hiyo, pia itapinga makato ya asilimia moja yanayofanywa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) dhidi ya wanufaika wa mikopo hiyo kwa ajili ya ada ya uendeshaji kwa kuwa serikali kila mwaka imekuwa ikitenga fungu maalum kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za bodi hiyo.

Kifungu 7.2.1.1 cha Mwongozo wa HESLB wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa Wanafunzi kinabainisha kuwa mnufaika wa mkopo wa bodi hiyo atalipa tozo ya kulinda thamani ya fedha ambayo itakatwa asilimia sita kwa mwaka tangu tarehe mnufaika aliyoanza kupokea mkopo.

Pia, katika kifungu 7.2.1.2 cha mwongozo wake huo, HESLB inaeleza kuwa itakata asilimia moja ya ada ya uendeshaji kwa mwanafunzi mnufaika.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Susan Lyimo, alisema kambi yao imeamua kuwasilisha hoja bungeni kupinga makato hayo.

Alisema kuwa kabla hoja hiyo haijatua kwa Spika, ataiwasilisha kwanza kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ili kamati hiyo ambayo yeye ni mjumbe, iitake serikali kupeleka bungeni muswada wa kurekebisha Sheria Na. 9 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya Mwaka 2004 ili vifungu vyenye makato hayo vifutwe.

"Serikali itambue kwamba HESLB na haifanyi biashara, bali inatoa huduma ya kuhakikisha watoto wanaotoka familia maskini wanapata elimu ya juu, lakini kwa hali ya sasa ya kuwaongeza deni wanufaika wa mikopo, hakuna haja ya kuwa bodi hiyo," Lyimo alisema na kueleza zaidi:

"Kama wanataka kufanya biashara, basi jukumu hili lisifanywe na HESLB, liachwe kwa benki. Kumtoza mnufaika wa mkopo wa elimu penalti ya asilimia 10 ya mkopo kisha tozo ya asilimia sita ya mkopo kila mwaka na asilimia moja kwa ajili ya uendeshaji si haki.

"Inakuwa ngumu kwa wanufaika kumaliza kulipa deni kwa sababu linaongezeka kila mwaka hata kama wanalilipa, vinginevyo ndugu waungane na mnufaika kulipa deni lote kwa siku moja.

"Kitafika kipindi vijana wetu hawa itakuwa shida hata kuingia kwenye maisha ya ndoa kwa sababu watahofu kuoa au kuolewa na mtu mwenye deni la HESLB ambalo hata ukianza kulilipa haliishi.

"Makato yenyewe ya marejesho ni asilimia 15 ya mshahara wa kila mwezi, huyo anayekatwa ana makato mengine ya bima ya afya, kodi ya serikali, michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii... yaani karibu asilimia 50 ya mshahara wake unaishia kwenye makato ya taasisi za serikali, huyu mtoto wa maskini ataishije?"

Mbunge huyo wa Viti Maalum (Chadema) kwa kutambua uzito wa suala hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona njia nzuri ya kutatua changamoto zilizojitokeza ni kuwasilisha hoja maalum bungeni kuitaka serikali kufanya marekebisho tena katika sheria iliyoanzisha HESLB.

"Hizi penalti za asilimia 10 na tozo ya asilimia moja nazo ni tatizo. Hakuna nchi nyingine inayofanya hivi. HESLB inatengewa fedha na serikali kwa ajili ya uendeshaji na watumishi wake wanalipwa mshahara na serikali.

"Pia tunaona hakuna haja kupiga penalti mnufaika kwa sababu hali halisi ya ajira nchini inajulikana. Kikubwa, bodi iwe na mfumo mzuri wa kuwatambua wanufaika," alishauri.

INAENDELEA UK. 8



Daktari wa Kituo cha Afya Tinde, Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga Vijijini, Josephine Otieno, akiwa amepiga magoti kuomba msamaha kwa niaba ya wauguzi wa kituo hicho, ambao wamekuwa wakituhumiwa kwa utoaji wa lugha chafu za matusi kwa wagonjwa pamoja na kuwafanyia ubaguzi wa kikabila, kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Solwa, Ahmed Salum akiwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Eneo la maziko kujengwa mnara, uzio

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Morogoro kuhakikisha eneo walipozikwa watu waliofariki dunia kwa ajali ya lori la mafuta lililopinduka na kuwaka moto katika eneo la Msamvu Itigi, Manispaa ya Morogoro, panawekwa uzio na kujengwa mnara maalum utakaokuwa na majina yote ya marehemu.

Lengo la ujenzi wa mnara na uzio ni kulifanya eneo hilo kuwa kumbukumbu ya tukio hilo la kihistoria.

Waziri Mkuu alisema hayo jana, alipotembelea makaburi ya Kola walipozikwa, huku miili mingine ikiendelea kuzikwa katika siku ya pili, mingine ikisafirishwa, na mingine ikiendelea kusalia chumba cha kuhifadhi maiti kwa taratibu zaidi.

Alisema watu wote wenye ndugu waliozikwa waruhusiwe kuyatembelea makaburi hayo, kuyajengea, kufanya ibada au taratibu zozote kulingana na mila zao wakati wowote, na kwamba nia ya uzio na mnara huo ni kuweka kumbukumbu kama maeneo mengine ambapo miili ya watu waliokufa kwenye ajali kadhaa nchini.

Majaliwa alipongeza ushirikiano uliooneshwa na wadau mbalimbali tangu ajali hiyo ilipotokea, vikiwamo vyombo vya habari, wataalamu wa Wizara mbalimbali, madaktari, wauguzi, wananchi na viongozi walioshirikiana kwa hali na mali kuhakikisha shughuli zote za tukio hilo zinafanikiwa.

Pia aliwashukuru waliojitolea kuchangia damu na misaada mbalimbali ya kibinadamu kwa ajili ya majeruhi na miili ya waliopoteza maisha.

"Tunavishukuru sana vyombo vya habari, bila kujali kikubwa, kidogo, magazeti, mitandao ya kijamii kwani toka tukio hili limetokea walikuwa mstari wa mbele kuhamasisha umma wa Watanzania kile kinachojiri," alisema na kuongeza:

"Watanzania waliweza kufikiwa na taarifa zote za matukio haya kwa wakati... Serikali inategemea zaidi ushirikiano huu uzidi kuendelezwa, na itazidi kutoa ushirikiano kwa kutoa hali halisi ya maendeleo ya nchi."

Akasema hadi sasa jumla ya miili tisa imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhi maiti cha Hospitali ya Rufanu ya Mkoa wa Morogoro ikisubiri kutambuliwa na mingine imeshatambuliwa ikisubiri taratibu za mazishi kutoka kwa familia husika.

**WAZIRI MHAGAMA**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu),Jenista Mhagama, alibainisha miili iliyobaki itaendelea kuhifadhiwa vyema kwenye majokofu hadi itakapotambuliwa au kuchukuliwa kwa maziko, na kwamba chumba

cha kuhifadhi maiti hakijaelemewa baada ya miili mingi kuchukuliwa kwenda kuzikwa.

Akabainisha miili yote imeshafanyiwa vipimo vya vinasaba, hivyo kurahisisha ndugu kwenda kuwatambua wakati wowote, kwani taarifa zao zitaendelea kuhifadhiwa, huku akimshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa Maelekezo kwa Waziri Mkuu kushirikisha wizara na mawaziri wote wanaohusika kusimamia suala zima la maafa, ili wahakikishe majeruhi wanapata tiba stahiki na miili inahifadhiwa kama inavyostahili.

INENDELEA UK. 8

# Kibano chaja waliosambaza picha walioungua Morogoro

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, ameliitaka Jeshi la Polisi kuwakamata wanaosambaza picha za marehemu mitandaoni.

Masauni alitoa kauli hiyo jana mjini Morogoro mara baada ya swala ya Eid iliyofanyika katika Msikiti Mkuu wa Mkoa huo.

Kiongozi huyo wa wizara alisema kusambaza mitandaoni picha za marehemu ni kuwadhalilisha wahusika na ni uvunjaji wa sheria za nchi.

"Ninaziagiza mamlaka na vyombo vinavyohusika vihakikishe vinafuatilia na kuchukua hatua kwa wale ambao wanakiuka sheria za nchi yetu kwa kusambaza mitandaoni picha za marehemu," aliagiza.

Masauni alisema siyo vema kuanza kutumia majanga ya kitaifa kama lililotokea Morogoro la watu zaidi ya 70 kufariki dunia ndani ya muda mfupi, kuanza kusambaza picha za waathirika mitandaoni kwa dhamira ya kudhalilisha.

"Watu hawa wamefariki dunia na mtu yeyote katika tukio lile angekufa, mimi au wewe, ndugu yako au jamaa yako, fikiria kama ni jambo limekukuta au ndugu yako halafu ukachukua picha na kuisambaza kwenye mitandao, katika mazingira kama yale," Masauni alisema.

Alisema kufanya hivyo siyo tu kunavunja sheria za nchi, bali pia ni kinyume cha utamaduni wa Mtanzania.

"Wananchi watambue kwamba kuvunja sheria ni kosa na hatua zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya mhusika aliyefanya hivyo, natoa wito kwa wananchi kuacha tabia hiyo ya kudhalilisha wengine," alisema.

Jumamosi iliyopita, kulitokea tukio la moto lililohusisha roli lenye tangi la mafuta lililolipuka na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 70 na majeruhi.

## HABARI KIMATAIFA

# Ajali Morogoro, amani vyatalawa Eid

**Na Waandishi Wetu**

WAUMINI wa dini ya Kiislamu wametakiwa kujifunza kupitia tukio la moto lililotokea mkoani Morogoro na kuishi maisha yanayompendeza Mwenyezi Mungu kwa kuwa hawajui siku ya mwisho ya maisha yao.

Sambamba na hilo, wametakiwa kuendelea kuwaombea viongozi wakuu wa serikali ili wawe na busara na hekima katika kuliongoza vyema taifa.

Wakati hayo yakihimizwa, Rais wa Zanzibar, Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka waumini wa dini hiyo na Watanzania kwa ujumla kudumisha amani ambayo ni tunu muhimu kwa taifa la Tanzania.

Akitoa mawaidha katika ibada ya Sikukuu ya Eid el Hajj, iliyofanyika katika msikiti wa Gadafi jijini hapa, Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Shaaban, alisema Waislamu wanatakiwa kujifunza kupitia tukio hilo kwa kuishi katika misingi inayompendeza Mungu ili kujiandaa na safari yao ya mwisho katika maisha yao.

"Tunaona kama ndugu zetu waliokufa pale Msamvu, Morogoro kutokana na ajali ya lori la mafuta ambavyo waliteketea kwa moto, hivyo ndivyo ilivyo hata kwetu kwani hatujui kifo chetu kitakuwaje. Ni lazima tujiandae kila wakati kwani Mwenyezi Mungu anatoa hukumu yake baada ya sisi kufa," alisema.

Pia aliwataka waendelee kuwaombea viongozi wakuu kwa kuwa bila viongozi wakuu wa nchi kuwa na busara, hekima na afya njema, hawawezi kuliongoza taifa, hivyo kuchangia kwa baadhi ya mambo kutokwenda sawa.

"Lazima tuendelee kuwaombea hawa viongozi wetu kwani bila wao kuwa na vitu hivi, taifa haliwezi kusonga mbele. Lazima tuendelee kuwaombea kwa Mungu ili wayafanikishe yale yote ambayo wameyapanga kwetu," alisema.

Aliwataka waumini wa kiislamu kuwa na umoja kwa kufanya mambo kwa kushirikiana ili kujikwamua kiuchumi.

"Ndugu zangu Waislamu, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, hivyo yatupasa kushirikiana ili kutoka hapa tulipo kama mnavyoona kwa kiongozi wetu Mufti (Sheikh Mkuu wa Tanzania) ambavyo ameondoa migogoro iliyokuwapo awali baina ya makundi mbalimbali ya Waislamu nchini," alisema.

Aidha, aliwataka Waislamu kuacha tabia ya kuitumia siku ya Eid el Haji kuwa ni sehemu ya kulewa pombe kupita kiasi au kuwa wakorofi wa kupindukia.

Katika hatua nyingine, Sheikh wa Wilaya ya Bahi, Suleman Twalib, aliwataka Waislamu kuitumia sikukuu hiyo kuwakumbuka watu wasiojiweza wakiwamo yatima, wajane na wazee.

Sheikh Twalib aliwataka kuhakikisha wanatumia furaha hiyo ya sikukuu kujumuika na watu wa jamii hiyo ambao mara nyingi wamekuwa wakisahaulika.

Alisema inasikitisha kuona baadhi ya waumini wa Kiislamu inapofikia siku kama hiyo, wako tayari kutumia mali na fedha zao kwa anasa huku wakiwaacha wasiojiweza bila kuwasaidia.

Pia aliwataka waumini wa wilaya hiyo wenye sifa ya kuwa viongozi katika nafasi za uenyekiti wa serikali za mitaa kujitokeza kugombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwishoni mwa mwaka huu.

### BAKWATA WATOA POLE

Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) Mkoa wa Singida limetoa pole kwa Rais john Magufuli kutokana na vifo vya watu 71 waliofariki dunia kwa kuungua moto mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki.

Katibu wa Bakwata Mkoa wa Singida, Burhan Mlau, alitoa pole hiyo katika sala ya Eid Al Haji iliyofanyika jana katika viwanja vya Shule ya Msingi Sumaye, mkoani hapa.

"Tunampa pole Rais wetu kwa msiba huu mkubwa tulioupata pamoja na wafiwa na tunawaombea majeruhi wote wapate nafuu na kurejea katika shughuli za ujenzi wa taifa" alisema Mlau.

Katika sala hiyo, Mlau aliwataka Waislamu mkoani hapa kuwa kitu kimoja na kuondoa utengano kupitia taasisi zao mbalimbali badala ya kutengana.

"Nawaombeni ndugu zangu Waislamu tuendelee kushikamana na kupendana kupitia taasisi zetu jambo ambalo litadumisha uislam wetu na kumpendeza Mwenyezi Mungu," alisisitiza.

Katika kusherehekea sikukuu hiyo Mlau aliwaomba waislam wa mkoa huo kusherehekea kwa utulivu na amani huku wakiwaangalia watoto wao kwa ukaribu.

### JAFO ATAKA AMANI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jaffo, alisema Tanzania haiwezi kwenda katika uchumi wa kati bila kuwa na amani.

Jafo alisema hayo jana katika Baraza la Eid na sala ya Eid el-Hajj kitaifa iliyofanyika katika viwanja vya Masjid Kibadeni Chanika jijini Dar es Salaam, ambako alikuwa mgeni rasmi.

"Ajenda ya amani, hakuna yeyote mwingine ambaye atafurahia kuona nchi inakosa amani. Tunapaswa kujielekeza kwenye amani na ukipoteza amani umevunja amani ya nchi, Watanzania tuendelee kuliombea taifa," alisema Jaffo.

Alisema ufisadi, dhuluma na chuki vinajenga matabaka baina ya watu, lakini Rais Magufuli amejitahidi kuviondoa tangu alipoingia madarakani na ndiyo maana aliamua kuanzisha Mahakama ya Mafisadi ili watu wabadilike kimawazo na kifikra.

Mufti Mkuu wa Tanzania, Abubakary Zubeiry, alisema Bakwata haitavumilia mtu atakayeivunja amani, heshima na kwamba itahakikisha chombo hicho kinaheshimiwa na kila Mwislamu.

Kwa upande wake, Kaimu Sheikk wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ramadhani Kitogo, aliwataka Waislamu kuwa kitu kimoja, waungane, washikamane na wadumishe amani

Naye Katibu Mkuu wa Bakwata, Alhaj Nuhu Jabir Mruma, alisema: "Tunakerwa na migogoro inayotokea ndani ya misikiti. Malizeni haraka, msipomaliza kwa haraka migogoro yenu Bakwata litaingilia kati. Tunataka migogoro yote imalizwe ngazi ya chini kabla haijaletwa katika ngazi ya juu."

***Imeandikwa na Paul Mabeja na Peter Mkwavila, DODOMA; Doto Mwaibale, SINGIDA na Gwamaka Alipipi, DAR.*** ***Habari zaidi Uk. 23***

# Rais wa Afrika Kusini kuwasili leo

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ataingia nchini leo kwa ziara ya siku mbili na baadaye kushiriki katika mkutano wa viongozi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Makonda alisema hayo jana wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujio wa rais huyo, jijini Dar es Salaam.

Mkutano wa viongozi wa SADC unatarajiwa kuanzia Agosti 16 na Rais Dk. John Magufuli ambaye ndiye mwenyeji wa mkutano huo atakabidhiwa kijiti cha uenyekiti wa SADC kutoka kwa Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob.

Makonda alisema wiki hii itakuwa ya maandalizi ya kuwapokea marais wa nchi za Jumuiya hiyo watakaohudhuria mkutano huo. Viongozi wa nchi 16 wanatarajiwa kuingia nchini kushiriki mkutano huo.

Pia, Makonda alisema ujio wa viongozi hao utatoa fursa kwake kuuliza jinsi nchi hizo zinavyowashughulikia wanaume wanaowaumiza wanawake.

Alisema wanawake wengi wa Jiji la Dar es Salaam wamekuwa wakilalamikia kuumizwa na wanaume

INAENDELEA UK.8




Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akipita jirani na vibao vinavyoonyesha kufungwa kwa Barabara ya Akachube, kwa ajili ya ukarabati mkubwa unaoendelea katika eneo la Kijitonyama, Manispaa ya Kinondoni, jijini humo jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Kigogo CCM ashukia waliochoma nyumba

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ameunga mkono uamuzi wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kusitisha operesheni ya kuwaondoa na kuwachomea nyumba na mazizi wananchi wa Kijiji cha Vilimavitatu wilayani Babati mkoani Manyara.

Amesema kitendo kilichofanywa na viongozi hao wa wilaya ni cha kinyama kwa kuwa kimefanywa dhidi ya raia wasiokuwa na hatia.

Akizungumza na wanachama wa CCM wilayani Meatu mkoani Simiyu kwenye ziara yake mkoani humo mwishoni mwa wiki, Dk. Bashiru alisema operesheni hiyo iliyoendeshwa na uongozi wa Wilaya ya Babati imesababisha familia nyingi kuishi bila makazi.

Alisema operesheni hiyo imefanyika wakati tayari Rais John Magufuli alishaunda kamati ya mawaziri wanane akiwamo Mpina kushughulikia changamoto za wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi na hajatoa uamuzi wa mwisho kuhusu suala hilo.

Alisema ni lazima viongozi wa chama hicho waliopewa dhamana ya kusimamia serikali, kufuatilia kwa karibu maagizo yote ya Rais ambaye ni Mwenyekiti wa chama.

Tayari Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mpina amesitisha operesheni ya kuwaondoa na kuwachomea nyumba, mazizi ya mifugo na makambi ya uvuvi wananchi wa Kijiji cha Vilima vitatu na kuunda timu ya wataalamu kutoka wizara nae kufuatilia utekelezaji wa operesheni hiyo na kuwasilisha ripoti hiyo serikalini kwa uamuzi zaidi.

"Inawezekanaje mkuu wa nchi ameelekeza tulieni kwanza tufanye utafiti, tufanye uchambuzi, msifanye lolote mpaka tutakapokuwa tumetoa maelekezo halafu mtu anageuka, aliyeteuliwa na Rais. huyo huyo anavuruga utaratibu," Dk. Bashiru alihoji.

"Maagizo ya Rais ni maagizo ya mwenyekiti, ukishasikia ameagiza Rais na ni Rais wa CCM, wewe hayo ni maagizo ya mwenyekiti wako, anza kutekeleza ndiyo namna ya kukipa heshima chama chetu, tukianza kupishana kati ya serikali na chama katika mambo ya msingi, hatutaweza kupata uhalali wa kuongoza nchi yetu."

Ilielezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi wiki iliyopita kuwa operesheni hiyo ya Babati iliyofanyika Julai mwaka huu, imesababisha wananchi wengi kukosa mahali pa kuishi kutokana na nyumba zao kuchomwa moto na sasa wanaishi chini ya miti.

## HABARI KIMATAIFA

# Sababu zinazochangia afya ya akili zatajwa

**Na Augusta Njoji,** aliyekuwa IRINGA

IMEELEZWA kuwa takriban asilimia moja ya idadi ya Watanzania wanakabiliwa na matatizo ya afya ya akili, huku sababu zinazochangia hali hiyo zikitajwa kuwa ni vinasaba na hali za kimaisha.

Kwa mujibu wa Daktari wa Afya ya Akili katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ububuyu, alisema sehemu kubwa ya wagonjwa wenye matatizo hayo wanahudumiwa katika hospitali za Mirembe na Muhimbili.

“Maeneo mengi ya mjini yana watu wengi zaidi wenye matatizo hayo kuliko vijijini, hii asilimia moja ni ya wale ambao wanachanganyikiwa kabisa na kufikia hatua ya kuokota makopo,”alisema.

Alisema watu hao wanahitaji tiba ili kuondokana na tatizo hilo.

“Pia tuondoe suala la unyanyapaa kwa kuwaita machizi hawa watu wana tatizo la Afya ya akili sio chizi, hili neno hili linaonesha unyanyapaa halipaswi kutumiwa, maana hata wanaoumwa hawapendi kulisikia,” alisisitiza.

Aidha, alisema upande wa ugonjwa wa sonona asilimia 8 hadi 20 ya watanzania wanakabiliwa nao.

“Maeneo ya mijini pia yana changamoto zaidi kwenye “depression” kuliko vijijini, vichocheo vipo vingi mijini kama vile msongo wa mawazo(stress), vilevi na changamoto za kimaisha tangu utotoni,” alisema.

Mtaalam huyo huyo alisema ugumu wa maisha na unyanyasaji unawapata wakiwa utotoni na watoto wa mjini wanaathirika zaidi na hali hiyo kuliko wa vijijini.

Oktoba 10, mwaka 2018, akitoa tamko la Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, kuhusu siku ya afya ya akili Duniani, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Muhammad Kambi, alisema imani za kishirikina kwa jamii ni moja ya sababu kuu ya wagonjwa wengi wa afya ya akili kushindwa kufikishwa katika hospitali ili kupata matibabu mapema.

Alisema wagonjwa wengi wenye matatizo ya afya ya akili nchini wamekuwa wakipelekwa kupata tiba za kiimani na kushindwa kufikishwa katika hospitali ambapo wangepata matibabu kwa wakati mwafaka.

“Nitoe wito kwa jamii kuhakikisha kuwa wagonjwa hawa wa matatizo ya afya ya akili kuletwa katika hospitali ili waweze kupatiwa matibabu kwani matibabu pamoja na dawa zote zinazohusu afya ya akili zinatolewa bure katika taasisi zetu za serikali,”alisema Prof. Kambi.

Alisema kuwa serikali kwa upande wake imeendelea na utekelezaji wa sera ya afya ya mwaka 2007 ambayo inalenga katika kutoa huduma bila malipo kwa wagonjwa wa akili.

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa magonjwa ya akili

INAENDELEA UK. 8

## Salma Kikwete awataka wazazi kusomesha watoto

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAZAZI na walezi katika mikoa ya Lindi na Mtwara, wametakiwa kuwahimiza watoto wao kwenda shule wapate elimu itakayowasaidia katika maisha yao ya baadae.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na mke wa Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, Salma Kikwete, alipokuwa akitoa salamu kwa wananchi waliojitokeza katika kilele cha Siku ya Wakulima, Nanenane Kanda ya kusini katika Manispaa ya Lindi.

Salma pia aliwashauri wazazi kuwaelimisha watoto wajiepushe na mimba za utotoni ili kufikia ndoto zao.

Salma ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum, alisema wasichana wanapopata mimba wakiwa na umri mdogo, hali hiyo inawasababishia athari kubwa ikiwamo kuwakatishia ndoto zao za baadae.



Mkurugenzi wa Tanzania Youth Alliance, Peter Masika, akizungumza na vijana wakati wa maonyesho ya vijana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya vijana duniani yaliyofanyika jijini Dar es Salaaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali mbioni kubadili mitaala elimu ya ualimu

**Na Salome Kitomari**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema inakusudia kufanya marekebisho ya mitaala ya elimu ya ualimu ili iendane na mabadiliko mbalimbali.

Mabadiliko hayo ni pamoja na mitaala ya shule za msingi na sekondari ambayo yalianza kutumika mwaka 2015.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa elimu ya ualimu, waliokutana jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa maoni ya kuboresha usimamizi na maendeleo ya maboresho ya mitaala ya ualimu.

Alisema mtaala wa mafunzo ya ualimu uliopo sasa ni wa zamani akitolea mfano wa mafunzo ya ualimu kwa walimu wa diploma ambao ni wa mwaka 2008, huku ngazi ya cheti ukiwa wa mwaka 2009 hivyo kutoendana na mtaala mpya wa elimu msingi ambao unazingatia ufundishaji wa KKK.

“Elimu ni suala la kitaifa hivyo serikali haiwezi kujifanya haisikii, jamii inasema nini ndio maana kikao cha wadau kimeitishwa na pia Waziri wa Elimu yupo mbioni kuitisha mkutano wa wadau kwa lengo la kupata maoni ya namna bora ya kuboresha elimu,” aliongeza Dk. Akwilapo.


Pia Katibu Mkuu huyo aliwataka wadau hao kutumia mkutano huo kujadili na kutafakari kwa kina mfumo wa maandalizi ya walimu nchini kwa kuzingatia mada ya Usimamizi na Maendeleo ya Elimu ya Ualimu, Fursa na Changamoto pamoja na upimaji na tathmini yake.

“Tumieni mkutano huu vizuri na mambo mtayakojadili yajikite katika kuona ni namna gani mnaboresha mahiri zinazohitajika kwa mwalimu, ama mkufunzi, mazingira na miundombinu wezeshi, uongozi na usimamizi wa mafunzo, upimaji na tathmini ya mafunzo pamoja na maendeleo endelevu ya mwalimu,” alisisitiza Dk. Akwilapo.

Naye Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema mkutano huo wa wadau wa elimu utachochea mabadiliko katika sekta nzima ya elimu kwa kuwa ili kufanikiwa katika sekta hiyo ni lazima kuwe na ushirikishwaji wa wadau wa elimu.

“Tumekutana kwa ajili ya kuongelea moyo wa taifa letu, elimu ni moyo wa taifa unaposema elimu unapozungumzia elimu ya ualimu katika kuleta mabadiliko ya sekta nzima ya elimu,” aliongeza Dk. Mtahabwa.

“Unaweza kujenga shule nyingi, ukawa na vifaa vya kutosha, lakini kama hauna walimu bora ni kazi bure hivyo tunataka walimu wawe na waledi, wawe kioo cha jamii kuanzia uvaaji wake, kutembea, kuongea na namna anaivyoishi shuleni na hata kijijini awe mfano wa kuigwa katika jamii,” alisema.

## MJADALA

# Mahakama yakubali viongozi EAGT kushtakiwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam imekubali kuwa viongozi wa Kanisa la Evangelistic Assemblies of God (EAGT), wanastahili kushtakiwa mahakamani kwa tuhuma za ubadhirifu wa mali za kanisa ikiwamo ukwepaji kodi kwa kuingiza magari kinyume cha taratibu na uvunjaji wa Katiba ya kanisa hilo.

Viongozi hao ambao ni walalamikiwa katika kesi hiyo ni wadhamini wa kanisa hilo, Mchungaji Christomoo Ngowi na Mchungaji Asumwisye Mwang'mbola (kwa sasa marehemu).

Wengine ni Askofu Mkuu Brown Mwakipesile, Katibu Mkuu, Mchungaji Leonard Mwizarubi na Mweka Hazina Mchungaji Praygod Mgonja, wote wa kanisa hilo.

Uamuzi huo umetolewa Agosti 9, mwaka huu na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Leila Mgonya, baada ya kutupilia mbali hoja tano za pingamizi la awali la walalamikiwa wakidai kwamba hawastahili kufunguliwa kesi na kushtakiwa kama watu binafsi katika maombi madogo ya madai namba 54/2019.

Walalamikaji ni wachungaji Yared Lesilwa, Gilbert Weja na Petrol Kapama kwa niaba ya wachungaji wengine 546 nchini, wamefungua maombi hayo Februari 11, mwaka huu na kupangiwa kusikilizwa mbele ya Jaji Mgonya.

Walalamikaji kupitia Wakili Edwin Swalle, wamefungua maombi hayo wakiomba mahakama kuruhusiwa kuwashtaki viongozi hao kwa tuhuma za ubadhirifu wa mali za kanisa ikiwamo ukwepaji wa kodi kwa kuingiza magari kinyume cha taratibu.

Ilidaiwa kuwa magari hayo yalipata msamaha wa kodi wa serikali wakati hayapo kwenye orodha ya mali za kanisa jambo ambalo ni uvunjifu wa katiba, kuwafukuza wachungaji bila ya kufuata katiba ya kanisa na sheria za nchi.

Vile vile, walalamikiwa kupitia wakili Didas Kanyambo, walipinga maombi hayo wakidai kuwa hawastahili kushtakiwa kwa mashtaka hayo ila bodi ya wadhamini ya kanisa hilo ndiyo ishtakiwe siyo wao kama viongozi kwa majina yao.

Hata hivyo, mahakama iliangalia kama wadaiwa hao wanastahili kushtakiwa binafsi ama bodi ya wadhamini ya kanisa hilo, ilijiridhisha kwamba wanastahili kufunguliwa mashtaka na kuburuzwa mahakamani.

Wakili Swalle, alidai kuwa kwa kuwa mahakama imekubali maombi yao walalamikaji wanatarajia kuwafungulia mashtaka ya ubadhirifu wa mali za kanisa, ukwepaji wa kodi kwa kuingiza magari kinyume cha utaratibu na uvunjaji wa katiba ya kanisa hilo.

Katika madai ya msingi, walalamikiwa hao wanatuhumiwa kutengeneza Tin namba zaidi ya nne kwa jina la kanisa na kwamba kwa mujibu wa sheria, taasisi inatakiwa kuwa na Tin namba moja tu.

TIN zinazosemekana zimesajiliwa na mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa jina la EAGT ni pamoja na; TIN No. 1000932326 kwa jina la Temeke Evangelistic Assemblies of God.

# Sera yakwamisha viuadudu kupulizwa

**Na Beatrice Moses**

TATIZO la kisera nchini lilikwamisha matumizi ya dawa ya viuadudu inayozalishwa na Kiwanda cha kuzalisha viuadudu vya kuangamiza viluilui vya mbu cha Tanzania Biotech Product(TBPL).

Dawa hiyo yenye uwezo wa kuua mazalia ya mbu,inatajwa iwapo ingetumika miezi kadhaa iliyopita ingesaidia kupunguza idadi ya waliougua ugonjwa wa dengue.

Hayo yalibainishwa na Meneja Ubora wa TBPL Samuel Mziray, alipokuwa akingumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, wakati wa maonyesho ya nne ya bidhaa katika wiki ya viwanda vya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika(SADC) yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

"Tatizo la kisera nchini ilikuwa na afua yake ambayo ni vyandarua kuwekewa viatilifu,ndiyo lililokwamisha dawa hiyo isinyunyizwe," Mziray alisema.

Alibainisha kuwa pamoja na hayo wamepata taarifa kuwa Wizara ya Afya imejipanga kuanzia mwaka huu wa fedha kutenga bajeti itakayowezesha dawa hiyo kusambazwa nchini.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

# UNAUDITED RESULTS
## FOR THE SIX MONTHS ENDED JUNE 30, 2019

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

During the first half of 2019, Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) recorded a total revenue of TZS 158bn, similar to the performance in the first half of 2018.

In terms of Operating Profit, TPCPLC delivered TZS38.7bn thus maintaining the same margin as in the first six months of 2018. TPCPLC Net profit for the first half of 2019 is TZS 26.2bn.

TPCPLC remains the leader in the market and persists in its efforts to achieve the highest results for its shareholders and stakeholders.

Prospects
TPCPLC will continue in its determination to maintain its market leadership position.

Appreciation
The Board would like to thank all its stakeholders for their support during the period. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders in the future

**BY ORDER OF THE BOARD**

**Hakan Gurdal**
**Chairman of the Board**
**22 July 2019**

| INCOME STATEMENT | JAN - JUN 2019 TZS'000 | JAN - JUN 2018 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 157,596,722 | 157,863,811 |
| Cost of sales | (98,032,697) | (95,003,294) |
| **Gross profit** | **59,564,025** | **62,860,517** |
| Selling and administrative expenses | (9,950,088) | (12,280,417) |
| Other operating income/ (charges) | (1,131,711) | (1,411,288) |
| Depreciation and amortisation | (9,786,410) | (10,276,822) |
| **Operating profit** | **38,695,816** | **38,891,990** |
| Financial items | (1,106,328) | 537,981 |
| **Profit before tax** | **37,589,488** | **39,429,971** |
| Taxes on income | (11,391,507) | (12,206,740) |
| **Net profit for the period** | **26,197,981** | **27,223,231** |

| BALANCE SHEET | 30 JUNE 2019 TZS'000 | 30 JUNE 2018 TZS'000 |
|---|---|---|
| **Assets** | | |
| Non current assets | 158,649,886 | 161,450,642 |
| Current assets | 137,133,026 | 124,862,876 |
| **Total assets** | **295,782,912** | **286,313,518** |
| **Equity and Liabilities** | | |
| Equity | **198,955,802** | **195,696,482** |
| Non current liabilities | 37,781,288 | 31,015,506 |
| Current liabilities | 59,045,822 | 59,601,530 |
| **Total equity and liabilities** | **295,782,912** | **286,313,518** |

**Tanzania Portland Cement PLC**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania.**
**Tel +255784108600 Fax: +255784108609**
**www.twigacement.com**
**Email: info@twigacement.com**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tanzania ina haki ya kuvuna mema SADC

**MKUTANO** wa 39 wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)unafanyika nchini ambapo tunatarajia viongozi wakuu 16 wa nchi na serikali za nchi hizo wanachama watahudhuria.

Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo yenye historia ya aina yake. Ni miongoni mwa nchi zilizokuwa mstari wa mbele katika ukombozi na mapambano dhidi ya ubaguzi na utawala dhalimu uliokuwa katika nchi kadhaa za kusini mwa Afrika.

Chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Tanzania iliongoza mapambano kusini mwa Afrika, baadhi ya viongozi kadhaa wa nchi zilizotawaliwa kwa mabavu walifika na kupewa mafunzo au hifadhi ya muda ili kujipanga vyema kwa mapambano.

Mara kadhaa baadhi ya viongozi wa nchi hizo ikiwamo Msumbiji hawakusita kubainisha jinsi ambavyo walijisikia huru wakiwa kwenye hifadhi zao kwa kuwa hata wananchi wa kawaida waliwapa ushirikiano mzuri.

Baada ya ukombozi wa nchi zilizokuwa katika ukoloni pamoja na ubaguzi wa rangi hususan Afrika Kusini, sasa SADC imekusudia kujitafutia maendeleo na ustawi wa jamii miongoni mwa nchi wanachama, ikiwa ni mtangamano wa kikanda.

Mtangamano huo una hatua tano, ambazo zinatajwa kuwa ni soko la pamoja, umoja wa forodha, umoja wa kiuchumi, eneo huru la biashara na shirikisho la kisiasa.

Nchi za Sadc zimejiwekea malengo ambayo ni n kufikia eneo huru la biashara ifikapo mwaka 2008, umoja wa forodha (2010), soko la pamoja (2015), umoja wa fedha (2016) na hatimaye kuwa na sarafu moja mwaka 2018.

Mkutano wa wakuu wa serikali na nchi umetanguliwa na maonyesho ya Nne ya viwanda SADC ambapo wafanyabiashara, wajasiriamali na wawekezaji walipata fursa ya kushiriki.

Maonesho hayo yamefuatiwa na mijadala mbalimbali ya kimaendeleo katika nyanja tofauti, ikiwamo uwezeshaji wa viwanda, kukuza soko la bidhaa na ubora wa bidhaa husika, huduma za maendeleo ya jamii, siasa na usalama.

Kutokana na mazingira yalivyokuwa kwenye maonesho hayo, ni wazi kwamba wananchi wengi hawakupata fursa ya kushiriki, lakini wale wachache walioshiriki wanaweza kufikisha jumbe mzuri kwa wenzao.

Kwa upande wa taasisi, tumejulishwa kuwa Bohari Kuu ya Dawa imepata jukumu la kununua dawa na kuzipeleka kwa nchi wanachama kulingana na makubaliano waliojiwekea.

Kiwanda cha kuzalisha viuadudu vya kuangamiza viluilui vya mbu nchini cha Tanzania Biotech Product (TBPL) tayari kimeanza kung'ara kwa nchi za SADC baada ya nchi hizo kutangaza nia ya kununua viuadudu hivyo.

Kuanzia leo tumaamini kuwa mambo mengi na makubwa yatafanyika kutokana na kuanza kwa vikao kadhaa kuanzia vya makatibu wakuu, mawaziri hadi kilele chake ambacho viongozi wakuu watakutana.


Miongoni mwa mambo yatakayofanyika ni kubadilishana nafasi za uongozi wa jumuiya, huku Rais John Magufuli akitarajiwa kukabidhiwa uenyekiri ataodumu nao kwa kipindi cha mwaka mmoja. Rais Hage Geingob wa Namibia anayemaliza muda wake ndiye atakabidhi kijiti kwa Rais Magufuli ambaye kwa sasa anashikilia nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa SADC.

Tunaamini kwamba Rais Magufuli ataiwakilisha vyema Tanzania, na ni matarajio yetu kwamba chini ya uongozi wake makini, kwa nafasi hiyo, SADC itapiga hatua kadhaa kutoka hapo ilipo na kusogea mbele.

Ni matarajio yetu kuwa baada ya mkutano huu, SADC itapaa kwa kasi ili kufikia malengo ambayo wanachama wamejiwekea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ajali ya Morogoro iturudishe kwenye maadili si vinginevyo

Na Raphael Kibiriti

**NIANZE** kwa kuungana na wananchi wenzetu wa mkoa wa Morogoro na wote walioguswa kwa namna moja au nyingine na msiba mzito uliolikumba taifa letu, kufuatia vifo vya Watanzania 71 kwa takwimu za hadi jana asubuhi.

Ni vifo vilivyotokana na ajali ya moto ya Agosti 10, baada ya gari lililokuwa limebeba petroli kupinduka eneo la Msamvu ambapo baadhi ya watu walilivamia na kufungua koki zake ili waibe mafuta hayo.

Katika mchakato huo usio halali, moto ulilipuka na kuwaunguza wote waliokuwa katika 'fursa' ya kuiba mafuta hayo.

Ni bahati mbaya kwamba, baadhi ya watu waliokuwa katika shughuli zao halali za kila siku nao wameathirika.

Muungwana anaungana na hatua zilizochukuliwa na serikali za kuwahudumia waliothirika na ajali hiyo, wakiwamo walioopoteza maisha.

Mbali na kuendesha operesheni ya kitaifa ya kuwahifadhi waliofariki, lakini kupitia kwa Rais John Magufuli, serikali imebeba gharama zote za kuwatibu majeruhi, huku ikitangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa.

Ni mengi yamezungumzwa kwa namna tofauti kuhusiana na kadhia hiyo kwa mtazamo chanya lakini pia mtazamo hasi.

Wapo wanaovinyooshea vidole vyombo vya ulinzi na usalama vyenye dhamana ya kuhakikisha kuna ulinzi na usalama wa maisha na mali za watu katika mazingira yote, yakiwamo yale yanayohusisha ajali mbalimbali kama hii iliyotokea.

Wanavinyooshea vidole kwamba havikutimiza wajibu wao na ndiyo maana kadhia hiyo ikatokea.

Wakati Muungwana akiungana na Rais Magufuli kwamba huu si wakati wa kunyoosheana vidole kulaumiana, bali kutoa kipaumbele kwa matibabu ya majeruhi, anadhani kuna somo kwa Watanzania la kuendelea kujifunza.

Kuendelea kujifunza kuwa 'utamaduni' usio wa kimaadili tunaozidi kuuendekeza kwa kasi ya ajabu wa kuvamia magari yanayopata ajali ili kuiba na si kutoa msaada, utazidi kutuangamiza tusipobadilika.

Imeripotiwa mara nyingi kwenye vyombo vya habari jinsi watu wanavyovamia na kupora mali za majeruhi wa ajali.

Na mbaya zaidi badala ya kutoa msaada, wengine wanadaiwa hata kufikia hatua ya 'kuwamaliza' kabisa majeruhi ili tu waweze kuwaibia mali walizonazo.

Muungwana ambaye anaishi eneo la Wazo Hill jijini Dar es Salaam ameshuhudia mara nyingi, jinsi magari yaliyofeli breki yanayokimbiliwa na watu.

Yanakimbiliwa si kwa ajili ya kwenda kutoa msaada katika mtelemko wa barabara ya Wazo kwa wanaoifahamu, ila kwenda kuiba mifuko ya simenti, gari itakapoanguka.

Si upande wa magari ya simenti tu, kuna matukio kwa mfano katika barabara ya Nelson Mandela inayopitisha magari yanayobeba mafuta kutoka ama kwenda kuchukua mafuta bandarini.

Kuna watu ambao hufungua koki ya magari hayo ili kukinga mafuta wakati mwingine wakitumia mifuko ya nailoni, katikati ya misururu ya magari.

Aidha, imeshuhudiwa namna ambavyo watu huvamia gari zilizopata ajali zikiwa na vinywaji kama bia na kuiba kreti za vinywaji, wengine 'wakipoza' makoo yao bila ya kujali kwamba huo ni wizi.

Mbali na bidhaa kama za petroli, barabara hizi husafirisha pia bidhaa kama kemikali za sumu na milipuko ambayo yote ni ya hatari.

Muungwana anasema ni somo la kuendelea kutoa funzo kwamba kuita ajali kama hizi kuwa ni 'fursa' ya kujineemesha kwa namna yoyote ile ni kinyume cha maadili ya kiasili ambayo kila binadamu ameumbwa nayo.

Maadili ya kujua chema na kibaya, kwamba haihitajiki kwa kweli hadi aje polisi ama ofisa yeyote wa serikali kumwambia mtu kuwa kitendo cha kuchukua dumu nyumbani kwake kwenda kuiba mafuta ya gari lililopata ajali hakikubaliki.

Wakati waathirika wa ajali hiyo wanaendelea kutibiwa, Muungwana anaasa Watanzania kurudi kwenye maadili na utamaduni wa kusaidia watu wanaopatwa na ajali, badala ya kuchukulia ajali kama fursa.

Anasema, siri ya mafanikio ni kufanya kazi halali, si vinginevyo.

# HABARI PICHA



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu Mkoa wa Dodoma wakishiriki Swala ya Eid El Haji iliyoswaliwa jana katika Uwanja wa Jamhuri. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waumini ya dini ya Kiislamu wakitakiana heri ya sikukuu ya Eid El Haji, baada ya kumalizika kwa swala, katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya viongozi na mawaziri wanawake pamoja na wananchi wakisikiliza hotuba iliyotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), katika sherehe za Baraza la Eid El Haji katika viwanja vya Langoni, Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo (wa pili kushoto), Mufti wa Tanzania Sheikh Abubakari Zuberi (kushoto) na viongozi wengine wakishiriki swala ya Idd El Haji, iliyofanyika kitaifa katika Viwanja vya Msikiti wa Kibadeni Chanika Zogo Hali, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Sheikh wa Mkoa wa Singida, Salum Mahami (kulia), akiongoza kuomba dua katika Swala ya Eid El-Haji, katika viwanja vya Shule ya Msingi Sumaye, mkoani humo jana. Kushoto ni Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu (Bakwata), Mkoa wa Singida, Burhan Mlau. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Alhajj Ali Mohamed Shein, akihutubia Baraza la Eid El Haji, katika viwanja vya Dole, Wilaya ya Magharibi A Unguja jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mikopo elimu ya juu kaa

INATOKA UK. 2

**KAULI YA WIZARA**

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu suala hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Willian Ole Nasha, alikiri kupokea malalamiko ya wanufaika kuhusu kuwapo kwa uonevu katika urejeshaji wa mikopo hiyo na kwamba wizara yake inaendelea kuyafanyia kazi.

Hata hivyo, Ole Nasha alisema baadhi ya changamoto zilizoibuka kuhusu urejeshaji wa mikopo hiyo, utatuzi wake unahitaji kurejea bungeni kufanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya Mwaka 2004.

"Tumesikia malalamiko na siyo kwamba hatujayapata, tumeyapata na tunayatolea ufafanuzi na kusambaza taarifa kwenye vyombo mbalimbali vya habari," alisema.

Ole Nasha alisema serikali ni sikivu na kwamba kwa sasa inafanya mapitio ya mfumo mzima wa mikopo hiyo ili kuangalia njia bora ya kutatua changamoto zote zilizopo.

"Tunahitaji kuendelea kutoa elimu ingawa inafahamika kwa sababu mkataba wa mikopo umeeleza kila kitu, tunaendelea kutoa elimu ili watu wafahamu zaidi na kila mwaka tunafanyia marekebisho mwongozo wa mikopo.

"Kuna mambo ya kisheria ambayo hatuwezi kuyafanyia marekebisho mpaka sheria ikabadilishwe bungeni, lakini yale ambayo yapo chini ya kanuni zetu tunafanyia marekebisho kila wakati tunapoona kuna haja ya kufanya hivyo," alisema.

Naibu waziri huyo alisema tozo ya asilimia sita imewekwa kwa lengo la kulinda thamani ya fedha ili kusaidia wanafunzi wengine wanaotaka kusoma kwa kupewa mkopo na Serikali.

"Tozo ya kutunza thamani inafanya ile thamani ya mkopo wako isipotee, yaani usiwe umekukopesha Sh. milioni moja na wewe uje urudishe milioni moja baada ya miaka saba, haitakuja kutusaidia, lengo la serikali siyo kukusanya fedha, bali kutunza thamani ya fedha," alisema.

Ole Nasha alibainisha kuwa uzoefu wa wizara yake unaonesha kuwa ukiacha miezi 24 iliyotolewa na HESLB kwa wanufaika kuanza kuhesabiwa muda wa kulipa deni, mdaiwa anaweza kumaliza deni lake ndani ya miaka 10 kama hatapigwa penalti.

"Utafiti unaonyesha kuwa inachukua miaka minne hadi 10 mnufaika kumaliza kulipa deni lake endapo ataanza kulipa kwa wakati," Ole Nasha alisema.

Hata hivyo, utafiti huo unakinzana na takwimu za urejeshaji mkopo za HESLB ambazo zinaonesha kuwa kati ya wanufaika 479,779 waliopatiwa mikopo hiyo tangu serikali ilipoanza kuitoa mwaka 1994, ni wanufaika 11,214 (asilimia 2.3) waliofanikiwa kumaliza kulipa madeni yao.

Pia, wanufaika wa mikopo hiyo waliozungumza na Nipashe wiki iliyopita, walidai wanufaika wengi wa mikopo hiyo walioanza kuilipa, wameshindwa kumaliza urejeshaji kutokana na deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka.

"Wito wetu ni kwamba ukichukua ule mkopo , tukijenga ustaarabu wa kulipa, inawezekana wanafunzi wote wanaoenda chuo kikuu, wanaohitaji mikopo wapate kwa sababu ni hela ambayo ipo kwenye mzunguko.

"Haimaanishi kwamba sisi kama wizara hatufanyii kazi changamoto zinazojitokeza, tukipata changamoto tunatoa elimu kuhusu hali ilivyo sasa na tukiona kuna haja ya kurekebisha, pale tunapoona tunaweza tunafanya, na mengine kama haya (malalamiko ya uonevu katika urejeshaji mkopo), inabidi turudi bungeni," Ole Nasha alisema.

Mara ya mwisho Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kufanyiwa marekebisho ilikuwa Novemba 2016, serikali ilipowasilisha bungeni muswada ambao pamoja na mambo mengine, ulipendekeza mnufaika wa mkopo arejeshe mkopo kwa makato si chini ya asilimia 15 ya mshahara wake wa kila mwezi badala ya asilimia nane iliyokuwa awali.

# Rais wa Afrika Kusini kuwasili

INATOKA UK. 3

kwa kutapeliwa na kuachwa na majeruhi moyoni mwao.

Alisema akiwa kama Mkuu wa Mkoa, hawezi kuwaongoza watu wenye kuumizwa hivyo atakwenda kuwashughulikia na kwamba kupitia mkutano huo wa SADC watapata uzoefu jinsi wao wanavyoshughulikia wanaume wa aina hiyo.

"Tuna mpango wa kukutana na kinadada wote walioumizwa na ahadi za kuolewa, lakini wakaachwa ili kujadiliana kwa kina namna gani ya kuwashughulikia wanaume hao, lakini pia tutajifunza kwa wenzetu wa SADC sheria zao zinafanyaje kuwashughulikia wanaume wadanganyifu," alisema na kuongeza:

"Lengo ni kuepusha kinadada wasiingie kwenye uhusiano wa kuumizwa, lakini pia itasaidia kuondoa ndoa za kimya kimya, wageni wetu watatuambia huko kwa Mfalme Mswati wanafanya utaratibu gani, Zimbabwe wanafanyaje ili tuone ni njia gani ya kuwaondoa kinadada wasiendelee kuumizwa," alisema Makonda.

Pia, Makonda alisema kuna mpango wa kuanzisha kanzi data ya ndoa zote zilizopo katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kupunguza utapeli wanaofanyiwa wanawake kwa kudanganywa kuolewa.

Wakati huo hui, Mkutano wa Mawaziri wa SADC unatarajiwa kuanza leo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, atakabidhiwa uenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa ngazi za mawaziri.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa pikipiki mpya zinazotarajiwa kutumiwa katika mapokezi ya viongozi na wakuu wa nchi na serikali wa SADC kwaajili ya kuhudhuria mkutano huo unaoendelea jijini Dar es Salaam, Prof. Kabudi, alisema serikali imekuwa ikiendelea na maandalizi mbalimbali ya mapokezi ya viongozi hao ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri yakiwamo magari na pikipiki na hoteli watakazofikia viongozi hao.

Pia Prof. Kabudi kwa niaba ya serikali, ameeleza kuridhishwa na kufurahishwa kwa namna vyombo vya habari nchini vinavyoripoti kizalendo mkutano unaoendelea wa SADC jambo ambalo limeongeza uelewa wa wananchi kuhusu Jumuiya hiyo na kuvitaka kuendelea kufanya hivyo katika masuala yote yanayohusu maendeleo ya nchi.



Mwendesha baiskeli akiwa ameisheheni magunia ya mkaa, katika eneo la Zogowali Chanika, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sababu zinazochangia

INATOKA UK. 4

kutoka Hospitali ya Mirembe Dk. Damas Andrea alisema kuwa zaidi ya asilimia 60 ya wagonjwa wa akili nchini huwa hawaendi hospitali bali kwa waganga wa kienyeji.

Alisema kuwa Takwimu zinaonyesha pia kuwa katika kipindi cha mwaka 2016 vijana 62,000 duniani walitaka kujiua kutoka na matatizo ya msongo wa mawazo (Sonona) na wengi wao ni kutoka nchi zinazo endelea ikiwemo Tanzania.

"Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa Tanzania ipo katika nchi kumi bora zinazoongeza kwa matukio ya kujiua kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo sonona," alisema Dk. Andrea.

Alisema kuwa magonjwa ya afya ya akili kwa asilimia 50 mengi yanatokea katika umri wa kuanzia miaka 14, ni umri ambao vijana wengi wamekuwa na changamoto mbalimbali kama vile matumizi ya dawa za kulevya kwa wingi.

"Magonjwa haya ya akili yapo katika umri wa rika tofauti tofauti kwa watoto, vijana pamoja na wazee, na kwa asilimia kubwa vijana wa umri huu wa miaka 14 hadi 19 wamekuwa katika wakati mgumu kutokana na matumizi ya dawa za kulevya," alisema.

# Eneo la maziko

INATOKA UK. 2

**WAFIWA WAFUNGUKA**

Nao baadhi ya ndugu wa watu walioopoteza maisha waliozikwa siku ya pili walizungumzia janga hilo la kupoteza ndugu zao.

Mzee Kassim Mzee aliyefiwa na mdogo wake, Issa Kasanda, aliyekuwa mpigadebe katika kituo kikuu cha mabasi cha Msamvu, alisema ndugu yake ni miongoni mwa waliopoteza maisha katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) alikopelekwa kwa matibabu.

Alisema alipata taarifa za kutoweka kwake baada ya kwenda nyumbani kwake usiku na alipofika Hospitali ya Morogoro alikoelezwa alikuwa amelazwa, akajulishwa alikuwa tayari amepelekwa Muhimbili alikopoteza maisha.

Katika eneo la Kichangani, nyumbani kwa Ramadhani Benjamin, (marehemu), mwandishi wa habari hizi alifika na kuzungumza na mkewe ambaye alisema alipata taarifa za kifo cha mumewe kupitia kwa mama yake, ambaye alifika nyumbani kwao akiwa analia, na alipohoji alimueleza kuhusu ajali hiyo ya moto.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, aliulizia taarifa za mumewe ambaye anafanya kazi kiwanda cha kufyatua matofali cha Simba ambacho kipo jirani.

Mwanamke huyo aliyeachwa akiwa na hali ya ujauzito wa mumewe, na mtoto mmoja, alipoulizia habari zake kwa kuwa aliachana naye tangu jana yake, usiku alipoagana naye kwenda kazini zamu ya ya usiku, aliambiwa mumewe alitoka baada ya kusikia ajali, na hakurudi, wakamtafuta miongoni mwa majeruhi hawakumuona, hadi walipopima vinasaba kupitia mwanaye na kubaini ni miongoni mwa waliokufa.

# Mbunge ajivunia mafanikio

**Na Mwandishi Wetu,** IGUNGA

MBUNGE wa Manonga wilayani Igunga mkoani Tabora, Seif Gulamali, ameeleza kuridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

Akizungumza na Nipashe mjini Igunga jana kuhusu ziara yake ya siku 23 jimboni iliyohusisha na vijiji vyote 65 vya kata 19 za jimbo hilo jipya, Gulamali alisema aliamua kufanya ziara hiyo ili kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema katika ziara yake hiyo alishuhudia mwitikio mkubwa wa wananchi kwenye mikutano, huku wengine wakilazimika kusimamisha msafara wake kumpa pongezi kwa kazi nzuri inayoendelea kufanywa na serikali ya awamu ya tano jimboni kwake katika nyanja zote ikiwamo elimu, miundombinu, maji, afya, kilimo na viwanda.

**Mwaka 2016, tulikuwa wa tisa, 2017 tulikuwa wa 10 na 2018 tukawa 10 tena. Na hii inatokana na kuhamasisha wanafunzi. Nimekuwa nikigharamia masomo ya wanafunzi wanaofanya vizuri jimboni.**

"Kwa kweli, kazi kubwa imefanyika Manonga. Mfano, tumeweza kufufua Kiwanda cha Pamba cha Manonga ambacho kilisimama kwa zaidi ya miaka 20, leo kimefufuka na kinafanya kazi mwaka wa pili sasa na kuongeza ajira kwa vijana huku pia kikiongeza ulimaji wa pamba jimboni," alisema.

Gulamali aliishukuru serikali ya awamu ya tano iliyo chini ya uongozi wa Rais John Magufuli kwa kuboresha miundombinu, akibainisha kuwa jimbo lake limepatiwa Sh. milioni 700 toka serikalini ili kujenga daraja ma Mto Manonga.

"Kwa sasa, makandarasi wako eneo la mradi, ilikuwa ni kilio cha muda mrefu toka awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu ya nne lakini hapa tumefanikiwa huku miundombinu ya barabara ikizidi kuimarishwa jimbo zima," alisema.

"Miradi ya maji kwa vijiji vya Mwisi na Kalemela nayo inatekelezwa kwa Sh. milioni 341 zinazotumika kujenga miundombinu. Pia Sh. milioni 560 zitatumika kwa mradi wa Nguriti na Mwamala huku mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ukiendelea kuingia jimboni," alisema.

Kuhusu sekta ya afya, Gulamali alisema wamefanikiwa kupata Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Simbo ambacho kimekamilika huku akinunua gari la wagonjwa kwa Sh. milioni 120 kwa ajili ya kituo hicho.

"Kituo cha Afya cha Choma kimeboreshwa na zahanati mbalimbali zikipokea Sh. milioni 10 kila moja kutoka mfuko wa RBF kwa ajili ya uboreshaji. Pia tunajiandaa kufungua zahanati mpya kama za Itale, Bugingija, Chapela na Imalilo," alisema.

Katika sekta ya elimu, Gulamali alisema wamefanikiwa kuongeza ufaulu wa wanafunzi kutokana na hamasa anayoitoa ya kugharamia masomo ya wanafunzi wanaofaulu vizuri jimboni kwake.

Alisema kwa miaka mitatu mfululizo, Wilaya ya Igunga imekuwa miongoni mwa halmashauri 10 bora kati ya halmashauri zaidi ya 180 Tanzania nzima katika mitihani ya taifa.

"Mwaka 2016, tulikuwa wa tisa, 2017 tulikuwa wa 10 na 2018 tukawa 10 tena. Na hii inatokana na kuhamasisha wanafunzi. Nimekuwa nikigharamia masomo ya wanafunzi wanaofanya vizuri jimboni.

"Mwaka 16 tulisomesha wanafunzi 50 jimbo zima, mwaka uliofuata wanafunzi 150, mwaka jana (2018) wanafunzi 245 na mwaka huu ufaulu umeongeza umefikia 300 na wote wanalipiwa kupitia Seif Gulamali Foundation.

"Mwaka huu tumepata mwanafunzi anayesoma shule ya kata katika Jimbo la Manonga, amepata Daraja la Kwanza kwa pointi nane (A sita na B) na ameongoza wilaya nzima.

"Hii yote ni hamasa niliyoifanya na wanafunzi wote sasa wanapambana wafaulu kwa sababu wanao uhakika wa kusomeshwa na mbunge wao," alisema.

Gulamali alisema katika ziara yake hiyo, pia alifuatilia utekelezaji wa ahadi ya CCM ya kuhakikisha Shule za Sekondari Ziba, Mwisi na Choma zinakuwa na kidato cha tano na sita, akibainisha kuwa tayari Ziba imepokea wanafunzi wa kidato cha tano mwaka huu.

Alisema Shule za Sekondari Mwisi na Choma ziko katika maandalizi ya kupokea wanafunzi hao mwakani, hivyo kulifanya jimbo hilo jipya kuwa na shule tatu za kidato cha tano na sita.

Wilaya nzima ya Igunga kwa sasa ina shule tatu zinazopokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita (mbili zikiwa Jimbo la Igunga Mjini).

Gulamali pia alisema serikali ya awamu ya tano pia imefanikiwa kuongeza idadi ya shule za kata jimboni huko kwa kujenga shule za Ibologero, Tambarale, Mwamala, Buhekela, Ugaka, Manonga na Seif Khamis Gulamali.

## Mwauwasa yaanika sababu ongezeko la maji

**Elizabeth Faustine na Neema Emmanuel,** MWANZA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), imesema sababu ya ongezeko la gharama na tozo za maji ni kuboresha huduma za majisafi na uondoaji majitaka kwa kutatua changamoto zilizopo kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Mwauwasa, Mhandisi Antony Sanga, wakati akifungua mkutano kati ya mamlaka hiyo na wanahabari mkoani Mwanza ulioratibiwa na Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC) uliolenga kuimarisha mahusiano na utendaji kazi baina ya taasisi hizo.

Mhandisi Sanga alisema, baadhi ya maeneo yamekuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji, hivyo wamekusudia kuboresha kwa kujenga miradi mipya yenye kuongeza mtandao wa usambazaji na kuyafikia maeneo hayo, ili lengo hilo litimie ndio sababu ya kuongeza gharama za ankra ya maji kwani mamlaka hiyo inajiendesha kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato.

"Hatubadilishi bei ya maji kwa ajili ya maslahi ya watumishi, tumelenga kuboresha huduma na miundombinu ya maji pamoja na kutatua changamoto za upatikanaji wa maji kwenye maeneo mengi hususani yale ya milimani na pembezoni," alisema Mhandisi Sanga.

Alisema, mara ya mwisho Mamlaka ya Udhibithi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), iliidhinisha mabadiliko ya bei za maji Mwauwasa takribani miaka minne iliyopita, kwa kipindi chote wameendelea kutumia bei zile zile licha ya kuwapo mabadiliko ya gharama mbalimbali za watoa huduma.




Mbunge wa Temeke, Abdallah Mtolea, akizungumza wakati akizindua Taasisi ya Open Mind na Kongamano la Vijana Wajasiriamali, jijini Dar es Salaan jana, ikiwa sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani. Kulia ni Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Abel Otieno 'MC Rhevan' na Mtaalamu wa Fedha, Liliani Mbilinyi. **PICHA: JOHN BADI**

## Wanahisa TCCIA waazimia ujenzi viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WANAHISA wa Kampuni ya TCCIA Investment PLC wameazimia kujenga viwanda ikiwa ni sehemu ya uwekezaji wa hisa za wanachama wake sambamba na azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo2025.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mkutano wa 14 wa wanahisa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni hiyo, Fortunatus Magambo, alisema wajumbe katika mkutano wameazimia kufanya uwekezaji zaidi sekta ya viwanda ili kuongeza faida ya kampuni na hatimaye ongezeko la gawio kwa wanahisa.

"Uwekezaji kwenye sekta ya viwanda ni muhimu sana kwa nyakati hizi kwani kutapanua wigo wa kupata faida katika uwekezaji na hivyo wanahisa kunufaika zaidi kupitia gawio," alisema Magambo.

Alisema kama wasimamizi na washauri wakuu wa menejimenti katika kuendeleza kampuni watahakikisha kuwa malengo yote waliyojiwekea katika kuifanya kampuni ya TCCIA Investment PLC yanatekelezwa na kuleta matokeo chanya.

"Serikali ya awamu ya tano imeelekeza nguvu kwenye ujenzi wa viwanda hivyo kama kampuni ni lazima tujielekeze huko ili kuunga mkono juhudi za serikali na pia kuongeza mapato ya kampuni," alisema Magambo.

Alisema malengo ya kampuni ni kuongeza faida kupitia uwekezaji mbalimbali hasa katika sekta ya viwanda ili kufanya kampuni kupata faida na kupelekea gawio kwa wanahisa kuongezeka hali itayoamsha hamasa kwa wananchi kuwekeza katika mfumo ya hisa.

Mwenyekiti huyo aliwataka Watanzania kujenga utamaduni wa kuweka katika hisa kwenye masoko ya hisa kama dhamana kubwa ambayo itakuja kuwanufaisha baadaye kupitia magawio pamoja na kuuza hisa zake pale wanapohitaji.

Afisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Donald Kamori, alisema lengo la mkutano huu wa mwaka ni kukutana na wanahisa na kupeana taarifa za kiutendaji na pia kutoa mapendekezo juu ya hatua mbalimbali za kiutendaji.

"Kubwa ni kupokea taarifa za bodi ya wakurugenzi juu ya utendaji mzima wa kampuni kwa mwaka na kutathmini mafanikio na changamoto mbalimbali ili kuleta ufanisi katika utendaji na kupelekea faida ya gawio kuongezeka," alisema Kamori.

Mkutano wa 14 wa wanahisa ulilenga pia kutazama changamoto na kutoa mapendekezo ambayo yangeboresha utendaji kazi wa kampuni katika kukuza mitaji na kuchangia faida kuongezeka.

# Tanzania kuanzisha utalii wa kumbi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inajipanga kujenga ukumbi mkubwa wa mikutano utakaoweza kutumika kwa ajili ya mikutano mikubwa ya kimataifa ili kuongeza zao la utalii nchini.

**Dar es Salaam imechangamka, hoteli zimejaa wageni, magari ya kukodi na biashara zingine zimepata wateja kipindi hiki cha mkutano.**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Aldof Mkenda, amesema ukumbi huo utakaojengwa Dar es Salaam utavutia mikutano mikubwa ya kimataifa na kuongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jana alipotembelea Makumbusho ya Taifa kwa lengo la kujionea maandalizi ya kupokea wageni wa SADC, wanaopanga kutembelea Makumbusho ya Taifa.

"Kumbi za mikutano ni moja ya zao la utalii kwa sababu watu wanapokuja kushiriki mikutano ya kimataifa ni watalii kwa kuwa wanapata fursa pia za kiutalii," alisema.

Vile vile, alisema Tanzania ina kila sababu ya kuwa na ukumbi mkubwa wa mikutano utakaowezesha mikutano mikubwa ya kimataifa kufanyika kwa sababu ya sifa ilizonazo.

Serikali ya awamu ya tano imekamilisha ujenzi wa jengo la abiria (Termina III) katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere ambao una uwezo wa kuhudumia abiria zaidi ya milioni sita kwa mwaka.

Vile vile, serikali imeliwezesha Shirika la Ndege la Tanzania (ATC) ili liweze kufanyakazi yake vizuri na kununua ndege mpya ambazo zinaenda mpaka nje ya nchi.

"Haya yote ni mazingira wezeshi kwa mikutano ya kimataifa," alisema Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii.

Prof. Mkenda alisema mkutano wa SADC ambao unafanyika Tanzania umetoa fursa kubwa za kitalii na uchumi kwa Tanzania.

"Dar es Salaam imechangamka, hoteli zimejaa wageni, magari ya kukodi na biashara zingine zimepata wateja kipindi hiki cha mkutano," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo na kuonyesha ukarimu kwa wageni hao.

Alisema pamoja na kupata fursa za kiuchumi Tanzania inataka kuonyesha mchango wake katika ukombozi wa Afrika na hayati Mwalimu Julius Nyerere alikuwa mwasisi wa ukombozi wa nchi za Afrika.



Dereva wa bodaboda akiwa ameisheheni magunia ya mkaa katika eneo la Goba, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wataalamu elekezi wa mazingira wanolewa

**Na Enock Charles**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kwa kushirikiana na Idara ya Giografia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wameendesha mafunzo ya siku tano kwa wataalamu elekezi lengo likiwa kuweka sawa mambo ya msingi yanayohusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA).

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kufunga mafunzo hayo Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema makubaliano ya kuwaandaa wataalamu elekezi kati ya Baraza na Idara ya Giografia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itaongeza tija hasa kipindi hiki ambapo serikali imeazimia kujenga uchumi wa viwanda.

"Makubaliano ya taasisi hizi mbili katika kutoa mafunzo kwa wataalamu elekezi yatasaidia sana kupunguza ucheleweshaji wa kufanya Tathmini ya

Athari kwa Mazingira (TAM) hali inayoathiri sana uwekezaji, hivyo kurudisha nyuma juhudi za serikali za kuleta wawekezaji," alisema Dk. Gwamaka

Dk. Gwamaka aliongeza kuwa mafunzo hayo yamekuja katika wakati muafaka hasa ikizingatiwa kuwa kipaumbele cha serikali ya awamu ya tano ni ukuaji wa viwanda ili kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025.

"Azma ya viwanda itaambatana na mabadiliko chanya na hasi kwa nchi yetu kama historia inavyoeleza kwa baadhi ya nchi, hivyo ni lazima kuwa na miongozo thabiti ya kimazingira ikiwamo uhuishaji wa masuala ya mazingira bila kuathiri wimbi la wawekezaji walioamua kuja kuwekeza hapa nchini," alisema.

Mkuu wa Idara ya Geografia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Opportuna Kweka, alipongeza makubaliano ya taasisi hizo mbili kwani yatasaidia kuharakisha ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

"Nalipongeza Baraza pamoja na Chuo Kikuu Dar es Salaam kwa namna walivyoafikiana kuanzisha programu hii ambapo itasaidia kurahisisha ufanywaji wa TAM hali itakayoongeza idadi ya wawekezaji hapa nchini," alisema Dk. Kweka.

# TBS yabaini nondo zisizo na ubora sokoni

**Na Joseph Mwendapole**

UKAGUZI wa kushtukiza uliofanyika maghala ya vifaa vya ujenzi jijini Dar es Salaam umebaini kuwapo kwa baadhi ya nondo zinazozalishwa na baadhi ya viwanda zisizokidhi viwango vya ubora vilivyoainishwa kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi huo uliendeshwa wiki iliyopita na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), kwenye maghala ya kuuza nondo yaliyopo Buguruni, Mbagala, Kariakoo na Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ukaguzi huo mwishoni mwa wiki, Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Ramadhan Shija, alisema hatua hiyo inalenga kujiridhisha kama wazalishaji wa nondo viwandani wanafuata matakwa ya viwango husika pamoja na kutoa elimu kwa umma.

Shija alisema kwenye ukaguzi huo wamebaini baadhi ya nondo ni fupi kulingana na kiwango husika.

"Nondo nyingine tumebaini kuwa ni fupi, kwa kuwa badala ya kuwa na urefu wa futi 38 zina urefu wa futi 37.6, hivyo kuna udanganyifu unaofanyika," alisema Shija.

Kwa upande wake, Mkaguzi Mwandamizi wa TBS, Donald Manyama, alisema ukaguzi wao ulilenga kujua urefu wa nondo na kipenyo.

Alisema kupitia ukaguzi wao wamebaini baadhi ya nondo zinafikia kipenyo husika na zingine hazifikii. Kwa mujibu wa Manyama, baada ya kubaini kasoro hizo kazi inayofuata ni kwenda kwa wazalishaji na kuwaeleza kuhusu kasoro walizobaini ili wazirekebishe vinginevyo watachukuliwa hatua za kisheria.

Pia, Manyama alisema kasoro walizobaini kwenye baadhi ya nondo zinawasukuma kufanya ukaguzi huo nchi nzima na kutoa elimu kwa umma, umuhimu wa kuhakikisha bidhaa wanazotaka kununua zinakidhi vigezo kwa kuonyeshwa nyaraka husika na wazalishaji au kufika ofisi za shirika hilo kupata ushauri.

# Meya awawakia wanaohujumu mapato

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MSTAHIKI Meya wa Jiji la Arusha, Karisti Lazaro, ameitaka halmashauri ya jiji hilo kuwakamata na kuwatia pingu watumishi wote watakaoonekana wanahujumu mapato ya halmashauri hiyo.

Alitoa agizo hilo juzi kwenye kikao cha robo ya mwisho ya mwaka 2018/19 cha Baraza la Madiwani, alipokuwa akimpongeza Mkurugenzi wa jiji hilo, Dk. Maulid Madeni, kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato na hatua anazozichukua za kuwakamata watumishi wote wa halmashauri hiyo, wanaojihusisha na uhujumu wa mapato .

Alisema baraza hilo linamuunga mkono kwa hatua hizo anazozichukua za kuwabana watumishi wasio waadilifu, ambao ni mafisadi na kuongeza kwamba hata kama kuna madiwani ambao wanashirikiana na watumishi wasio waadilifu nao wachukuliwe hatua.

Alimesema kuwa Mkurugenzi ameziba mianya, lakini atambue kuwa hivyo ni vita kubwa ila asiogope kwa kuwa baraza hilo linamuunga mkono kwenye vita dhidi ya maofisa wote wanaohujumu halmashauri na wanataka wapigwe pingu.

"Mkurugenzi wetu usiogope hii ni vita ila sisi tupo nyuma yako na tunataka wanaohujumu halmashauri yetu wapigwe pingu," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Jiji, Dk. Maulid Madeni, alisema halmashauri hiyo imechangia Sh. milioni 140 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa barabara unaofanywa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) lengo likiwa kuzifanya bara bara zote za jiji kuwa za lami.

Alisema halmashauri haiwezi kujiondoa kwenye masuala ya utengenezaji wa barabara, ndio maana imetoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kuzijenga na kusisitiza kuwa Tarura licha ya kuondolewa, lakini inawajibika kwa halmashauri hiyo.

Madiwani wakichangia katika baraza hilo walisema kuwa Tarura tangu waondolewe halmashauri, wamekuwa huru, hawatoi ushirikiano kwa madiwani na wamekuwa na urasimu.

# Wahimizwa kusaidia makundi yasiyojiweza

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WATANZANIA wametakiwa kujenga tabia ya kusaidia makundi yasiyojiweza hususani watoto yatima wanaokabiliwa na changamoto za kimaisha, ili waweze kufikia malengo waliyojiwekea kama watu wengine.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Elimu wa Shule za Msingi wa Jiji la Arusha, Sarah Mwangasa, wakati alipokuwa katika hafla fupi ya ugawaji wa msaada wa sare za shule, mabegi na vyakula uliotolewa na kikundi cha kijamii cha Friends of Batuli, kwa wanafunzi yatima wanaosoma katika shule za msingi Osunyai na Sombetini katika Halmashauri na Jiji la Arusha.

Mwangasa alisema wapo watoto wengi wasiojiweza wanaosoma katika shule 48 za Jiji la Arusha ambao wanakabiliwa na changamoto za kukosa mahitaji muhimu ya kimaisha ili wafanikiwe kufikia malengo ya kielimu.

**Natoa wito kwa jamii kuona umuhimu wa kujitolea kusaidia jamii kadiri wanavyobarikiwa na Mwenyezi Mungu ili watoto hawa wafanikiwe kufikia malengo yao.**

"Natoa wito kwa jamii kuona umuhimu wa kujitolea kusaidia jamii kadiri wanavyobarikiwa na Mwenyezi Mungu ili watoto hawa wafanikiwe kufikia malengo yao," alisema.

Awali, msemaji wa kundi la Friends of Batuli, Mwalimu Batuli Kisaya, alisema kundi hilo limeanzishwa mahususi kwa lengo la kusaidia jamii hususani watoto yatima na wenye mahitaji maalumu, kupitia michango yao.

Alisema kuwa kundi hilo limeguswa na watoto yatima wanaosoma katika shule hizo, baada ya kubaini kuwa wanakabiliwa na changamoto ya uhitaji wa vitendea kazi vya shuleni na kuamua kuhamasishana kuwachangia watoto hao.

"Kundi letu limejikita kuhamasisha jamii vitendo ili kusaidia makundi maalumu, kwa ajili ya kuwawezesha na wao waweze kupata faraja na kuishi kama watoto wengine wanaolelewa na wazazi wao," alisema Batuli.

Alisema kikundi hicho, kiligawa msaada wa mabegi ya shule, sare za shule na vyakula kwa wanafunzi wapatao 59 na msaada huo umegharimu Sh. milioni 1.5.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi waliopatiwa msaada huo, Robert Jacob na Jeremiah Daniel, kutoka shule za msingi Osunyai na Sombetini, walishukuru kwa msaada huo na kuomba Watanzania kuwakumbuka makundi maalumu yenye mahitaji kama wao.



Wafanyakazi wa kampuni ya Mbegu ya Kibo Seed, wakifurahia kombe la mshindi wa kwanza wa kampuni za Mbegu Kanda ya Kaskazini, ushindi walioupata wakati wa maonyesho ya Nanenane, Kanda ya Kaskazini, yaliyomalizika kwenye viwanja vya Themi Arusha wiki iliyopita. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wakulima, wafugaji Kanda ya Kaskazini kupima kisasa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKULIMA na wafugaji wa Kanda ya Kaskazini wametakiwa kulima kilimo cha kisasa ili wapate mavuno mengi yenye tija kwao na taifa, ili kupata malighafi kwaajili ya viwanda na kukuza uchumi.

Akizungumza jana kwenye maonyesho ya Nanenane Kanda ya Kaskazini yaliyomalizika kwenye viwanja vya Themi jijini hapa Agosti 12, mwaka huu, Mratibu wa mauzo wa kampuni ya mbegu ya Kibo Seed, Hassan Kimweri, alisema anawaomba wakulima na wafugaji kulima kwa kutumia kanuni bora za kilimo cha kisasa ili wavune mavuno mengi na bora.

Alisema endapo wakulima na wafugaji watapata mazao bora wataweza kuuza nje ya nchi baada ya kuandika na kupata fedha za kigeni.

"Maendeleo ya viwanda yanayotamkwa kila siku na serikali ya awamu ya tano yanategemea sana malighafi bora na za kutosha kutoka kwa wakulima na wafugaji, sasa tusipolima na kufuga kwa kutumia mbinu bora na za kisasa za kilimo itakuwa ndoto, tutafaulu tukilima kisasa na kusikiliza wataalamu wa kilimo na kutumia mbegu bora," alisema Kimweri.

Alisema viwanda vinavyoendelea kujengwa vinahitaji kwa wingi malighafi kama za kusindika sharubati (juisi), nyanya za kopo, matikiti maji, mahindi kwaajili ya unga na vyakula vya mifugo, nyama bora za ng'ombe na mbuzi pamoja na mbogamboga.

Kimweri alisema wakulima hawana budi kuamka usingizini na kuziendea benki zinatoa mikopo ya kilimo na ufugaji ili kupata pembejeo bora ikiwamo mbegu bora.

Alisema wakulima na wafugaji ni kivutio cha watalii kwa kuwa wanapotembelea hoteli za kitalii wanategemea mazao bora ya wakulima kutoka mashambani kwaajili ya mlo zikiwamo mboga, matunda na nyama.

"Wakulima wanatakiwa kwakweli kubadilika na kuwa na mtazamo chanya kwa kuacha kilimo cha kizamani, wanategemewa na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, maana asilimia 71 ya Watanzania ajira zao zipo kwenye kilimo na ufugaji, sasa tusipobadilika tutachezea uchumi wetu tu," alisema Kimweri.

Alisema Kampuni ya Kibo Seed Co. imeshinda nafasi ya kwanza kwa kampuni ya mbegu ya Kanda ya Kaskazini, kwenye maonyesho ya Nanenane ya mwaka 2019 kutokana na mbegu bora wanazotoa ambazo zimekuwa mkombozi mkubwa kwa wakulima kwa kuwapatia mavuno mengi na bora.

Pia, wamekuwa na wataalamu wanaotembelea wakulima wanapokuwa wameanza msimu wa kilimo na kuwafundisha kanuni bora za kilimo.

Kimweri alisema kampuni yake katika maonyesho ya Nanenane mwaka huu, imealika vikundi vya wakulima kutoka Mwanza, Singida na Tanga kuja kujifunza na kupata uzoefu wa wakulima na kampuni zingine za mbegu.

Alitaja mbegu zinazotumiwa na wakulima sehemu mbalimbali nchini, kuwa ni za mahindi, vitunguu, nyanya, mbegu za majani ya ng'ombe na mbogamboga.

# Ashauri kuwapo kampeni dhidi ya ugonjwa wa ini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Kibosho iliyopo Moshi Vijijini, Dk. John Materu, ameishauri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuanzisha kampeni maalum ya kitaifa itakayotumika kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara na tiba dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini (Hepatitis B).

Kwa mujibu wa Dk. Materu, iko haja kwa serikali kuelekeza nguvu zaidi vijijini kwa kutoa elimu kuhusu ugonjwa huo hasa kutokana na wananchi wengi kutokuwa na uelewa juu ya ugonjwa wa homa ya ini.

**Elimu zaidi kuhusu ugonjwa wa homa ya ini inahitajika ili kuwakinga wananchi na ugonjwa huo, kwa kuwa endapo wagonjwa watapatiwa chanjo na tiba mapema ugonjwa huo unatibika katika hatua za awali.**

"Bado kuna idadi kubwa ya wananchi vijijini hawana uelewa kuhusu ugonjwa wa homa ya ini, kuna kila sababu sasa Wizara ya Afya ikaja na mkakati maalum au kampeni maalum ya kutoa elimu juu ya huu ugonjwa ambao unaonekana kuwa tishio,"alisema.

Alisema elimu zaidi kuhusu ugonjwa wa homa ya ini inahitajika ili kuwakinga wananchi na ugonjwa huo, kwa kuwa endapo wagonjwa watapatiwa chanjo na tiba mapema ugonjwa huo unatibika katika hatua za awali.

Ugonjwa huo unasababishwa na vitu mbalimbali ikiwamo virusi vya Hepatitis B na C na maambukizi mengine ya bakteria, fangasi (kuvu) na matumizi ya pombe kali ambayo yanachangia kuleta shida hiyo.

"Homa ya ini ni tofauti na ule ugonjwa wa manjano, tunachanganya, watu wanafikiri mara nyingi kwamba maambukizi ya Hepatitis B au C ambayo inaleta shida kwenye macho yanakuwa na manjano, kwamba ile homa ya manjano ndio homa ya ini.

"Sio kila mtu mwenye manjano kwenye mapafu yake kwamba ana maambukizi ya virusi vya Hepatitis B au C, kuna vyanzo vingine vingi vinaweza kusababisha manjano kwenye macho ikiwamo saratani ya kongosho na magonjwa mengine ya virusi, ni tofauti. Kitu kingine kinaweza kuleta madhara ni dawa ambazo mtu anatumia anaweza kupata manjano kwenye macho yake."

Duniani kote watu wanaoishi na virusi vya Hepatitis B, wako milioni 257, kulinganisha na watu milioni 37 ambao wanaishi na virusi vya Ukimwi. Kwa Tanzania ukubwa wa maambukizi ni asilimia 4.5 licha ya Tanzania kujitahidi kutoa chanjo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo cha Uuguzi Kibosho, Devotha Shayo, akizungumzia huduma zinazotakiwa kutolewa kwa wagonjwa wanaopata ugonjwa huo, aliwataka wauguzi kuwa na lugha nzuri kwa wagonjwa ikiwa ni pamoja na kutoa huduma bora na elimu ya kujikinga na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akimkabidhi tuzo Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Kaskazini wa Vodacom Tanzania, Brigita Stephen, baada ya kampuni hiyo kuibuka mshindi wa kampuni bora upande wa mawasiliano kanda hiyo katika maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika jijini Arusha. Kushoto kwa Ulega ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (mwenye kofia). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kilimanjaro yatajwa kinara matukio ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKOA wa Kilimanjaro unatajwa kuwa miongoni mwa mikoa 10 nchini ambayo ni kinara wa matukio ya ukatili na unyanyasaji wa wanawake na watoto wa kike.

Kwa mujibu wa Ofisa Ustawi wa Jamii wa Manispaa ya Moshi, Magreth Reuben, kundi la watoto wa kiume pia liko katika hatari ya kuathiriwa na vitendo hivyo kutokana na viashiria na idadi ya matendo ya kinyama yanayojitokeza hivi sasa.

Hayo yamo katika taarifa yake aliyoitoa, wakati akizungumza na wanaharakati wanaounda jukwaa la mashirika yasio ya kiserikali mkoani Kilimanjaro.

Alisema matukio makubwa kwa sasa ni ubakaji, ulawiti na ngono zembe kwa watoto wenye umri mdogo.

Pia, aliyataka mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa huduma katika jamii kwa asilimia 80 kutenga bajeti za kuhakikisha yanawafikia jamii kwa karibu na kutoa elimu za kufichua vitendo viovu vinavyofanyiwa watoto pamoja na wanawake sehemu wanazoishi.

Katika mkutano na jukwaa hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi, alisema halmashauri hiyo kwa sasa ndiyo inaonekana kuwa kinara wa matukio ya ukatili.

Kutokana na kasi ya matukio ya ukatili, Mwandezi ameyataka mashirika hayo kutoa elimu kwa jamii na kufuatilia kwa karibu kesi za unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ambazo zinawagusa wanawake na watoto.

Nao baadhi ya wanaharakati Mkoa wa Kilimanjaro wakitoa maoni yao katika jukwa hilo, walikiri kuwapo kwa matukio ya ukatili na kwamba changamoto kubwa wanazokutana nazo katika kukabiliana na matukio hayo ni pamoja na kesi nyingi zinazopelekwa mahakamani kumalizika kiaina, baada ya ndugu na jamaa kurudisha kesi hizo nyumbani.

# Wawekezaji wavutiwa sekta ya mifugo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MCHAKATO wa kuwaanda Watanzania kuzalisha kwa wingi malighafi ya viwandani wakati Tanzania ikielekea katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, umeanza kuwavutia wawekezaji wa sekta ya mifugo na mazao yake kuwekeza kulingana na mahitaji ya soko.

Kampuni ya Match Maker Tanzania ambayo inafanya kazi kwa karibu na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), linaloendesha mradi wa faida maziwa kwa wafugaji wa wilaya za Hai na Siha, mkoani Kilimanjaro, imeeleza nia yake ya kuendelea kuwawezesha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kufuga kulingana na mahitaji ya masoko la maziwa ndani na nje ya nchi.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu, Mkurugenzi wa Kampuni ya Match Maker, Peniel Uliwa, ameeleza kuwa mpango wa huo una lenga kuchochea ajira, ustawi endelevu wa jamii na kufungua fursa za upatikanaji wa malighafi ya viwandani kupitia sekta ya mifugo na hasa ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa.

"Kimsingi tunaendelea kuwawezesha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kufuga kulingana na mahitaji ya masoko la maziwa ndani na nje ya nchi kwa kuwahimiza vijana kujiunga katika vikundi ili iwe rahisi kupata fursa za mikopo zitakazowasaidia kupanua wigo wa miradi yao ya kiuchumi.

"Yako mambo mengi sana yanaweza kusimamiwa na wadau wengine wanaoweza kuisaidia Serikali ya Tanzania kufikia ndoto zake, mfano ni kuboresha mazingira na usimamizi wa uwekezaji wa sekta binafsi hasusani viwanda vya kusindika maziwa, nyama, ngozi, samaki, mafuta ya kula, madawa na vifaa tiba, vyakula vya binadamu na mifugo."

Alisema moja ya mambo ambayo hivi sasa wanayakazia wanapokutana na wananchi na hasa wafugaji ni ubora wa uhifadhi wa malisho mabichi ya mahindi kwa ajili ya chakula cha mifugo maarufu kama sailage.

Ubora katika uhifadhi wa malisho hayo, husaidia kuruhusu kuhifadhi karibu viinilishe vyote vilivyo kwenye mimea ambavyo vinatajwa kuongeza tija ya maziwa kwa asilimia 15.

Wakati wadau hao wakihimiza pia matumizi ya teknolojia kwenye tasnia ya maziwa, baadhi ya wataalam wa mifugo akiwamo Marijan Kizigha wametaka kuwapo na njia mbadala ya kufikia ndoto hizo kwa serikali kuainisha sera na mikakati ya kuongeza mapato.

Alizitaja njia hizo kuwa ni kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyopo hususani katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki, kuongeza wigo wa kodi kwa kurasimisha sekta isiyo rasmi, kuboresha mazingira ya uwekezaji na urasimishaji ili kuvutia biashara na uwekezaji ukiwamo.

Nyingine ni kuboresha miundombinu, vivutio vya kodi, sera thabiti zisizobadilika mara kwa mara, upatikanaji wa ardhi na uwapo wa taratibu za kisheria na usimamizi bora pamoja na kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 13, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## JE, WAJUA?



Ukurasa 18

## Ethiopia yapanda miti milioni 350 kwa saa 12

Ukurasa 15



## 'Tunapress bolt aina zote' ni Kiswahili au hapana?



# MFUMO WA UDHIBITI MWENDO WA MABASI NA SARAKASI ZAKE

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI

## VING'ORA NA VIMULIMULI BINAFSI, MARUFUKU BARABARANI




Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), David Misime.
**PICHA: JESHI LA POLISI**

KATIKA siku za hivi karibuni kumejitokeza tabia ya baadhi ya madereva wa vyombo vya moto yaani, magari, bajaji na pikipiki kufunga taa za vimulimuli au za rangi rangi, taa zenye mwanga mkali (spot light) na kufunga ving'ora kwenye magari ya kiraia au watu binafsi na pikipiki zote za kiraia jambo ambalo ni kinyume na sheria ya kanuni za usalama barabarani.

Tabia hiyo ilimkera Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Lazaro Mambosasa ambapo Agosti 5, 2019 alitoa katazo la kupiga marufuku magari, bajaji na pikipiki binafsi katika Mkoa wa Dar es salaam kutumia ving'ora, taa za rangirangi na vimulimuli.

Kutokana na kujitokeza kwa baadhi ya watu walioamua kufunga vimulimuli na ving'ora na kuvitumia wawapo barabarani, hivyo kusababisha usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara hapa nchini, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), David Misime naye alitoa ufafanuzi.

Alitoa ufafanuzi kwa kuweka msisitizo kuwa Jeshi la Polisi nchini linaelekeza katazo hilo si kwa Mkoa wa Dar es salama tu, bali ni kwa nchi nzima.

Madereva hupenda kufunga vifaa hivyo ili waweze kupewa kipaumbele wawapo barabarani kwa kujua au kwa kutofahamu kuwa ni kinyume na sheria, kanuni na taratibu zilizopo jambo ambalo si sahihi.

Aliongeza kuwa, kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani sura ya 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002 kifungu cha 39 B (I) na (2) kinafafanua juu ya matumizi ya ishara ikiwepo ving'ora na vimulimuli.

Sheria hiyo imeeleza pale dereva atakapoona kuna ulazima wa kutoa tahadhari au kuzuia hatari dhidi ya watumiaji wengine wa barabara sheria hiyo imeendelea kueleza dereva hatatumia ishara hizo kwa nia yeyote zaidi na ilivyoelezwa katika kifungu hicho kidogo cha kwanza na wala haruhusiwi kutumia ishara hizo kwa muda mrefu zaidi ya mazingira yaliyopo yanayomlazimu kutoa tahadhari.

Aidha, Kwa mujibu wa sheria hiyo ya Usalama barabarani kifungu 54 (1), (2),(3),(4) na (5) vinaeleza mazingira, matumizi ya vimulimuli, ving'ora na wanaoruhusiwa kufunga ving'ora, vimulimuli na kuvitumia kutoa ishara za tahadhari na watumiaji wengine kupaswa kuwapisha au kuwapa kipaumbele.

"Wanaoruhusiwa kutumia ving'ora na vimulimuli kwa mujibu sheria hiyo ni magari ya dharura ambayo ni ya Polisi, Majeshi ya Ulinzi, Zimamoto na Uokoaji, Magari ya kubeba Wagonjwa au magari mengine na matela ambayo yamepata kibali kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali" alisema SACP Misime.

Magari mengine ni yale yanayotumiwa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Hivyo kama haupo katika makundi hayo ni kinyume cha sheria kufunga ving'ora, taa za rangirangi na vimulimuli na kuvitumia uwapo barabarani.

Kutokana na mazoea ambayo yameanza kujitokeza kwa baadhi ya watu wenye vyombo vya moto kufunga vifaa hivyo vya kutoa ishara na kuvitumia wawapo barabarani watambue waliopewa fursa hiyo ni magari ya misafara ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa Wakuu wa Vyombo vya Dola, magari ya dharura kama nilivyotaja hapo juu na yaliyopewa kibali na Waziri mwenye dhamana na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na si vinginevyo,

Taarifa ya Jeshi la Polisi kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, imesisitiza kuwa wataendelea kuchukua hatua dhidi yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Pia limetoa onyo kwa madereva wenye tabia hiyo waiache mara moja lasivyo watakamatwa.

***Imetolewa na:***
***Ofisi ya Uhusiano***
***Makao Makuu ya Polisi.***
***S.L.P. 9141,***
***DAR ES SALAAM.***



# TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Visawe, Vitawe na Vitate ni nini?

TOLEO lililopita, tulieleza kwa kirefu baadhi ya maneno yenye maana zinazokaribiana. Mara hii twawaleteeni maana ya 'vitawe' yaani maneno yenye maana zaidi ya moja. Sasa endelea ...

Umoja wa vitawe ni kitawe. Vitawe huchukua umbo au mofolojia -sarufi- yaani tawi la isimu linalohusika na uchambuzi na uchanganuzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa maneno katika lugha moja lakini katika muktadha wa kimatumizi huenda kitawe kikawa na maana tofauti.

Katika matumizi ya vitawe, mzungumzaji au mwandishi ni lazima awe makini ili kuondoa utata katika sentensi au usemi wake. Ifuatayo ni mifano ya maana ya vitawe:

Chungu: kifaa cha mfinyanzi cha kupikia; aina ya mdudu mweusi; kuwa na maumivu; patikana kwa wingi. Fuma: dunga kwa mkuki au mshale; suka sweta, fulana n.k. Goma: ngoma kubwa; susia, kataa au kaidi amri. Guni: chombo cha seremala cha kukwangulia ubao au cha kupimia pembe za miraba iliyo sawa; shairi la Kiswahili lililokosa kutosheleza kanuni moja au zaidi ya ushairi wa Kiswahili.

Harija: fedha zinazotumika katika shughuli za biashara au matumizi ya nyumbani; hoja nyingi za maneno zisizokwisha. Hema: tweta, pumua kwa nguvu; kibanda cha turubali. Jaa: furika hadi pomoni; jalala, mahali pa kutupa takataka. Kaa: kipande cha kuni kilichoungua; keti; aina ya mnyama wa majini. Kama: mfano, jinsi, mshabaha; shika chuchu za mnyama na kutoa maziwa. Kamba: uzi mnene; aina ya samaki wa baharini. Katika: vunjika, kwenye, ndani ya. Kigae: kifaa cha kuezeka paa la nyumba kilichotengenezwa kwa udongo au saruji; kipande kidogo cha chombo kilichovunjika; kigereng'enza (kipande cha chungu au mtungi uliovunjika). Kinga: zuia madhara fulani yasimfike mtu au mahali; jambo au dawa ya kujiepusha na madhara; kipande cha ukuni chenye moto au kilichoungua.

Kipepeo: kitu kinachopepea ili kuleta upepo au ubaridi; samaki mpana mwenye umbo la duara, rangi za mchanganyiko na mapezi ya nyuma mapana; mdudu mwenye umbo jembamba na mbawa pana zenye rangi mbalimbali na hupendelea kutua kwenye maua. Kuba: dari ya nyumba iliyojengwa mfano wa tao au bakuli lililofudikizwa; kaburi lililojengewa ukuta mfano wa chumba. Kuna: tumia mbuzi kusugua nazi; kuwako, kuwa huku na huku; sugua panapowasha.

Mbuzi: mnyama mdogo wa nyumbani anayefugwa kwa ajili ya nyama au maziwa; chombo cha kukunia nazi. Meza: kifaa cha mbao, chuma au plastiki cha kuandalia chakula au kuandikia; pitisha chakula kooni hadi tumboni.

Mwanamgambo: askari wa akiba aliyepata mafunzo ya kijeshi kwa ajili ya ulinzi wa taifa lake lakini asiye mwajiriwa wa jeshi, raia anayejitolea kufanya kazi ya ulinzi; mpiganaji wa kundi haramu hususan la waasi.

Mwari: msichana anayewekwa ndani kwa kutawishwa; mgonjwa aliyetengwa na kuwekwa ndani ili apate matibabu bila ya kuonekana na watu; bwana au bibi harusi wakati wa fungate (kipindi ambacho maharusi hukaa ndani na kuhudumiwa).

Nyanya: bibi, mama mzaa baba au mama; tunda la mnyanya ambalo hutumika kama kiungo cha mboga au kutengenezea kachumbari. Nyoka: tambazi mrefu mwembamba ambaye hana miguu, mwenye rangi mbalimbali anayetambaa kwa kunyiririka.

Paa: aina ya mnyama pori wa jamii ya mbuzi; kisusi cha nyumba; ruka kwenda angani; ambua magamba ya samaki; koka moto. Pea: aina ya tunda; kifaru; kaukiwa na sauti au potelewa na sauti; komaa, kuwa pevu. Paka: mnyana mdogo wa nyumbani anayekula panya; tia rangi, eneza rangi kwa kitu. Panda: kwea; manati; makutano ya njia au matawi ya mti ama vidole; tia mbegu au mche ardhini; atika. Rai: bembeleza; nguvu, siha, uzima; maoni, nasaha, ushauri; lisha chakula.

Shuka: kipande cha nguo, leso au kitambaa; teremka bei au gharama; teremka kutoka mahali palipo juu kama mti, ukuta, ngazi n.k. Sijida: alama inayotokeza kwenye paji la uso kutokana na kuguswa, kwa mfano kwenye mkeka au mswala wakati wa kuswali; tendo la kuinamisha uso na kuugusisha kwenye mkeka au mswala unaposwali.

Sita: nambari au tarakimu iliyo kati ya tano na saba; babaika, kuwa na wasiwasi, kutokuwa na hakika. Somo: mtu wa jina moja na mwingine; rafiki; kungwi, mwalimu wa unyagoni. Tai: aina ya ndege alaye mizoga; aina ya vazi au kipande cha kitambaa kivaliwacho kwenye ukosi wa shati au blauzi. Tema: kata; kutupa mate au chakula kutoka kinywani. Tembo: ndovu; pombe.

Uhuni: tabia ya kuzurura mitaani, kuwasumbua watu na kufanya vitendo vibaya; tabia ya kukaa bila mke au mume. Varanga: maneno ya kutia fujo; ingilia kwa ghafla mazungumzo aghalabu yasiyokuhusu. Vua: toa nguo kutoka mwilini; opoa samaki kutoka majini; okoa kutoka hatarini.

Wamba: tandaza na funga kitu kama vile ngozi kwenye ngoma au kamba kwenye kitanda; ishiwa na fedha, kuwa katika shida ya fedha za matumizi; enea kila mahali, zagaa. Yamini: mkono wa kulia; tendo au maneno ya kuapa. Ziada: kitu kilichoongezwa; kiasi kinachobaki baada ya matumizi. Ziara: tendo la kwenda mahali fulani kwa sababu maalumu, kwa mfano kutembelea au kufanya mazungumzo fulani; kaburi. Toleo lijalo tutawaleteeni maana ya neno 'Vitate.'

Nafasi ndogo iliyobaki tumalizie na jinsi waandishi wanavyochafua lugha ya Kiswahili: "Zahera ni fulu kicheko huko" ni kichwa cha habari kwenye gazeti la michezo. 'Fulu' si Kiswahili. Mwandishi angeandika: "Zahera ni kicheko tu" bila neno 'fulu'.

***Methali: Dira ya binadamu ni kichwa***

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

NA MICHAEL ENEZA

# 'Tunapress bolt aina zote' ni Kiswahili au hapana?

KUKUA kwa lugha ni pamoja na kuchukua maneno kutoka lugha nyingine au tamaduni tofauti na kuyaingiza katika lugha husika, hasa kwa matumizi ya kitaaluma na kibiashara ambako lugha hiyo haina mbadala wake unaoweza kutumika kwa njia rahisi.

Ulazima huo unakubalika hata kwa wahafidhina wa kukua kwa lugha ya Kiswahili ambao wanataka lugha hii ibaki katika uzio wa lugha za kikabila za Pwani na upeo wake uwe ni Kiarabu ambako Kiswahili kimekulia.

Wasiwasi wao ni kuanza kuelekeza hisia, fikra na uchukuaji wa maneno kutoka lugha za Wazungu na hasa Kiingereza, wakisema si Kiswahili.

Kwa mfano imekubalika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), fani ya utafiti wa Kiswahili, kuwa badala ya kutumia 'kuchukua maneno' ya lugha moja kwenda nyingine wanatumia dhana ya 'kuunda istilahi,' na wanakazania sana kuwa ni neno la Kiswahili wakati 'halisafishiki' kutoka mandhari yake ya Kiarabu.

Ili neno liwe sehemu ya lugha husika, viunganishi vyake vinahitaji kuleta maana katika lugha hiyo, na ndiyo inakuwa rahisi kuelewa mtu anazungumza nini.

Hakuna chembe ya Kiswahili katika 'istilahi,' ni neno lenye muundo wa Kiarabu moja kwa moja kwa maana kuwa vina vyake, mizizi yake, siyo ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine kuna eneo la ukuaji lugha linajumlishwa katika dhana ya 'Kiswahili Sanifu,' dhana ambayo pia inaleta mgogoro kihisia, kama usanifu huu maana yake ni usahihi au ni jitihada ya kuundaunda kitu kipendeze, mbele ya yule anayekiunda.

Kusanifisha ni kama kupamba, ni unadhifu wa kitu fulani pale ambapo unadhifu hasa ni muonekano wa mtu, na siyo kitu, na kwa maana hiyo kusema Kiswahili Sanifu ni kuashiria kuwa kina mwelekeo, mpangilio au hulka ya matumizi, mazoea ya aina fulani.

Ukiangalia unaona tunajitahidi kukwepa neno 'staili' ya matumizi, kuwa ni sehemu ya 'usanifu.'

Kuna maana ya kawaida ya matumizi ya dhana ya usanifu ambayo labda si njema kwa tafsiri pana ya hisia kitaaluma ya 'Kiswahili Sanifu,' kuwa mtu anaposema 'anamsanif' mtu mwingine (si kawaida kuisikia ile 'u' mwishoni) maana yake anamfanyia mzaha.

Sasa kama Kiswahili 'kinasanifiwa,' maana yake ni ile ya neno 'kusanif' katika Kiswahili cha kawaida, au linapata maana inayokubalika kwa dhana ya kutumia Kiswahili sahihi, linalotokana na jinsi 'sanif' inavyoeleweka, labda kwa Kiarabu?

Bila kujua wanachokifanya, ni wazi kuwa Kiswahili Sanifu mara nyingi ni mzaha katika lugha, unaoitwa usahihi.

Sehemu kubwa ya wateja wa Kiswahili Sanifu ni Idara za Serikali, hasa katika maandalizi ya maelezo bungeni kuhusu kinachofaywa na wizara tofauti wakati wa Bajeti.

Kwa mfano mtu anaelezea shughuli za Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi atajitahidi kutumia tafsiri zinazopitishwa au kubuniwa (na siyo 'kusanifiwa') na wataalamu wa Baraza la Kiswahili na taasisi kadhaa, kama TATAKI, Mlimani.

Kuna mengi ya kujifunza katika taarifa hizo hasa kuhusiana na majina ya viumbe ambayo kwa kawaida yanasikika kwa Kiingereza, hivyo labda kuna Kiswahili chake hakijulikani sana, au labda kimepatikana.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe (katikati), akizungumza wakati akifunga kongamano la kimataifa la Vyombo vya habari vya Kiswahili lililoandaliwa na Kigoda cha Mwalimu Nyerere Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

Yako maeneo mengine ambako watumiaji wenyewe wanabuni siyo maneno ila jinsi ya kuyatumia, kwa mfano 'spea' za magari (wataalamu walijaribu kueneza neno 'vipuri' zamani lakini si rahisi kusikia likitumiwa na mafundi mitaani).

Ndiyo hapo tunaingia katika maneno yaliyochokoza mada, unapopita maeneo ya Mwenge jijini ukafikia 'fremu' ya kutoa huduma za aina tofauti kwa wenye vyombo vya moto ambako tangazo hilo linaonekana.

Kwa mtu mwenye uelewa kuwa lugha inakuzwa na watumiaji wenyewe, kilichoandikwa hapo hakina tatizo lolote, ameongea Kiswahili kutaja huduma zilizopo, basi.

Angeongea Kiingereza iwapo anachokifanya pia kingewekwa katika lugha hiyo, iwe 'We press bolts of all types' (au We press all types of bolts) kwani cha msingi hapo ni jinsi taarifa au tangazo linavyomgusa mtu. 'Tuna-' ni kitu kinachofanyika mahali fulani, halafu 'press' ni huduma inayoeleweka kwa wenye vyombo vya moto ambako 'vyuma'vyake vinasuguana, hivyo kupoteza uwezo wa kustahimili msukumo wa mizunguko ya 'injini,' magurudumu, n.k.

Mtu akisema 'we press...' anaongea Kiingereza lakini akisema;'tunapress' anaongea Kiswahili, kwani 'press' imeingia hapo kama kifaa, ni matumizi ya kitaaluma kwani majina ya vifaa au viingizwaji katika eneo lolote la chombo cha moto vina majina yake.

> Kuna maana ya kawaida ya matumizi ya dhana ya usanifu ambayo labda si njema kwa tafsiri pana ya hisia kitaaluma ya 'Kiswahili Sanifu,' kuwa mtu anaposema 'anamsanif' mtu mwingine (si kawaida kuisikia ile 'u' mwishoni) maana yake anamfanyia mzaha.

Yako baadhi ya majina ambayo yameshaingia katika Kiswahili kwani yanatumika sana, hivyo kuanzia mwanzo yakapewa majina ya Kiswahili, au majina yakachukuliwa kwingine kutumika huko kwa mfano neno 'usukani.'

Unaweza kujiuliza kama neno hilo lilianzia katika chombo chochote kingine chenye usukani, kama majahazi yalikuwa na kifaa kama hicho, au alitokea mtu akafananisha kuendesha gari kwa kutumia kifaa hicho na kushona vikapu, 'ma-sweta' kwa kutumia kijifimbo chembamba 'kusukia.'

Pia kuna neno 'gurudumu' ambalo kupata kiini chake ni kubahatisha; hivi limetoka kwingine likaingia humu?

Ku-press katika Kiswahili halisi ni 'kubana' kitu fulani, lakini kuna chembe ya ziada ambayo haileti akilini na neno kubana, kwa mfano ku-press mvinyo, au katika uchapishaji wa vitabu na magazeti hiyo mitambo ni (printing) press, kiasi cha kutoa jina kwa taaluma ya uandishi habari.

Uhuru wa uchapishaji ukawa msingi, 'press freedom,' yaani uwezo wa kupeleka mitamboni, mashine ibonyeze karatasi, utoe chochote unachotaka.

Hivyo ziko 'press'za aina kadhaa, za haraka zikiwa ni hizo za mvinyo (kubana tunda la mzabibu litoe kinywaji cha sukari kinachoandaliwa kiwe divai, mvinyo).

Nyingine ni kuibana karatasi iguswe kwa nguvu na chuma chenye wino ili herufi zitoke; nyingine ni hii ya kuchonga chuma.

Sasa kwa mfano hakina msanifu asiyetaka Kiingereza, na labda badala ya 'kutohoa' neno kutoka lugha anayotaka yeye, atake watumiaji hao watumie Kiswahili cha 'kuchonga' chuma bado itakuwa tatizo.'

'Kuchonga' kwa Kiswahili ni kushika kisu au panga, na hata wembe katika mazingira tofauti, na kuweka ncha kali zaidi katika kitu fulani, ili matumizi yake yafae au yarahisishwe.

Huwezi kuondoa ncha halafu ukawa 'unachonga; chochote, hivyo ukipita 'fremu' nyingine utakuta 'wanachonga' funguo, kwani hapo kuna dhana ya ncha, hata kama ina tofauti na ncha za vifaa vingine.

Lakini 'bolt' hazina ncha bali mchongo wa kina stahili, kutumiwa kuzungushia kibanio cha chuma ili kifaa kitumike ipasavyo, n.k.

Ni wazi mafundi barabarani hawana muda wa kuhangaika kutafuta maneno tofauti ya hapa na pale yakiwemo hasa ya kuchonga, kuzungushia, vibanio vya chuma n.k. ili tu wakwepe neno 'bolt' wakati kila fundi na hata asiye fundi anajua 'bolt' ni nini.

Tatizo la usanifu lugha ni kujaribu kukwepa vianzio vya wazi vya kutumia maneno bila kuhangaika, kwa kuyaingiza tu katika kianzio cha Kiswahili, kwa mfano 'tuna...'ambayo ni taarifa kwa mpita njia asiyejua Kiingereza, hivyo 'We press...' ingemsumbua nini hasa, wakati 'tunapress' ni rahisi kuelewa, au wasanifu watasema 'swadakta.'

Ni hali halisi ya jinsi ya kuchanganya maneno ya kiufundi kama 'bolt' au 'ku-press,' kwa kukubali tu kuwa yatumike yalivyo.

## ELIMU

NA WILLIAM CHARLES

# Mfumo wa udhibiti mwendo wa mabasi na sarakasi zake

- Baadhi waupinga wakidai unalenga kukusanya mapato zaidi
- Wanaoukubali wasema unasaidia kufuatilia mienendo ya madereva wao
- Nchi jirani 'zatia timu' nchini kujifunza

UNAWEZA kusema ni patashika nguo kuchanika kwa jinsi suala la mfumo wa kudhibiti mwendokasi wa mabasi nchini kwa minajili ya kuhakikisha usalama wa abiria lilivyo na mvutano mkali baina ya wamiliki wa mabasi, madereva na taasisi za serikali.

Mnamo mwaka 2017 Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (LATRA), zamani SUMATRA ilianza kuufanyia majaribio mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia mwenendo wa kasi ya magari, hususani mabasi ya abiria ujulikanao kama Vehicle Tracking System (VTS).

Hiyo ni katika kukazia sheria ya usalama barabarani (1973) ili kulinda usalama wa wadau wote wanaotumia barabara.

Hata hivyo, baadhi ya madereva na wamiliki wa mabasi wanapinga namna unavyoendeshwa, wakidai mfumo huo ni mradi unaolenga zaidi kukusanya mapato, badala ya kudhibiti mwendokasi ili kuepusha vifo na majeruhi vinavyotokana na ajali za barabarani.

Hoja hii inakanushwa vikali na mamlaka za serikali.

Mfumo huu unaohusisha kampuni binafsi zilizopewa kazi na LATRA kufunga vifaa maalum kwenye mabasi ili kuweza kusoma kuanzia namba za basi husika, mahali lilipo, linapopita pamoja na mwendo wake, umefanyiwa majaribio tangu mwaka 2017, na sasa unatumika rasmi kwenye mabasi zaidi ya 3,323 yanayofanya safari zake mikoa mbalimbali nchini.



Ndiyo namna magari yasivyofuata sheria za usalama barabarani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Kamanda wa Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani nchini , Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Fortunatus Musilimu (mwenye kifimbo) akiwa katika operesheni ya kukagua mabasi ya abiria yanayosafiri mikoani .

**MKURUGENZI**

Mkulugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe anasema tangu kuanza kutumika kwa mfumo huu, madereva wengi wameachana na tabia ya mwendo hatarishi kwasababu wanajua wanatazamwa muda wote na VTS.

Hatahivyo anasema wapo wachache wasiotii sheria ambao wanaadhibiwa kwa kuzingatia sheria, kanuni za LATRA pamoja na sheria nyinginezo za usalama barabarani.

"Ni mfumo wa kisasa kwani tuna uwezo si tu wa kuona dereva alipo na mwendo anaoenda nao, bali kujua hata sehemu ambazo dereva alifunga breki za ghafla," anasema na kuongeza:

"Maofisa wa LATRA wanakuwa kazini muda wote wakipokea taarifa za mienendo ya mabasi yote... wanapoona yanayozidisha mwendo ulioelekezwa kisheria, wanatuma taarifa kwa polisi walio katika maeneo ya uelekeo wa basi au maofisa wa LATRA ili wachukue hatua kwa madereva husika."

**UWAMATA**

Katibu wa Umoja wa Madereva wa Mabasi (UWAMATA), Abdallah Lubala hakubaliani na ufanisi wa teknolojia hii.

Anasema kama LATRA ina lengo la kudhibiti mwendokasi wa mabasi, inatakiwa kutumia mfumo wa kianalogia kwa kufunga vidhibiti mwendo (Speed governor) na si vifuatilia mwendo (VTS).

"VTS haizuii dereva kuzidisha mwendo, inapiga kengele tu mwendo unapozidi kilometa 85 kwa saa, wakati kidhibiti mwendo kinaweza kuzuia gari lisiongeze mwendo zaidi ya ule uliokubalika kisheria," anasema na kuongeza:

"Mpaka sasa bado sheria zinatambua kidhibiti mwendo, hii VTS ni ya kibiashara zaidi...haiwezekani dereva apelekewe faini ya mwendokasi inayofikia milioni 11, akiuliza imekuwaje, anajibiwa kuwa alizidisha mwendo miezi minne iliyopita."

Lubala anasema madereva wanalazimishwa kulipa mamilioni ya fedha, huku akitoa mifano ya madereva wawili anaodai walipelekewa ankara ya milioni 3 na milioni 11, na baadhi ya faini wakitakiwa kulipa Sh. laki mbili kwa kila kosa kwa mujibu wa kanuni za LATRA na si Sheria ya Usalama Barabarani inayotaja faini ya elfu thelathini kwa kila kosa.

**MBUNGE 'MSUKUMA'**

Hoja zake zinaungwa mkono na Joseph Kasheku 'Msukuma', Mbunge wa Geita Vijijini na mfanyabaishara wa mabasi ya abiria mkoani Mwanza, Geita na Dar es Salaam.

Anabainisha kuwa tayari wafanyabaishara wameshatoa malalamiko kuhusu VTS na uendeshaji wake, kikiwemo kikao cha wamiliki wa mabasi na waziri mkuu kilichofanyika Juni 30, 2019 jijini Dodoma.

"Lengo la serikali ni kudhibiti mwendokasi na si kuwatumia madereva kama chanzo cha mapato... Wafanyabiashara tunasema tunahitaji kidhibiti mwendo na si kifuatilia mwendo...hili tulishamwambia hata waziri mkuu," anasisitiza.

Msukuma anabainisha kuna ulazima wa serikali kutengeneza mfumo wa kuwa na mtoza faini mmoja na si madereva kutozwa faini na maofisa wa LATRA, na siku zingine polisi huku faini hizo zikiwa na tofauti kubwa.

"Mfumo wenyewe wa VTS, 'seva' zake zinashikiliwa na kuendeshwa na watu walio mtaani (kampuni binafsi), kwahiyo ni rahisi kuchezewa na wamiliki mfumo," anasema na kuongeza:

"Kwanini LATRA wanashindwa kuuendesha wenyewe badala yake wanakuwa waangalizi tu?... Dereva wa Dar - Mwanza anaambiwa amezidisha mwendo mara 100, alipe faini milioni 3 wakati mshahara wake ni laki mbili kwa mwezi, haiwezekani."

**TRAFIKI**

Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Mratibu Msaidizi wa Polisi (ASP), Deus Sokoni anafafanua hatua ambazo polisi huchukua unapojitokeza utata katika udhibiti wa mwendokasi.

"Sheria mama ya usalama barabarani ni Sheria ya Usalama Barabarani, imeruhusu uwepo wa kipima mwendo (speed radar), ambapo polisi tunaita tochi, na LATRA kupitia kanuni zao ndiyo wanatumia VTS," anasema na kuongeza:

"Kisheria ushahidi wa mwendokasi unaorekodiwa na tochi ya polisi, ambayo askari anaishika na kulipiga picha gari linalokimbia huwa haubishaniwi hata mahakamani, ni ushahidi wa mwisho na unaojitosheleza."

ASP Sokoni anasema VTS ni mfumo mzuri kubaini tabia za dereva na kumwajibisha ila si mzuri sana kiusalama barabarani kwasababu inachukua muda kurekodi mwendo, kutafuta taarifa za basi na kisha kuzituma na hivyo dereva anaweza kuwa ameshatenda makosa mengi yanayohatarisha usalama wa abiria.

"Tochi ya polisi ikimnasa dereva aliye kwenye mwendokasi, anasimamishwa na kupigwa faini pamoja na onyo... VTS inahitaji muda mrefu na inapotokea utata baina ya mwendo uliorekodiwa na VTS au tochi ya trafiki basi inazingatiwa zaidi tochi," anasema na kuongeza:

"Hiyo ni kwasababu ipo kutokana na sheria mama na VTS ipo kutokana na kanuni za sheria nyingine... vivyo hivyo kwenye kutoza faini, faini ya polisi inazingatiwa zaidi."

Katikati ya mwezi Julai, 2019 zilisambaa tetesi kupitia mitandao ya kijamii kuwa mfumo wa VTS umesitishwa kutumiwa na LATRA.

Hata hivyo, Julai 20, mamlaka hiyo ilitoa ufafanuzi ikisema makosa ya mwendokasi yaliongezeka kwa zaidi ya asilimia 230, ndani ya kipindi cha wiki mbili tu baada ya kuenea kwa taarifa hizo.

Aidha, ilifanya kikao na wamiliki wa mabasi na kusisitiza kutositisha na kwamba inaendelea kuchukua hatua kali kwa madereva.

**TABOA**

Katibu wa wamiliki wa mabasi (TABOA), Ernea Mrutu anasema mfumo wa VTS hauna shida kwani unawasaidia hata wamiliki wa mabasi kufuatilia mienendo ya madereva wao na kuokoa mafuta yanayopotea zaidi kutokana na mwendokasi.

Hata hivyo, Mrutu anaomba pamoja na uwepo wa VTS, pia kiongezwe kidhibiti mwendo ili kumzuia dereva asizidishe mwendo.

"Hatupingi VTS, mfumo huu unaunganisha LATRA na mmiliki wa gari na wote wanakuwa na uwezo wa kuona mwenendo wa dereva mwanzo mpaka mwisho wa safari. Madereva waendeshe mwendo unaokubalika kisheria," anasema na kuongeza:

"Tumewaomba LATRA kwasababu wao ni wachache kuweza kukagua mwendo wa magari yote, basi watuunganishe TABOA tuwe na uwezo wa kuyafuatilia mabasi yote ili kuyabaini yanayouchezea mfumo na kuyaripoti...si kumuunganisha mmiliki mmojammoja tu na basi lake kama ilivyo sasa."

**UFAHAMU**

Ingawa king'amuzi cha VTS kinachofungwa katika mabasi hupiga kengele kwa nguvu kila dereva anapozidisha mwendo wa Kilometa 85 kwa saa, lakini abiria wengi hawafahamu kengele hiyo huashiria nini.

Hiyo inasababisha wasichukue hatua zozote za kumuonya dereva ili apunguze mwendo, jambo linalohatarisha usalama wao.

Abiria wanne kati ya watano ambao mwandishi aliwauliza iwapo wanafahamu namna ya kutambua kama dereva wa basi alilopanda amezidisha mwendo, walisema hutumia njia za asili za kuangalia kasi ya kupishana na miti au kuyapita magari mengine.

Ni mmoja tu ndiye aliyesema husubiri kusikia mlio wa king'amuzi cha VTS kujua kama dereva wa basi anazidisha mwendo.

Eveline Joseph, ambaye hufanya safari kati ya majiji ya Dar es Salaam na Mwanza mara kwa mara anasema:

"Nimewahi kusikia mlio katika baadhi ya safari zangu, hususani ambazo nilipata viti vya mbele... sikuelewa kama ni VTS, kwasababu inalia kidogo na kunyamaza... hivyo askari ambao huingia ndani ya mabasi kutuuliza juu ya uendeshaji wa dereva, pia hutuelimisha abiria kuhusu vifaa hivyo."

**RAMADHANI HAKEEM**

Ramadhani Hakeem ni abiria aliyekuwa akielekea Musoma kutokea Dar es Salaam wakati wa mahojiano na mwandishi wa makala haya. Anakiri kuifahamu VTS kupitia vyombo vya habari.

Anasema alimuona Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isaac Kamwele akitangaza uzinduzi wa mfumo wa VTS na namna unavyofanya kazi ndipo akaujua na kuanza kuufuatilia zaidi baada ya kusikia kuwa hata mtu binafsi anaweza kufunga kwenye gari lake.

"Baadaye nilijifunza zaidi kuhusu VTS kwa kusoma mtandaoni, na nikawa makini nikipanda basi nafuatilia kuona kama kengele ya VTS italia, ingawa mara kadhaa ambazo nilisikia ikilia sikuwahi kumwambia dereva apunguze mwendo kwasababu ya kuhofia abiria wenzangu kuniona msumbufu," anasema.

**TAKWIMU**

Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi nchini, jumla ya watu 61 wamefariki kati ya Januari mpaka Juni mwaka 2019, kutokana na ajali za mabasi, ukiwa ni wastani wa vifo vya watu 10 kila mwezi, huku asilimia kubwa ya ajali hizo zikisababishwa na mwendokasi.

Ripoti ya Usalama Barabarani ya Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), iliyotolewa mwaka 2018 inasema asilimia 30 za ajali barabarani katika nchi zilizoendelea hutokana na mwendokasi huku nusu ya ajali katika nchi za dunia ya tatu, Tanzania ikiwemo husababishwa na mwendokasi.

Tafiti za WHO zinabainisha zaidi kuwa kadri dereva anavyoongeza mwendo, ndivyo uwezekano wa ajali kutokea huongezeka.

"Gari linalokimbia kilometa 50 kwa saa litahitaji kusogea mita 13 zaidi mbele ili liweze kusimama na gari linalokimbia kilometa 40 kwa

Inaendelea Uk. 18

## JIELIMISHE

### MIKATABA YA GENEVA YATIMIZA MIAKA 70




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la Human Rights Watch, Kenneth Roth.
**PICHA: MTANDAO**

NI miaka 70 sasa tangu kusainiwa kwa mikataba minne ya Geneva, iliyoweka msingi wa sheria ya kimataifa ya kulinda haki za binadamu.

Hata hivyo, ingawa nchi 196 zimetia saini mikataba hiyo, utekelezwaji wake bado unasuasua.

Mikataba hiyo minne ya baada ya vita vikuu vya pili vya dunia iliweka kanuni za kulinda haki za raia na wanajeshi katika mazingira ya vita.

Ingawa nchi 196 ni wanachama wa mikataba hiyo, utekelezwaji wake wakati huu unakabiliwa na tishio katika maeneo kadhaa ya mizozo.

Kwa mujibu wa mikataba hiyo na itifaki kadhaa za nyongeza, raia na wanajeshi wanayo haki ya kutendewa kibinadamu katika mizozo ya kivita, na mashambulizi yoyote ya kijeshi yanaruhusiwa tu dhidi ya shabaha za kijeshi.

Lakini, wakati mizozo ya kisasa ikijikita zaidi katika mazingira ya mjini, pande zinazohasimiana zimekuwa mara kwa mara zikiikiuka mikataba ya Geneva.

Mashambulizi yaliyoibuka upya dhidi ya raia nchini Syria, mamia ya raia wanaouawa nchini Afghanistan, Shirika la kimataifa la Msalaba mwekundu linasema mikataba ya Geneva haionekani kuzuia unyama wa kivita kama inavyopaswa.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la Human Rights Watch, Kenneth Roth anasema ukiukaji wa mikataba hiyo umeenea kutoka Myanmar, Yemen hadi Syria. **DW**

# Mfumo wa udhibiti mwendo

Inatoka Uk. 17

saa litasogea kwa mita 8.5 mbele ndipo liweze kusimama...kila inapoongezeka kilometa moja kwa saa na uwezekano wa kutokea kwa ajali uonaongezeka kwa asilimia tatu," inasema sehemu ya ripoti hiyo.

Katika mazingira haya, udhibiti wa mwendokasi ni suala muhimu kwa usalama wa abiria, ingawa jitihada za udhibiti wa mwendokasi wa mabasi nchini zinaonekana kuibua mvutano.

**MWANASHERIA**

Mwanasheria wa madereva wa mabasi nchini Frank Kisanga anasema madereva wamemuelekeza kufungua kesi kuhoji uhalali wa matumizi ya VTS katika mabasi pamoja na kutozwa faini kwa kutumia kanuni za LATRA, badala ya sheria ya usalama barabarani.

Ngewe anajibu madai hayo, akisema:

"Kama madereva hawataki kutozwa faini na mamlaka yetu waache udereva wa mabasi, wakaendesha magari binafsi ambayo hatuyapi leseni ya kufanya kazi," anasema na kuongeza:

"Haiwezekani mamlaka ya usimamizi iwe haina mamlaka ya kuadhibu iliyowapa leseni za kufanya kazi husika... udhibiti mwendokasi unafanyika kuokoa maisha ya abiria na hata hao madereva walalamikaji."

Ngewe anasema kuanzia mwaka 1996 walipokuwa wakifunga kidhibiti mwendo kinachozuia gari isiweze kuzidisha mwendo kwa kuzuia mafuta yasitumike, madereva walikuwa waking'oa au kuvichezea vifaa bila wao kujua.

"Mfumo wa sasa wa VTS unaweza kuona kama basi limezuia kifaa kilichofungwa kisifanye kazi... tunaona kwenye kompyuta zetu na kuchukua hatua... hatuwezi kurudi nyuma, mambo yanabadilika na teknolojia inakua," anasema.

**JIRANI WAJIFUNZA**

Aidha, imebainishwa kwamba mataifa jirani yameshaanza kutuma maofisa wake wa masuala ya usalama barabarani nchini, kujifunza mfumo wa VTS, ili wakaanzishe katika mataifa yao.

## JE, WAJUA?



Vitalu vya miti ambayo inasaidia kukabiliana na mabadilliko ya tabianchi. **PICHA: MTANDAO**

# Ethiopia yapanda miti milioni 350 kwa saa 12

ETHIOPIA imevunja rekodi ya upandaji miti kwa siku moja ambapo katika uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti, imepanda zaidi ya miti milioni 350 kwenye bustani ya Gulele jijini Addis Ababa.

Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, (UN Environment) linasema kampeni hiyo ya kipekee, inalenga kukabiliana na uharibifu wa misitu na mabadiliko ya tabianchi.

Ikiwa ni sehemu ya mpango ulioanzishwa na Waziri Mkuu wa nchi hiyo Abiy Ahmed wa kupanda miti, kampeni hiyo inataka kuona kila siku miti milioni 200 inapandwa katika maeneo 1000 nchini kote.

Akizungumza kwenye tukio hilo, Ahmed anapongeza taifa lake kwa si tu kukidhi mpango huo lakini pia kuvuka lengo.

Miti hiyo milioni 350 ilipandwa ndani ya saa 12 na kuvunja rekodi ambayo iliwekwa na India mwaka 2016 ya kupanda miti mingi zaidi kwa siku moja, ambayo wakati huo ilikuwa miti milioni 50.

Wawakilishi kutoka Umoja wa Mataifa (UN) walishuhudia tukio hilo la aina yake ambapo Mkurugenzi wa UN Environment ofisi ya Afrika, Juliette Biao anasema:

"Afrika ina sifa na uwezo wa kuendeleza kampeni ya upandaji miti duniani, na kwa kuzingatia kuwa imeathirika zaidi na iko hatarini zaidi, hatua za kukabili mabadiliko ya tabianchi lazima zipewe kipaumbele katika siku za usoni."

Anaongeza kuwa, "Sisi katika UN Environment, tunaongoza kusaidia kujenga uwezo wa mataifa na watu wake kutekeleza wao wenyewe mikakati ya upandaji miti na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi."

UN inakadiria kuwa wigo wa misitu wa Ethiopia umepungua na kufikia asilimia 4 kwenye miaka ya 2000, kutoka asilimia 35 mwanzoni mwa karne iliyopita ya 20.

Kwa rekodi hiyo mpya ya Ethiopia, shirika hilo la mazingira la UN limetaka mataifa mengine ya Afrika yachukue hatua mapema ili kuipatia ufumbuzi changamoto hii badala ya suala la kukubali mambo kama yalivyo.

Wataalamu wanasema kuwa miti inasaidia bayonuai na mazingira kwa sababu kadri inavyokua, inafyonza hewa ya ukaa ambayo ni hatari sana kwa ongezeko la joto duniani.

Kwa mujibu wa chapisho moja katika jarida la kisayansi, watafiti wanakadiria kuwa upandaji miti kote duniani unaweza kuondoa theluthi mbili ya hewa chafuzi inayoingia angani kutokana na shughuli za binadamu. HABARI UN

# UTAFITI

## WATU WAAMINIFU HASWA KULIKO TUNAVYOFIKIRIA!

MIAKA kadhaa iliyopita, mtafiti mmoja "aligawa" vipochi 400 katika maeneo tofauti ya umma kama vile Benki, Kumbi za Sinema, hotelini, mahakamani na kwenye vituo vya polisi katika miji minane ya India.

Watu waliotumwa na mtafiti huyo, waliviwasilisha kwa walinzi wa maeneo hayo au wahudumu wanaokaribisha wageni, wakidai wameviokota njiani.

Baadhi ya vipochi havikuwa na hela na vingine vilikuwa na dola zaidi ya tatu, pesa taslimu.

Kila kipochi kilikuwa na kadi tatu zinazofanana za biashara, zilizo na jina la mwenyewe na anwani yake ya barua pepe, orodha ya vitu alivyotaka kununua na ufunguo.

Siku chache baadaye kundi la watafiti waliojidai kuwa wenye vipochi hivyo walisubiri kupigiwa simu na hao walinzi, kama sehemu ya utafiti wa kubaini kiwango cha uaminifu wao.

Vipochi hivyo vilikabidhiwa kwa wanaume 314 na wanawake 86 katika miji ya Ahmadabad, Bangalore, Coimbatore, Hyderabad, Jaipur, Kolkata, Mumbai na Delhi.

Asilimia 43 ya vipochi vilivyokuwa na pesa viliwasilishwa kwa wenyewe, lakini vile ambavyo havikuwa na hela ni kidogo sana vilivyoripotiwa kupatikana, kwamba ni asilimia 22 tu ndivyo vilivyowasilishwa kwa wenyewe.

Matokeo ya utafiti huu wa kushangaza uliochapishwa hivi karibuni katika Jarida la kisayansi, unathibitisha kuwa watu ni waaminifu kuliko vile "tunavyofikiria."

Alain Cohn, mtaalamu wa saikolojia ya tabia katika Chuo Kikuu cha Michigan nchini Marekani na ambaye pia ni mmoja wa watafiti hao anasema "Hatukutarajia tulichokiona."

"Watu wanapojua kuwa huenda wakafaidika kutokana na tabia ya kutokuwa na uaminifu, hamu ya kuficha ukweli inaongezeka... lakini usumbufu wa kiakili unaoandamana na hisia ya kujiona mwizi huwafanya kubadili mawazo, hasa ikiwa hawajazoea kuiba kitu cha mtu," watafiti wanasema.

Mji wa Kusini mwa India, ulikuwa na kiwango cha chini cha watu walioripoti kuokota vipochi vilivyokuwa na pesa, Bangalore (66%) na Hyderabad (28%).

Mji wa Coimbatore, uliandikisha idadi kubwa ya watu walioripoti kuokota vipochi ambavyo havikuwa na hela (58%), huku mji mkuu wa Delhi, ukiwa na kiwango cha chini cha wale waliorudisha vipochi ambavyo havikuwa na hela (12%).

Watafiti waligundua kuwa wanawake walifurahia sana kuwasilisha vipochi walivyookota, viwe na pesa au la wakilinganishwa na wanaume.

Utafiti wa "kuangusha" kipochi ama vipochi nchini India, ilikuwa sehemu ya utafiti mkubwa wa Kimataifa uliofanywa na watafiti ili kubaini tofauti kati ya uaminifu na maslahi binafsi.

Kati ya mwaka 2013 na 2016, watafiti "waliangusha" jumla ya vipochi 17,000 katika miji 355 ya nchi 40.

Baadhi ya vipochi hivyo vilikuwa na pesa, dola 13.45 za Marekani ambazo zimebadilishwa katika sarafu za nchi husika na kuongezwa kiwango chake kulingana na kiwango cha maisha cha watu wa nchi hiyo.

Miji mitano mikubwa kati ya minane ilishirikishwa katika utafiti huo. Watafiti walikadiria kuwa watu katika mataifa 38 kati ya 40 waturudisha vipochi vilivyo na hela. (mataifa mawili ambao waleti hazikurudishwa ni Peru na Mexico.)

Lakini kiwango cha pesa kilipoongezwa mara saba zaidi katika waleti hizo na kuangushwa tena katika mataifa matatu, kiwango cha waleti zilizorudishwa kilipanda kwa 18%.

Waleti zilizokuwa na pesa nyingi zilirudishwa kwa kiwango kikubwa Denmark (82%) na kiwango cha chini kutorudishwa ilikuwa (13%).

# wa mabasi na sarakasi zake

Maofisa wawili wa Mamlaka ya Usimamizi wa Usalama Barabarani nchini Rwanda (ARUA), walifika nchini na kutumia siku mbili kujifunza mfumo huo miezi sita iliyopita.

Aidha, maofisa watano wa NTSA ya Kenya walifika Julai mwaka huu kujifunza mfumo huo kwa wiki moja.

Mkurugenzi Mkuu wa NTSA ya Kenya Francis Meja alipoulizwa na mwandishi kuhusu alivyouona mfumo wa VTS ameupa 'heko', na kusema wamebaini mabasi yanayosafiri kati ya Tanzania na Kenya yalikuwa hayazidishi kilometa 85 kwa saa yanapokuwa Tanzania.

"Lakini yakivuka mpaka wa Namanga na kuingia Kenya, yanakimbia mpaka kilometa 140 kwa saa kwani VTS haiwezi kutumika kuadhibu makosa yanayotendeka nje ya Tanzania," anasema na kuongeza:

"Tumependa mfumo, tumejifunza na sasa tupo nyumbani Kenya tukianza kuandaa mazingira tuanze kuutumia na kuachana na kidhibiti mwendo...sisi hatutafunga VTS kwenye mabasi tu, tutafunga hata kwenye malori, na magari mengine ya kibiashara kama teksi."

**KITUONI**

Mwandishi alipotembelea kituo maalum kinachopokea taarifa za VTS zinazohusu mabasi yote 3,323 yaliyofungwa vifaa hivyo, aliona uwepo wa maofisa wasiozidi 10 wa LATRA wanaohusika katika ufuatiliaji wa mienendo ya mabasi na kuripoti maeneo mabasi yanayokoelekea.

Katika mazingira haya si rahisi mabasi yanayozidisha mwendo kinyume cha sheria ya barabarani kubainika na kuripotiwa papohapo kwani inabidi maofisa hao watafute taarifa za basi mojamoja.

Kwamba inapobainika lililozidisha mwendokasi, taarifa zinatumwa linapoelekea ili hatua zichukuliwe.

Ufinyu wa rasilimali watu wa kufuatilia mabasi haya ndiyo unasababisha malimbikizo ya makosa na faini mpaka kufikia mamilioni kwa dereva mmoja.

---

**Na Benjamin Smith**

## UCHAMBUZI WA KITABU;

# MINDSET (FIKRA)

KARIBU msomaji kujifunza kutoka vitabuni. Fikra chanya ni mwanzo wa mafanikio na ndio hufanya maisha yawe bora dhidi ya changamoto na magumu yoyote yale ambayo mtu aweza kupitia.

Mwandishi wa kitabu hiki Benjamin Smith anatualika sote kujua umuhimu wa kuwa na fikra chanya wakati wote.

Mwaliko huu wa kujijengea fikra chanya ndio unasaidia kuyafanya maisha yawe na furaha, utajiri na huimarisha afya ya mwili.

Fikra hasi, au hisia hasi huharibu maisha ya mtu na ndicho mwandishi Benjamin Smith anatuonyesha namna tunavyopaswa kudhibiti na kuepuka vyanzo vya hisia au fikra hasi zenye uharibifu.

Umuhimu wa kuwa na fikra chanya hufungua uwezekano wa fursa, utajiri na mafanikio. Fikra zinapokuwa chanya huvuta mambo chanya ndani ya mtu na nje ya mtu.

Ndani huvuta uimara, furaha, imani, ujasiri na nje huvuta utajiri wa watu na mali. Hakuna mtu asiyependa kuwa karibu na mtu wa fikra chanya.

Fikra chanya hulinganishwa na nishati au nguvu inayosambaa na kufanya wengine nao wawe na fikra chanya. Umuhimu huu wa fikra chanya ni kuyapa maana maisha na kujenga mtizamo chanya wa maisha iwe katika wakati bora au wenye changamoto.

Ili kuwa na fikra chanya mwandishi anaturudisha tujifunze juu ya utendaji kazi wa akili isotambuzi ambayo ndio huongoza na kufanya vitu pasipo utambuzi wetu.

Wakati ambao umekuwa umelala, basi hii akili hufanya kazi kubwa kama kukusaidia uote ndoto, mapigo ya moyo kuendelea kufanya kazi na kazi zote ambazo hufanywa pasipo akili tambuzi. Hii akili imekuwa na nguvu na maajabu makubwa namna walojua kuitumia imesaidia kuwaletea ubunifu na kuweza kudhibiti mawazo na hisia ndani ya mtu.


Akili hii huhitaji mazoezi ambayo unaweza kufanya na ikashika nguvu ya kukusaidia kupiga hatua. Tabia nyingi zinazokuja kuwa na nguvu na kumwongoza mtu huwa zimeota mizizi ndani ya akili hii isotambuzi.

Hii inatuonyesha namna kuacha uraibu wa vitu kama sigara, pombe, kujichua na michezo ya bahati nasibu huwa kazi, tofauti na watu walivyoanza.

Hii akili huchukua nguvu pale unaporudiarudia kitu kwa muda mrefu kufanya, kuongea au kufikiria. Hivyo ili kuvunja tabia mbaya au kujenga tabia bora lazima ziwe ni za kurudiarudia kwa muda mrefu.

Ili kujenga fikra chanya na kuepuka fikra hasi au mawazo hasi ni muhimu kufanya mazoezi ya kurudiarudia kujitamkia kauli chanya wakati wote.

Jikubali na kujiona una thamani kubwa kila siku. Kitendo cha kurudiarudia kujitamkia vizuri, kujiwazia vizuri, ndivyo unavyotuma taarifa katika akili isotambuzi itakayoweza kukusaidia baadaye ujione mtu mwenye mtizamo chanya, mwenye nguvu, mwenye uthubutu na kuona unaweza kufanya mambo makubwa kama wengine wawezavyo kufanya.




Hivyo shika kuanzia leo kuwa akili isotambuzi hushika nguvu kwa kurudia rudia jambo au kitu kila siku.

Haimaanishi ukianza kuwa na fikra chanya hutakutana na matukio mabaya, changamoto au magumu. Haya mambo yatakuja kila siku.

Mwandishi anatushirikisha jambo muhimu lingine la kujifunza la kuona uzuri katika ubaya. Hata kama jambo limetokea lenye ubaya basi kwa mtu mwenye fikra chanya ana kitu cha kujifunza kutokana na jambo hilo.

Mfano tukio la kukosea kitu kufanya kwa ubora limemtokea mtu. Mwitikio wa tukio hili aliye na fikra chanya hukumbushwa kuwa kukosea kwake ni fursa ya kujifunza, kujiandaa vizuri na pengine kujiboresha zaidi ya awali. Hivi ndivyo uzuri hupatikana katika ubaya.

Njia nyingine kama kuandika vitu ulivyojifunza kwa siku ni njia bora ya kukagua kwa kiasi gani fikra hasi zinavyoweza kudhibitiwa.

Unapoandika siku yako ulojifunza, unayohitaji kujiboresha inasaidia kuziepuka hisia hasi na kujenga maisha katika mtizamo au fikra chanya.

Kadri unavyoweza kujitengenezea huu utamaduni wa kuandika unayojifunza kila siku inayopita unaendelea kujenga uimara dhidi ya fikra hasi.

Fikra hasi ni nguvu ambazo unaposhindwa kudhibiti zinaweza kukuongoza zitakavyo na kuharibu hatua zako kwenda juu.

Dhibiti mawazo hasi yanayokuja kichwani kwako ukijua mawazo hubeba umbo. Dhibiti na hisia hasi kama hasira, chuki, wivu ukijua ni uharibifu unaoweza kukupotezea mwelekeo maishani.

Utakuwa umeona jinsi watu walio na fikra hasi ni watu hatari kukaa nao. Maneno yao tu hutosha kumaliza nguvu zako na hamasa ya kupiga hatua katika siku yako.

Hivyo jiepushe na makundi ambayo hunyonya nguvu zako na tafuta watu wenye fikra chanya ili upate hamasa ya kupiga hatua. Unaweza kushinda hili kwa kuwa na machaguzi mazuri ya watu unaowaruhusu waingie katika maisha yako.

Socrates alipata kusema juu ya kujijua wewe mwenyewe kama njia ya mafanikio katika maisha ya mtu.

Unapojijua wewe mwenyewe unajua namna wewe ni msimamizi mkuu wa mawazo, hisia na taarifa unazoziingiza katika akili yako.

Kila ambacho unakikosea usimamizi hasa maeneo haya mawazo, hisia, taarifa na picha unazojenga fikrani unaruhusu maisha yafanye yanavyotaka na kukupa chochote kile.

Ukiwa na maswali, maoni na ushauri basi usisite kuwasiliana kwa njia yoyote ile hapo chini. Kuwa na fikra chanya uvute maisha bora na yenye mafanikio kwako na wanaokuzunguka.

*Mchambuzi ni*
***Dk. Raymond Nusura Mgeni***
***raymondpoet@yahoo.com***
***+255 676 559 211.***
***Dar-es-Salaam***



# WADAU SABATO KASIKA

**ZAMANI shule za msingi na sekondari zilitoa vipaji vya wanamichezo mbalimbali walioleta sifa kwa nchi kitaifa na kimataifa tofauti na sasa. Tatizo liko wapi na nini kifanyike kurejesha hadhi hiyo? Wadau wanajadili.**



**SULEIMAN MATHEW (MCHEZAJI WA ZAMANI WA MPIRA WA MIGUU)**

KWANZA kaulimbiu ya 'michezo ni afya' ilichukuliwa kwa umuhimu mkubwa na wazazi wetu wakati ule wa utoto wetu na pia somo la michezo lilileta hamasa kwa wanafunzi kushiriki michezo shuleni. Ikumbukwe kuwa kulikuwa na mechi za upinzani shuleni za madarasa ambapo utakuta darasa la kwanza wanacheza mechi na darasa la pili, hali kadhalika darasa la tatu wanacheza na la nne na kuendelea. Kwamba kidato cha kwanza walicheza na kidato cha pili kama ilivyokuwa kwa vidato vya juu. Pia mashindano ya shule kwa shule na serikali ikichangia kutoa ruzuku shuleni ili michezo ichezwe. Aidha, walimu walikuwa wapo 'bize' kuhakikisha timu zao zinapata ushindi, hivyo ilikuwa rahisi kwa kila mwanafunzi kushiriki michezo shuleni ambapo michezo ya riadha, netiboli pia ilipewa kipaumbele kikubwa. Ndio maana walimu waligundua vipaji vingi na kuvitunza, tofauti na miaka hii ya karibuni ambapo michezo shuleni imekosa fursa na wazazi kutoa kipaumbele kwa watoto wao kushiriki masomo ya jioni ya ziada kuliko kushiriki kwenye michezo. Kwa hiyo ni muhimu kurudisha somo la michezo shuleni liwe ni sehemu ya mitaala na kuongeza walimu wenye taaluma ya michezo. Hatua hiyo inaweza kuleta jibu la swali lako kwamba nini kifanyike baada ya kukosekana kwa vipaji kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambavyo vilisaidia kuitangaza Tanzania katika mataifa mbalimbali.



**ELIZABETH TUNGARAZA (MWALIMU NA MTAALAMU NA MICHEZO)**

WANAFUNZI wa sasa walio wengi wanakula chakula cha aina moja, yaani chips kuku au chips mayai na pia muda wa kwenda shule, walio wengi wanapanda magari, siyo kama zamani wanafunzi walitembea kwa muda mrefu na hilo lilikuwa ni zoezi zuri la kuweka mwili vizuri au wanakimbia kwa ajili ya kuwahi namba shuleni wakiogopa adhabu. Vilevile msingi wa michezo umeachwa, hasa shule za msingi, watoto wengi hawashiriki na hakuna ufuatiliaji madhubuti, ndio maana vipaji havionekani kwa wanafunzi wa UMISETA na UMITASHUMTA. Hii inatokana na timu zinapokuwa kwenye kambi za mkoa na wilaya zinakaa muda mchache tofauti na zamani. Watoto hawapati nafasi wote kutokana na michezo kutofuatiliwa vyema tangu ngazi ya shule. Kama tumedhamiria kufufua vipaji kwa ajili ya manufaa ya taifa, basi tuangalie tulikojikwaa na kupasawazisha ili hatimaye tuweze kufikia kile tulichokikusudia, kwasababu vipaji vipo, kinachotakiwa ni kubuni mbinu za kuviendeleza. Wazazi washirikishwe kikamilifu ili wasaidie kuwaandaa watoto wao kwa kuwanunulia vifaa vya michezo kama viatu, kwani sidhani kwamba kwa majukumu mengi ambayo serikali inayo inaweza kufanya kila kitu. Ikumbukwe kuwa pesa zinazotolewa na serikali haziwezi kutosha hadi kununulia vifaa vya michezo, ndio maana nikashauri kushirikisha wazazi.



**DOMISIAN KASHAMBA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

TATIZO ni kwamba walimu wa sasa wanaandaa watoto wakati wa kipindi cha Umitashumta na Umiseta. Kipindi chote kuanzia Julai hadi Desemba hakuna michezo yoyote inayosimamiwa na mwalimu. Baadhi ya walimu wakuu hawapendi kushirikisha watoto kutokana na kuchangia nauli ngazi ya shule. Hivyo serikali ipeleke pesa moja kwa moja kwa wahusika kila ngazi kulingana na asilimia zilizotengwa badala ya kuwapa jukumu hilo walimu wakuu na wakuu wa shule. Pia serikali isaidie watu binafsi waliowekeza kwenye michezo kwa kutoa ruzuku ya uendeshaji wa kitengo cha michezo kwa shule binafsi mfano Filbert Bayi na nyingine na kusimamia matamko ya kuanzisha vituo na shule za michezo kila wilaya yawe katika matendo halisi. Cha msingi sasa ni kurudi tulikotoka, kwani kipindi hicho cha michezo tulikuwa ni wazalendo kwa kuimba nyimbo mbalimbali, lakini leo hilo halipo, tena ndio maana katika ngazi ya mkoa kwenye kuunda timu, mikoa mingi inalipua kutokana na ukosefu wa fedha na wanakaa kambini kwa muda mchache. Wanaona bora liende ili mradi wawafikishe kwenye mashindano ya kitaifa ili kutekeleza agizo. Pia baadhi ya maofisa michezo wa mikoa na wilaya hawana historia ya michezo kwenye maisha yao, hivyo hawawezi kubuni mikakati itakayosaidia timu zetu kupata msaada kwa wadau mbalimbali ili timu zikae kambini kwa muda mrefu kuliko kusubiria pesa kutoka serikalini. Watu wa aina hiyo waondolewe ili kuibua vipaji.



**NANCY MRIKARIA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KILA anayejua historia ya nchi kwenye michezo mbalimbali, atakuwa anakumbuka jinsi ambavyo baadhi ya watu waliitangaza Tanzania kimataifa kwa kutumia vipaji vyao vikiwamo vya kukimbia mbio za kilometa mbalimbali, lakini hilo leo ni kama halipo tena, kwani katika kizazi hiki hajatokea Mtanzania ambaye ameweza kuvunja rekodi za wale waliosifika miaka ya nyuma wakiwamo akina Filbert Bayi, Juma Ikangaa, Suleiman Nyambui na Mwinga Mwanjala. Sababu kubwa iliyotufikisha hapa tulipo ni vipindi vya michezo viliondolewa shuleni ikiwa ni pamoja na halaiki kwa wanafunzi, hivyo ni vigumu sana kutambua vipaji vya michezo kwa watoto wetu. Lakini bahati nzuri ni kwamba michezo imerudishwa shuleni na itakuwa ni rahisi kuibua vipaji hivyo. Kiongozi wetu mkuu, Rais John Magufuli amerudisha michezo hiyo shuleni na anasimamia vizuri na wasaidizi wake. Kwa hiyo ili iwe endelevu, asitokee tena kiongozi mwingine akapiga marufuku michezo shuleni, kwani inawajenga vijana, wanakuwa shupavu, pia inawajenga kimwili na kiakili. Itafika wakati tutawapata wanamichezo wengine kama waliopata majina makubwa mfano wa niliowataja hapo juu, yaani akina Filbert Bayi, Juma Ikangaa, Suleiman Nyambui na Mwinga Mwanjala.



**GRATIAN MKOBA (RAIS MSTAAFU WA CHAMA CHA WALIMU TANZANIA)**

KWANZA kabisa, kwa sasa michezo ni ajira, furaha na inajenga umoja na mshikamano katika jamii, kwani huwakusanya watu pamoja na bila kujua, wengi kati yao huonyesha hisia zao aidha kwa furaha au huzuni. Ndio maana wadau mbalimbali wa michezo nchini wamewahi kuishauri serikali kuangalia upya sera ya michezo nchini, hasa kwa shule za msingi kwa kuwa ndiko vipaji huanza kuonekana vyema na kuvidumisha. Walitoa ushauri huo kutokana na ukweli kwamba michezo shuleni kwa sasa haipewi kipaumbele kwa shule nyingi kiasi cha kuonekena kuwa si jambo la muhimu kwa maendeleo ya vijana kama ilivyo kwa masuala mengine. Shule nyingi hazina 'sports facilities'. Walimu wamekwishapoteza morali kitambo, kwasababu ya maslahi duni. Kwa hiyo kama tunataka kuibua vipaji kama zamani, basi waboreshewe maslahi yao ndipo tutaanza safari hii upya ya kuibua vipaji. Sera ya elimu nchini inasisitiza kujitegemea, ambapo haimaanishi kwa wanafunzi kufanya shughuli za kilimo pekee bali pia wafundishwe stadi mbalimbali za michezo ili watakapomaliza waweze kujitegemea. Lakini hilo haliwezi kufanikiwa iwapo walimu ambao ndio wanatakiwa kuwafundisha watakuwa hawajatimiziwa mahitaji yao vizuri. Hata wakihudhuria mafunzo ya kubuni na kuthubutu katika uendeshaji wa shughuli za michezo, hawawezi kufika mbali kama wataendelea kulalamikia maslahi duni.



# Moto wateketeza hekta 12 za ngano

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole, imepata hasaza ya zaidi ya Sh. milioni 36 baada ya hekta 12 za mashamba ya ngano yanayomilikiwa na kituo hicho kuteketea kwa moto.

Moto huo ulitokea juzi mchana na kudumu kwa dakika 45 na kuteketeza mashamba hayo na hatimaye kuzimwa na wananchi, wafanyakazi wa kituo hicho kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Ukoaji.

Kaimu Makamu Mkuu wa TARI- Uyole, Emmanuel Mwalukasa, alisema eneo hilo la kilimo lina hekta 22 ya ngano na kwamba kati ya hizo hekta 12 ndizo zilizoteketea kwa moto.

**Mashamba yanayolimwa katika kituo hicho ni zaidi ya 150 na kwamba jitihada za kuzima kwa haraka moto huo zimesaidia kupunguza athari.**

Alisema mashamba yanayolimwa katika kituo hicho ni zaidi ya 150 na kwamba jitihada za kuzima kwa haraka moto huo zimesaidia kupunguza athari.

"Taarifa za mashamba hayo kuungua moto nilizipata nikiwa kanisani majira ya saa sita mchana. Nililazimika kutoka na kuliarifu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao walifika na kuanza kuuzima," alisema Mwalukasa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema chanzo cha moto huo kinadhaniwa kusababishwa kipande cha mkaa chenye oto ambacho kilikutwa ndani ya mashamba hayo.

Alisema kutokana na upepo mkali, kipande hicho kilisababisha moto kusambaa na kuunguza mashamba hayo.

Kutokana na athari hiyo, Kamanda Matei alisema atashauriana na uongozi wa kituo hicho kutengeneza uzio kuzunguka mashamba ili kuthibiti shughuli za kibinadamu karibu na mashamba hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema jitihada za kuzima moto zimesaidia kupunguza madhara ambayo yangeteketeza hekta zote za mashamba ya ngano.

Alisema mpaka sasa chanzo kamili cha moto huo hakijajulikana na uchunguzi unaendelea huku akitoa onyo kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii kuacha upotoshaji wa taarifa hizo ambazo haziendani na uhalisia.

## Wapata manufaa mradi wa chumvi

Na Grace Mwakalinga, MOMBA

WANANCHI wa Kata ya Ivuna, Tarafa ya Kamsamba, Momba, mkoani Songwe, wameanza kuvuna chumvi kupitia mradi wao wa Itumbula ulioanzishwa mwaka jana.

Akizungumza hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Adrian Jungu, alisema kazi ya kuvuna chumvi imeanza baada ya taratibu zote za uvunaji kukamilika ikiwamo wananchi kufuata sheria.

Alisema tayari wananchi wameanza kuvuna chumvi na kwamba mchakato unaoendelea hivi sasa ni kuchanganya madini ya iodine na kupakia katika vifungashio tayari kwa matumizi ya nyumbani na maeneo mengine.

"Kupitia mradi huu wa uvunaji chumvi, serikali inategemea kukusanya ushuru lakini pia ajira zitazalishwa na wananchi kujiongezea kipato. Nawasihi wakazi wa maeneo haya kuutunza mradi huu ili uendelee kuwanufaisha," alisema Jungu.

Miongoni mwa wananchi wanaonufaika, Erick Mkamba, alisema mradi wa chumvi eneo la Itumbula ulianza kujengwa mwaka jana kwa michango yao na baadaye Rais John Magufuli aliongezea Sh. milioni 500 ambazo zimesaidia kutatatua changamoto ya vifungashio na maghala ya kuchakata bidhaa hiyo.

Alisema mradi huo utasaidia kubadilisha maisha yao kwa kuwa watajiongezea kipato na kufungua fursa zingine za biashara ndani ya mradi.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, alisema kilo 32,500 za chumvi zinakisiwa kuzalishwa kwa awamu moja.

Alisema mkoa unafanya jitihada za kuboresha zaidi miundombinu kuzunguka mradi huo ili kuongeza uzalishaji ili kuongeza huduma sokoni.

Mradi wa kuzalisha chumvi ulifufuliwa na wananchi baada ya kukwama kwa zaidi ya miaka 10 kwa sababu ya kukosekana kwa fedha za uendeshaji na sasa utakuwa miongoni mwa miradi ya kimkakati.



Wafanyabiashara na wadau wa madini wa Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara, wakifuatilia kikao cha elimu ya ulipaji kodi na ushuru juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wajengewa uwezo wa ufuatiliaji rasilimali

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

SHIRIKA la Kuhudumia Watoto Tanzania (CST), limezindua mradi wa kuwajengea uwezo wananchi katika ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali za umma jijini Mbeya.

Akizungumza juzi kwenye uzinduzi wa mradi huo, Mkurugenzi wa Shirika hilo, Noela Msuya, alisema mradi huo una lengo la kuonyesha uwajibikaji na utendaji kazi ili wananchi kuwa na ari ya usimamizi wa rasilimali mbalimbali za umma.

Alisema mradi huo utamsaidia mwananchi kufuatilia mapato na matumizi ili kuchochea uwajibikaji kwa viongozi na kujipatia maendeleo katika jamii.

"Ufuatiliaji wa mapato na matumizi kuanzia ngazi ya mtaa unalenga kuongeza uwajibikaji na kuboresha upungufu unaojitokeza. Nawasihi wananchi kuunga mkono mradi huo ili uwe chachu ya kuleta mabadiliko ndani ya jamii," alisema Msuya.

Ofisa Ufuatiliaji wa CST, Victor Sizya, alisema mradi huo unalenga kuongeza ufuatiliaji wa rasilimali za umma na kuwajengea uwezo wananchi kusimamia miradi yao ili kuwawajibisha viongozi pindi wanapobaini ubadhirifu.

Akizungumza kwa Niaba ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Ofisa Utumishi wa Jiji hilo, Gerald Ulizita, alisema mradi huo utakuwa chachu ya maendeleo katika ruzuku inayotolewa na serikali kwa ajili ya kuwezesha makundi ya watoto wenye uhitaji maalum kupata elimu.

Alisema mradi huo utachochea uwapo wa elimu jumuishi ambayo itahusisha watoto wenye mahitaji maalum na wengine ili kuhakikisha wanapata elimu na kwamba fedha za ruzuku zinazopatikana katika Halmashauri ya Jiji hilo zitasaidia kwa makundi hayo.

Miongoni mwa washiriki akiwemo, Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Airport, Simon Mwandambo, alisema elimu hiyo ni muhimu kuwafikia wananchi wa maeneo mbalimbali ya jiji la Mbeya.

Alisema elimu itawasaidia wananchi kutambua wajibu wao katika kushiriki shughuli za maendeleo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Iyunga, Oliver Mgeni, alisema kila mwananchi anapaswa kuwajibika mwenyewe bila kulazimishwa na kwamba kupitia viongozi wa maeneo wanapaswa kushiriki kwenye mikutano mbalimbali ikiwemo ya shule.

Shule 22 za msingi katika Jiji la Mbeya zitanufaika na mradi huo ambao umeanza mwaka huu.



# Vijana waliohitimu wachangamkia fursa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UMOJA wa vijana waliohitimu vyuo vikuu umeanzisha mfumo wa soko kiganjani (Ijen Store) ili kuwatafutia soko wakulima wa mbogamboga na kuwafundisha jinsi ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao hayo.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Ijen Agripreneurship, John Ngalaba, wakati alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mafunzo wanayotoa kwa wajasiriamali wanaolima mbogamboga katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya jiji la Dodoma.

Alisema wameamua kuanzisha mfumo huo ambao ni rahisi kuwasaidia wakulima hao vijijini na mijini ili kuepuka hasara ambayo wamekuwa wakipata wakati wa kilimo hicho.

**Bado kuna changamoto kwa baadhi yao kufanya biashara zao kwa kukiuka sheria hizo.**

Alisema wanawafundisha jinsi ya kutunza mboga zikiwa shambani na zinapofika sokoni.

"Pia, mfumo huu unawasaidia kupata soko kirahisi kwa sababu Ijen inawafuata wakulima shambani na kuwafundisha ikiwamo kuwapa elimu jinsi ya kutumia soko la kiganjani ili kuokoa bidhaa zisiharibike."

"Tumeamua kuanzisha mfumo huo baada ya kutembelea maeneo mengi ya wakulima na kuona mbogamboga na mazao mengine yanavyoharibiwa na wadudu katika bustani," alisema Ngalaba.

Alisema baada ya kuona hivyo waliamua kubuni njia hiyo ambayo imeonekana kuwasaidia wakulima hao na mazao mengine kwa sababu imewarahisishia jinsi ya udhibiti na upatikanaji wa soko kupitia mfumo huo.

"Tumeona mafanikio makubwa kwa baadhi ya sehemu ambazo tunawafundisha wengi wamefanikiwa kudhibiti bustani zao kupitia ushauri tunaowapa," alisema Ngalaba.

Alisema mpaka sasa wamefundisha wakulima wa mboga wa Ihumwa, vikundi zaidi ya 50 na walikuwa hawajui jinsi ya kuzitunza na kutafuta soko haraka.

"Pia tumetoa elimu kwa wakulima wa Mabwepande jijini Dar es Salaam na mfumo umeonekana kuwasaidia kwa kiasi kikubwa," alisema.

Naye, Meneja Masoko wa Ijen Store, Cynsia Lelo, alisema wakulima wameonekana kuitikia wito wa kutumia soko la kiganjani kwa sababu linawasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza upotevu wa bidhaa zao shambani.

Kwa upande wao, baadhi ya wakulima hao katika eneo la Ihumwa, walisema mfumo huo umewasaidia kupata masoko kwa haraka na kuondokana na bidhaa zao kuharibikia shambani.



Shekhe wa Wilaya ya Bahi, Suleman Twalib (aliyevaa koti), akishiriki kukata nyama siku ya Eid El Hajj, iliyofanyika katika Msikiti wa Taqwa Kigwe, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Lukuvi atoa somo ulipaji kodi ardhi, majengo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wananchi kutumia simu zao kulipa kodi ya ardhi na majengo ili kuondokana na vitendo vya kurubuniwa na maofisa ardhi kupunguziwa malipo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akifafanua kuhusu upotevu wa fedha za mapato ya kodi za malipo ya ardhi na majengo, jijini hapa.

Alisema hakuna sababu ya mwananchi kwenda kwa ofisa ardhi kuulizia deni analodaiwa katika jengo, kinachotakiwa ni kutumia simu yake ili kupata maelekezo ya nini anatakiwa afanye ili kukamilisha taratibu za malipo.

"Nawaomba wananchi kuweni makini na suala zima la ulipaji kodi za ardhi na majengo, msikubali mapatano na maofisa ardhi hata kama unahisi unadaiwa deni kubwa, tumia simu yako ya kiganjani itakupa maelekezo ya ulipaji pamoja na gharama husika," alisema Lukuvi.

Alisema serikali imeamua kufanya hivyo ili kuendelea kuwadhibiti maofisa wanaowarubuni wananchi kuwapunguzia gharama wanazodaiwa.

Akifafanua zaidi, alisema wizara yake imejipanga kusafisha uozo wote ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kutoka katika wizara hiyo hususan kwenye ulipaji kodi hizo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wananchi walisema mfumo wa kujua gharama za kodi ya majengo na ardhi kupitia simu utawasaidia kwa kiasi kikubwa kuepuka kutapeliwa na maofisa ambao sio waadilifu.

## Watakiwa kuchagua viongozi waadilifu

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WANANCHI wametakiwa kuchagua viongozi wenye sifa na waadilifu kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Mzee Mkongea Ally, wakati ulipotembelea Wilaya ya Kongwa na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ally alisema, katika uchaguzi huo wananchi wanatakiwa kuwachagua viongozi wa serikali za mitaa wenye sifa ili waweze kuwatumikia vizuri na watakaowaletea maendeleo kwenye maeneo yao.

"Kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru mwaka huu ni: 'Maji ni haki ya kila mtu tutunze vyanzo vyake', na tukumbuke kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo tukumbuke kuchagua viongozi wenye sifa katika uchaguzi huo," alisema.

Alisema uchaguzi huo ni muhimu kutokana na viongozi hao kutakiwa kuwajibika kwa wananchi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mtaa.

Awali, akitoa taarifa ya mradi wa maji Mtanana B, Mhandisi wa Maji wa Halmashauri ya Kongwa (MUWASA), Asha kilua, alisema gharama ya mradi huo ni Sh. milioni 7.7 na utahudumia wakazi 4,470.

Vile vile, alisema katika gharama hizo mchango wa wananchi ni Sh. milioni 4.5 na fedha zilizobaki zimetolewa na serikali kuu pamoja na wahisani.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, alisema Mwenge huo utazindua miradi saba katika wilaya hiyo ambayo imegharimu Sh. milioni 25.3.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni wa maji Mtanana B, vyumba viwili vya madarasa Shule ya Sekondari Pandambili, jengo la maabara hospitali ya Wilaya ya Kongwa, klabu ya kuzuia na kupambana na rushwa Shule ya Msingi NDC Narco na kuweka jiwe la msingi kiwanda cha maziwa Mbande.

**Kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru mwaka huu ni: 'Maji ni haki ya kila mtu tutunze vyanzo vyake', na tukumbuke kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo tukumbuke kuchagua viongozi wenye sifa katika uchaguzi huo.**



# Rais Shein ahimiza umoja ibada ya Iddi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wananchi kuendelea kudumisha amani na utulivu.

Dk. Shein aliyasema hayo jana katika hotuba yake aliyoitoa katika Baraza la Idd el Haj lililofanyika katika viwanja vya Langoni, Wilaya ya Magharibi A, ambalo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali na wananchi.

Katika hotuba yake, Dk. Shein alisema bila ya amani, maendeleo hayawezi kupatikana na hata waumini hawataweza kupata wasaa wa kufanya ibada kwa utulivu.

"Tunayasikia matukio mbalimbali ya kusikitisha yanayotokea katika mataifa mengine ambako amani imekosekana. Yanayotendeka huko ni vurugu, udhalilishaji na ukatili wa kila aina. Waumini wenzetu wamo ndani ya fadhaa, hawana maendeleo, hawana hata utulivu wa kufanya ibada," alisema Dk. Shein.

Alisema amani ni miongoni mwa baraka ambazo Mwenyezi Mungu amezitoa kwa wananchi na iwapo itachezewa kwa kujihusisha na vitendo vya uvunjifu wa sheria, itakuwa neema hiyo waliyopewa wanaikufuru na Mwenyezi Mungu atakuwa hayuko radhi.

**Tumshukuru Mola wetu kwa kutujalia kuwa na amani katika nchi yetu. Kila nikipata nafasi ya kuzungumza nanyi wananchi wenzangu, nimekuwa nikisisitiza juu ya umuhimu wa kuendelea kudumisha amani.**

"Tumshukuru Mola wetu kwa kutujalia kuwa na amani katika nchi yetu. Kila nikipata nafasi ya kuzungumza nanyi wananchi wenzangu, nimekuwa nikisisitiza juu ya umuhimu wa kuendelea kudumisha amani," alisema.

Dk. Shein pia alisema kutokana na kuendelea kuwapo kwa amani na utulivu, Zanzibar inaendelea kupiga hatua na kuimarika kwa uchumi wake kwa kila mwaka. Alisema hali hiyo ya kukua kwa uchumi inaiwezesha Serikali kupata nguvu zaidi za kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kutoa huduma mbalimbali ambazo wananchi wanazihitaji kwa ajili ya maisha ya kila siku katika hali bora zaidi.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, ukuaji huo wa uchumi umeiwezesha Serikali kuimarisha maslahi ya wafayakazi wa SOerikali na kuinua kipato chao na kupata uwezo wa kuitekeleza mipango mbalimbali wanayoipanga.

Rais Shein alisema ni jambo la faraja kuona kuwa hali hiyo pia imewawezesha baadhi ya watumishi kupata uwezo wa kifedha kwenda kutekeleza ibada ya Hijja mapema badala ya kusubiri fedha za kiinua mgongo kama ilivyozoeleka.

Pia Alhaj Dk. Shein aliwahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kwa wale wenye uwezo wa kifedha na afya njema, kuepukana na vipingamizi visivyo vya msingi ambavyo vinaweza kusababisha kushindwa kwenda kuitekeleza ibada ya Hijja.

Dk. Shein pia aliwataka wananchi kujitahidi kuwalea watoto sambamba na kuwarithisha misingi ya kuheshimu, kukinai na kuthamini vilivyo vyao kwa kuwa hiyo ni misingi ya uzalendo na kuwafunza maadili mema, silka, desturi na utamaduni waliourithisha kutoka kwa wazee.

Baraza hilo la Iddi pia lilihudhuriwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan; Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd; Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume na viongozi wengine wa vyama vya siasa, Serikali na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao Zanzibar.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mwanamwema Shein (katikati) na Makamo wa Rais, Samia Hassan pamoja viongozi wengine wakisikiliza hotuba iliyotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), katika sherehe za Baraza la Eid El Hajj zilizofanyika katika Viwanja vya Langoni, Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Watakiwa kutafakari elimu jumuishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU mbalimbali wa elimu jumuishi, wametakiwa kutafakari kwa kina juu ya dhana hiyo ili kuhakikisha kila mtoto mwenye mahitaji maalum anapata elimu kuanzia maandalizi, msingi hadi sekondari.

Akizungumza wakati wa warsha ya kujadili mwendelezo wa utoaji wa elimu jumuishi katika shule na vyuo, Naibu katibu Mkuu Utawala, Mwalimu Abdullah Mzee, alisema ni lazima kila mmoja kutafakari juu ya hali hiyo ili dhamira ya watoto ya kusoma iwafikie.

Mwalimu alisema bado kuna matatizo kadhaa katika baadhi ya sehemu juu ya utoaji wa elimu hiyo ikiwamo mitaala, vitabu na walimu, hivyo ni vyema vikarekebishwa ili kuasaidia utoaji wa elimu kwa mafanikio na kuwafanya watu wenye mahitaji maalum kupata elimu.

Alisema kuna baadhi ya makundi yanaonekana kusahauliwa kutokana na umasikini katika familia zao hali ambayo inawafanya kukosa fursa yao ya msingi ya kupata elimu, hivyo lazima wote wafikiwe.

Akiwasilisha mada tofauti Mkuu wa Kitengo cha Elimu Jumuishi na Stadi za Maisha, Mpaji Ali, alisema bado baadhi ya watu wenye mahitaji maalum wanakosa elimu kutokana na uchache wa shule kulinganisha na wingi wa watoto. Alitaja sababu nyingine kuwa ni unyanyapaa katika baadhi ya shule.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wadau wote na jamii kwa ujumla, kuendelea kushirikiana kwa kuwatoa watoto wenye mahitaji maalum na kuacha unyanyapaa ili nao wapate elimu kama watoto wengine.

Baadhi ya washiriki wa warsha hiyo walisema bado kuna matatizo kwa baadhi ya walimu kukataa kwenda kufundisha katika shule zenye wanafunzi wenye uhitaji maalum hali ambayo inachangia kukosekana kwa elimu kwa watoto hao.

Pia aliwashauri kuingizwa katika mitaala somo la lugha ya alama tokea darasa la kwanza ili wanafunzi waweze kuwasiliana wao wenyewe pamoja na watu wenye mahitaji maalum yakiwamo ya uziwi.

# Waongeza muda utekelezaji mradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema wamekubaliana na wasimamizi wa mradi wa huduma za jamii mjini (ZUSP) kuongeza muda wa ufanyaji kazi katika ujenzi wa mradi wa miundombinu wa mtaro ya kupitishia maji ya mvua eneo la Mikunguni ili kuimarisha mawasiliano ya usafiri.

Ayoub alisema hayo juzi baada ya kufanya ziara ya kuangalia undelezaji ujenzi wa eneo hilo na kusema ujenzi wa miundombinu hiyo umesababisha kujitokeza kwa usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaotumia barabara hiyo wakiwamo wafanyabiashara.

Ujenzi huo, alisema umesababisha barabara ya Mkunguni kufungwa kwa miezi miwili mpaka sasa na kwamba hali hiyo imesababisha usumbufu kwa watumiaji.

"Kutokana na hali hii tumekubaliana na wasimamizi wa mradi kwanza kusitisha ujenzi na kufungua njia kwa kipindi hiki cha sikukuu hadi wiki ijayo lakini pia kuongeza muda wa ufanyaji kazi mchana na usiku ili kuharakisha na kumaliza haraka kazi hiyo," alisema.

Mkuu wa Mkoa pia alisema kumekuwa na shughuli nyingi za maendeleo zinazofanyika katika maeneo ya mkoa huo na kusababisha msongamano wa magari na usumbufu kwa wananchi hatua ambayo kwa sasa serikali inajitahidi kuipatia ufumbuzi wa haraka.

"Tumeelezwa kuwa usumbufu wa kufungwa kwa barabara hii inatokana na kuharibika kwa mitambo ya utoaji wa vyuma katika ujenzi huu na ikawabidi wakakodi vifaa Dar es Saalam, hivyo tumeshuhudia mtambo huu umeanza kufanya kazi. Ni imani yangu kuwa barabara hii itafunguliwa hivi karibuni," alisema.

Ayoub aliwaomba wananchi wa mkoa huo kuendelea kuwa wastahamilivu katika kipindi hiki huku harakati za kuimarisha miundombinu hiyo ikiendelea.

Naye Mapema Mratibu wa ZUSP, Makame Ali Makame, alitaja sababu ya kufungwa kwa barabara hiyo kwa kipindi cha muda mrefu ni mvua na mitambo ambayo ilishindwa kufanya kazi.

Alisema mpaka sasa mitambo minne ililetwa katika ujenzi wa mradi huo kwa ajili ya kuchomoa vyuma ambavyo viliwekwa katika msingi huo na hatimaye ikashindwa kufanya kazi.

**Mpaka sasa mitambo minne ililetwa katika ujenzi wa mradi huo kwa ajili ya kuchomoa vyuma ambavyo viliwekwa katika msingi huo na hatimaye ikashindwa kufanya kazi.**

# Wakulima wa korosho sasa wapewa matumaini mapya

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI imewapa matumaini mapya wakulima wa korosho ambao hawajakamilishiwa malipo yao kutokatatamaa kwa kuwa wanunuzi wamepatikana, hivyo Korosho zote zilizopo maghalani zitanunuliwa muda mfupi kuanzia sasa.

Kauli ilitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, alipokuwa akiyafunga Maonesho ya 27 ya NaneNane Kanda ya Kusini, katika viwanja vya Ngongo Manispaa ya Lindi.

**Nachukuwa nafasi hii kuwaelezeni kwamba korosho zote zilizopo maghalani kuanzia kusini hadi Dar es Salaam zimepata wanunuzi.**

Mgumba alisema wakulima hawana sababu za kukata tamaa ya kutolipwa fedha zao za Korosho kwa kuwa bado uhitaji wa zao hilo duniani mkubwa, na kwamba wanunuzi wamepatikana.

"Nachukuwa nafasi hii kuwaelezeni kwamba korosho zote zilizopo maghalani kuanzia kusini hadi Dar es Salaam zimepata wanunuzi," alisema Mgumba.

Alisema kutokana na mahitaji makubwa ya korosho katika soko la nje, hata zile tani 512,000 zilizopo kwenye maghala hazitosherezi, na kwamba dalili zimeanza kuonekana kwamba korosho za mwaka huu zitakuwa na soko kubwa na bei stahiki.

"Kufuatia ubora wa korosho zetu, upo uhakika mkubwa bei ya zao hili kwa mwaka huu ukawa mzuri zaidi," alisema Mgumba.

Alikanusha taarifa zinazoendelea kutolewa kwamba korosho zilizopo kwenye maghala zimeoza, huku akiwataka wananchi kupuuza madai hayo kwa kuwa wanunuzi wamepitishwa na kuzikagua na kubaini ni mzima.

Aliwataka wananchi wa Lindi na Mtwara wajielekeze kulima mazao mengine mchanganyiko yanayostamili ukame yakiwamo ufuta, alizeti, karanga, mbaazi na muhogo yaweze kuwaongezea mapato, badala ya kuangalia zao moja la korosho pekee.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, amehaidi kufanyia kazi ushauri wa Nainu Waziri huyo kwa kutekeleza kilimo cha mazao mchanganyiko ili waondokane kutegemea zao la korosho na ufuta.



Wanahisa wa Kampuni ya TCCIA Investment PLC wakifuatilia mada katika Mkutano Mkuu wa 14 wa Mwaka uliolenga kujadili ukaguzi wa mahesabu na kutoa mapendekezo katika kuboresha utendaji wa kampuni hiyo ili kuongeza faida katika uwekezaji, jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waomba kibano makandarasi wachelewesha miradi mikubwa

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imeombwa kuweka kipengele cha kuwabana makandarasi wa miradi mikubwa ya ujenzi wa majengo na barabara kununua vifaa vya ujenzi, ili kuvijengea uwezo viwanda vilivyopo vinavyozalisha bidhaa hizo nchini.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Lodhia Group, Sailesh Pandit alisema kutokana na msamaha wa kodi unaotolewa kwa makandarasi huwachochea kununua vifaaa hivyo ikiwamo nondo nje ya nchi kwa wingi hatua ambayo inavidhorotesha viwanda vya ndani.

Pandit aliyasema hayo kiwandani kwake wakati akizungumza wilayani Mkuranga Mkoa wa Pwani katika ziara ya wajumbe wa mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwishoni mwa wiki.

Alisema hatua hiyo licha ya kudhorotesha viwanda pia huchangia ufinyu wa ajira kwa wananchi, kwa kuwa wenye viwanda hulazimika kuzalisha bidhaa chache kulingana na soko husika.

"Kwa sasa wafanyakazi wetu wanazalisha kwa saa 8 pekee, lakini tungekuwa na uhakika wa soko ni wazi kwamba tungekuwa tunafanya uzalishaji bidhaa nyingi hivyo tungelazimika kuajiri wengi pengine hata mara mbili ya waliopo sasa," alisema.

Alibainisha kuwa wameajiri wafanyakazi 600, huku kiwanda hicho kuwa na uwezo wa kuzalisha tani 10,400 kwa mwezi na kinazingatia kiwango cha ubora TBS.

"Ni jambo la kushangaza tunafanikiwa kuuza hadi tani 2,000 huko Congo, tunatarajia kujitanua zaidi kwenye nchi nyingine, wakati nchini kuna miradi mikubwa inaendelea tungeweza kuuza zaidi bidhaa zetu," alisema.

# Wanafunzi elimu ya juu kupata mkopo bila riba

**Na Joseph Mwendapole**

MAMIA ya wanafunzi wa vyuo vikuu wanatarajiwa kunufaika na mikopo ya elimu ya juu baada ya Kampuni ya Global Education Link ya jijini Dar es Salaam kuanza kuwakopesha bila riba.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Mikopo wa Kampuni hiyo, Mariam Sagini,

Mariam alisema wanatoa mikopo hiyo kwa wanafunzi wanaowapeleka nje ya nchi ambao wazazi wao hawana uwezo wa kulipa ada yote kwa mkupuo mmoja.

Alisema kuna vyuo ambavyo havikubali malipo ya awamu, hivyo wameona wasaidie kuwapunguzia mzigo wazazi ambao watashindwa kulipa kwa mkupuo mmoja.

"Mwaka wa masomo wa 2018/19 idadi ya walioomba mikopo hii ilikuwa kubwa sana na mwaka huu wa masomo tumeshaanza kuona idadi itakuwa kubwa sana sisi tunawapa na wanalipa ndani ya miezi minane hatutozi riba analipa alichochukua tu," alisema.

Kuhusu ushindi wa kwanza kwa upande wa elimu wa taasisi hiyo katika maonyesho Nanenane Simiyu na kupkabidhiwa tuzo na Waziri Mkuu msttafu, Mizengo Pinda, Ofisa Ufuatiliaji wa Kampuni hiyo, Hemed Mlapakolo, alisema kwenye kipengele hicho cha elimu wao walikuwa wa kwanza na mshindi wa pili aliibuka Chuo Kikuu cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), kiliibuka kuwa mshindi wa tatu.

Alisema walipatiwa cheti cha kombe kama sehemu ya kutambua mchango wa kampuni hiyo katika sekta ya elimu kwa kufanikisha wanafunzi wengi kujiunga na vyuo vikuu ndani na nje ya nchi.

Awali, Hemed alisema kwenye maonyesho hayo walitembelewa na Waziri Mkuu ambaye aliuliza iwapo wamefanyia kazi maelekezo aliyoyatoa kwenye maonyesho ya vyo vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) Mnazi Mmoja Dar es Salaam.

Kwenye maelekezo hayo, Waziri Mkuu alitaka kujua kama wanaishirikisha TCU kwenye ukaguzi wa vigezo vya vyuo vikuu ambavyo wamekuwa wakiwapeleka wanafunzi hao nje ya nchi.

"Tulimweleza kuwa tunalifanya hilo kwa kushirikiana na TCU na taasisi zingine za serikali lakini pia tulimweleza kuhusu huduma zingine tunazotoa kama mikopo kwa wanafunzi, Waziri Mkuu alifurahi na akasema anatamani kama kampuni zingine zingekuwa zinafanya kama Global Education Link," alisema.

HABARI KIMATAIFA

## Mvutano wazuka ndani ya serikali ya Italia

**ROMA, Italia**

KIONGOZI wa chama kinachotawala nchini Italia, ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani, Matteo Salvini, ameitisha uchaguzi mapema baada ya kutangaza kwamba serikali ya muungano haiwezi kuendelea kufanya kazi.

Hatua hiyo inafuatia miezi kadhaa ya mikwaruzano ndani ya serikali hiyo ya miezi 14, kati ya Chama cha siasa kali za mrengo wa Kulia na washirika wake.

Hali ya mgogoro serikalini, imeiweka Italia ya tatu kwa uchumi mkubwa katika nchi zinazotumia sarafu ya Euro katika hali ngumu ya kisiasa, isiyoweza kutabirika.

Katika taarifa yake, Salvini alisema alimwambia Waziri Mkuu Giuseppe Conte, ambaye sio mwanachama wa muungano wowote unaounda serikali, kwamba muungano wa serikali umevunjika na kwamba kwa haraka, anastahili kuwapa mamlaka wapiga kura kufanya maamuzi.

Alhamisi, Salvini alihutubia wafuasi wake katika Mji wa Pecara, pwani ya Adriatic, na kusema muda umewadia kwa wapiga kura wa Italia kufanya uamuzi. Waziri Mkuu huyo ambaye ameshiriki katika duru kadhaa za mazungumzo kutafuta suluhu la mgogoro serikalini, hata hivyo alisema sio wajibu wa Salvini kuitisha kikao cha bunge, wala kuweka mda wa kusuluhisha mgogoro wa kisiasa, na kwamba viongozi wengine wanastahili kuingilia kati.

Conte, alimtaka Salvini kujieleza ni kwa nini anataka serikali kuvunjwa.

Bunge la Italy, ambalo sasa limo katika mapumziko, huenda likarejea katika vikao vyake wiki ijayo ili kuchukua hatua muhimu.= Kwa mujibu wa Katiba ya Italy, kabla ya serikali kuvunjwa, bunge linastahili kupiga kura ya kutokuwa na Imani na serikali, na Waziri Mkuu kujiuzulu. **VOA**

# UN wang'ang'ania Libya

**TRIPOL, Libya**

NAIBU Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya amani, Bintou Keita, amesema kwamba Umoja wa Mataifa (UN) hauna nia ya kuondoka wala kutoka Libya licha ya mauaji ya wafanyakazi wake watatu Jumapili.

Watu hao waliuawa kutokana na mlipuko wa bomu lililokuwa limetegwa ndani ya gari mjini Benghazi, mashariki ya nchi hiyo.

Shambulio hilo la Jumamosi asubuhi limetokea wakati UN inajaribu kutafuta suluhisho la kusitisha mapambano yaliyoanza Aprili katika Mji Mkuu wa Tripoli. Mapiganao hayo yalianzishwa na wanamgambo wa national Army wenye makazi yao mashariki ya nchi ya Libya, yakiongozwa na Jenerali aliyeasi, Khalifa Haftar yakiwa na lengo la kuipindua serikali inayotambuliwa na UN, na mpaka sasa mapinduzi hayo hayajafanikiwa.

Baraza la Usalama la UN lilikutana katika kikao cha dharura jana kujadili suala la Libya. **VOA**



Waandamanaji Hong Kong wakipambana na Jeshi la Polisi jana katika Uwanja wa Ndege. **PICHA: REUTERS**

## Kampuni za kubeti zalaumiwa kufilisi wateja

**LONDON, Uingereza**

IDADI ya wacheza kamari wanaolalamika kuhusu kampuni za kamari ya Uingereza imepanda kwa karibu asilimia 5,000 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kwa mwaka jana kulikuwa na malalamiko 8,266, rekodi iliyokusanywa na tume inayohusika na michezo ya kamari, ikilinganishwa na malalamiko 169 mwaka 2013.

Malalamiko mengi yalihusu kampuni kukataa kulipa washindi au kushindwa kufanya kazi katika hali ya kuwajibika ipasavyo.

Ongezeko hilo limekuwapo kutokana na ongezeko kubwa la michezo hiyo ya kamari nchini Uingereza.

Kampuni makubwa ya kamari yameahidi kutenga pauni milioni 60 kwa mwaka kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili wacheza kamari na kusema kuwa wanafanyia kazi mpango wa kupunguza athari zitokanazo na kamari.

Mkurugenzi wa Tume ya udhibiti wa michezo ya kamari, Neil McArthur, alisema kuna sababu za ongezeko la malalamiko hayo.

"Tunalazimisha soko la michezo ya kamari kufahamu wateja wake, na hii pengine ni ishara njema kwa sababu inawafanya wateja kutaka uwepo usimamizi zaidi na ningependa waendelee kufanya hivyo," alisema McArthur.

Alisema soko limetanuka kwa haraka sana tangu serikali ilipopunguza vikwazo kwenye soko la kamari na matangazo mwaka 2007.

Alisema wacheza kamari kwa sasa wanapoteza karibu mara mbili zaidi ya kampuni za kamari yalivyokuwa yakipoteza miaka 10 iliyopita. McAthur alisema kwa mwaka jana, wacheza kamari walirekodiwa kupoteza kiasi cha pauni bilioni 14.5.

Ongezeko kubwa liko kwenye kamari inayochezwa mtandaoni, ambapo michezo mipya imewavutia wateja wapya. **BBC**

## Maandamano yasababisha kusitishwa safari za ndege

**HONG KONG, China**

MAOFISA wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Hong Kong wamesitisha Jumatatu usafiri wa ndege katika kiwanja cha ndege cha jimbo hilo ambacho ni mojawapo ya viwanja vyenye usafirishaji mkubwa wa watu na mizigo duniani.

Kusitishwa kwa shughuli za kiwanja hicho kunatokana na shinikizo la waandamanaji ambao ni wanaharakati wa mji huo ambao wamevamia uwanja huo na kusababisha shughuli zote kusimama.

Polisi wa Hong Kong wamewambia waandishi habari kwamba wanaharakati wapatao elfu 5 waliwasili na kukusanyika kwenye ukumbi wa kuondoka wasafiri kwa siku ya nne, tangu siku ya Jumatatu.

Wakati huo huo, idadi kubwa ya waandamanaji wamejeruhiwa Jumatatu katika mitaa mingi ya Jimbo la Hong Kong katika mapambano na polisi wa kuzuia ghasia.

Waandamanaji wenye hasira wamezuia barabara na kukaidi amri ya polisi ambao wametumia gesi ya kutoa machozi na risasi za plastiki kuwatawanya waandamanaji.

Serikali ya Jimbo la Hong Kong iliyo chini ya mamlaka ya China imesema watu 54 wamejeruhiwa katika ghasia hizo.

Viongozi wa china wametaja maandamano ya Jumatatu kama vitendo vya ugaidi.

Wakati huo huo, Kiongozi wa Hong Kong, Carrie Lam ameonya kuwa maandamano ambayo yamekuwa yakiendelea kwenye mji huo, yanaharibu uchumi.

Lam alitoa kauli hiyo wakati mgomo wa siku tatu ukianza katika uwanja wa ndege wa Hong Kong.

Aidha, kiongozi huyo wa Hong Kong ameapa kuwa licha ya maandamano hayo kuendelea, uongozi wake haupo tayari kulegeza kamba kuhusu matakwa ya waandamanaji. Waandamanaji wamekuwa na mkutano na wafanyabiashara katika mji huo na kuhamasisha wakazi wa Hong Kong kwenda katika uwanja wa ndege kukaa kwa siku tatu, ili kupata uungwaji mkono wa kimataifa.

Wanaharakati Hong Kong, wanapinga mpango wa uongozi wa eneo hilo kupitisha sheria ambayo itaruhusu wakazi wa eno hilo kushtakiwa nchini China, kwa kile wanachosema, wanaolengwa ni wapinzani wa serikali ya Beijing.

Serikali ya China inasema haitavumilia kuendelea kushuhudiwa kwa maandamano hayo wanayosema yanaharibu mji huo. **VOA**

# Wananchi wataja vigingi vinne kwa mbunge wao

**Na Lulu Mussa, SINGIDA**

VIONGOZI wa Tarafa ya Mandewa wilayani Singida wamemwomba Mbunge wa Singida Mjini, Mussa Sima (CCM), kutatua changamoto nne zinazoikabili tarafa yao.

Kero hizo ni uhaba wa maji, ubovu wa miundombinu ya barabara, kutokuwa na umeme na moshi unaotoka kwenye moja wa kiwanda unaohatarisha afya zao.

Viongozi hao walieleza kero hizo kwa niaba ya wananchi walipozungumza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye tarafa hiyo juzi na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa jimbo hilo wakiwamo madiwani wa kata zote 18 za jimbo hilo.

Walisema suala la maji limekuwa kero kubwa hasa kwenye vitongoji vilivyoko mbali na mji huo kwa kuwa visima wanavyovitegemea vimekauka kutokana na ukame huku wakimwomba kuingilia kati suala la moshi kutoka viwandani.

"Tarafa ya Mandewa ni kubwa na imekuwa na mwamko mkubwa wa wawekezaji kununua viwanja lakini hawajengi kwa sababu hakuna maji ya uhakika, vijana wetu wanakosa ajira za muda," alisema Maulid Sima, kiongozi wa tarafa hiyo.

Godfrey Mumwi, kiongozi mwingine wa tarafa hiyo, alisema wanashindwa kuanzisha shughuli mbalimbali za ujasiriamali katika eneo lao kutokana na kutokuwapo kwa nishati ya umeme.

"Kuhusu suala la maji tunatumia visima ambavyo ikifika mwezi wa tisa (Septemba) vinakauka, vinajaa maji hadi mvua ya awamu nyingine inyeshe, umekuja kijana wetu (Sima), tutapata ahueni na tutashirikiana nawe bega kwa bega ili kuzitatua kero hizi," Mumwi alisema.

Katika mkutano huo, Sima ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), aliwatoa hofu viongozi na wananchi kuhusu utatuzi wa kero hizo huku akiwashukuru kwa kumkumbusha suala hilo kwa kuwa analifahamu.

"Kuhusu kero ya moshi, ndani wiki hii nitatuma wataalamu kutoka wizarani kwa ajili kwenda katika kiwanda kile, pia watazungumza nanyi ana kwa ana. Mwenyekiti aandae mkutano tu, siwezi nikakubali wananchi kuendelea kuteseka.

"Taarifa ya wataalamu itatusaidia kufanya uamuzi, ondoe hofu. Nimepata taarifa ya kuwa moshi huo na majitaka katika kiwanda hicho yanafunguliwa usiku na kilishawahi kupigwa faini ya Sh. milioni 20 na mtangulizi wangu (Kangi Lugola) alipokitembelea," Sima alisema.

Kuhusu maji, Sima alisema Wilaya ya Singida Mjini imetengewa zaidi ya Sh. bilioni 33 kwa ajili ya kuboresha huduma za maji na anaamini fungu hilo litamaliza kero hiyo.

Alisema uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika jimbo hilo pia unashughulikiwa na Serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijijini (Tarura).

Mbunge huyo pia alitoa mabati 50 kwa ajili ya ujenzi ya Shule ya Msingi Mwaja na mifuko ya saruji 80 kwa Kata ya Magwanjuki huku akiahidi kujenga Kituo cha Polisi cha Mandewa.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (wa pili kulia), akikabidhi tuzo kwa mwanafunzi Kelvin Victor, wakati wa mahafali ya wanafunzi waliosoma nje ya nchi kupitia kampuni ya Global Education Link, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Wa (pili kushoto), ni Mkurugenzi wa Global Education Link, Abdulmalik Mollel na Mwenyekiti wa wazazi ambao watoto wao wanasoma nje ya nchi, Bonaventure Katuma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# Mwanafunzi huyu anatafutwa

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa darasa la saba katika Shule ya Tuwapende jijini Dar es Salaam, Daniel Evans (12), anatafutwa na wazazi wake baada ya kuondoka nyumbani na kwenda kusikojulikana.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Evans Rubara, aliyefika jana kwenye ofisi za gazeti hili Mikocheni jijini Dar es Salaam, alidai Daniel aliondoka nyumbani Jumamosi iliyopita majira ya asubuhi.

"Wakati Daniel akiondoka nyumbani, nilikuwa nimekwenda kwenye kikao cha wazazi shuleni kwao, niliporudi ndugu yangu ambaye nilimwacha naye, alisema mtoto alitoka kwenda nje kucheza, tulipoona kimya, tulianza kumtafuta maeneo mbalimbali bila mafanikio," alidai.

Alisema tayari alishatoa taarifa Kituo cha Polisi Mbweni jijini kuhusu kupotea kwa mtoto wake huyo na taarifa hiyo kupewa namba RB/273/019.

Alidai kuwa Jumapili katika harakati za kumtafuta, walipofika kituo cha daladala Kwa Jumbe, baadhi ya waendesha bodaboda walidai walimwona akipita eneo hilo.

Alidai kuwa jana pia walipata taarifa kutoka kwa Mwalimu Mkuu wa shule anayosoma mtoto wake, Daniel alionekana maeneo ya Kerege siku hiyo.

"Daniel alionekana Kerege ambako alikwenda kumtafuta rafiki yake aitwaye Hilally. Tulikwenda kwa Hilally, tukamkuta babu yake ambaye alitueleza kuwa, Daniel alifika hapo Jumamosi kumtafuta Hilally ambaye wakati huo alikuwa hayupo, tulikaa naye hadi jioni na aliaga anaondoka," alidai.

Evans alidai kuwa kabla ya kuondoka aliulizwa kama ana nauli na alisema alikuwa na Sh. 200 na babu huyo alimwongeza Sh. 2,000 na aliahidi angerudi tena siku iliyofuata ili akutane na Hilally.

Alidai hadi jana saa saba mchana, mtoto wao alikuwa hajarudi nyumbani kwa rafiki yake huku akibainisha kuwa huwa na tatizo la pumu.

"Tunaomba yeyote atakayemwona Daniel atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu 0788 180 097 au 0655 832 600," aliomba.

# Serikali yatakiwa uwekezaji zaidi wa dawa za wajawazito

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeshauriwa kuwekeza katika upatikanaji wa dawa zinazotumiwa na wazazi wakati na baada ya kujifungua, ili kusaidia, pamoja na mambo mengine, kupunguza upoteaji damu unaoweza kusababisha vifo.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utetezi wa Afya (HDT), Dk. Peter Bujari, alipokuwa akizungumza na wahariri na wanahabari jijini Dar es Salaam. Dk Bujari alisema kufanikisha ufanisi katika kuokoa vifo vya wajawazito na watoto wachanga ni hatua muhimu itakayoiwezesha nchi kutimiza malengo ya kimataifa yanayohusu 'maeneo' hayo.

Mkutano huo ulifanyika baada ya HDT kupata taarifa maeneo tofauti, zikiashiria kutokuwapo hali nzuri ya upatikanaji dawa kwa ajili ya wajawazito.

Alisema wajawazito wanapojifungua wananyemelewa na maambukizi yanayopaswa kudhibitiwa, kifafa cha uzazi, upungufu wa damu, magonjwa ya moyo na kupotea kwa damu.

Kwa mujibu wa Dk Bujari hali hiyo inaweza kuzuiliwa ikiwa kituo cha afya ama hospitali zitakuwa na dawa za kutosha zinazojumuisha ferrous sulphate inayotumika kuongeza damu, misoprostol inayochomwa ili tumbo la mzazi lisinyae hivyo kuzuia upoteaji wa damu na oxytocin.

Dk. Bujari alikariri taarifa ya Bodi ya Madawa (MSD) ikionesha kuwa kwa kipindi cha Februari mwaka huu, dawa hizo zilikuwa kwa matumizi ya miezi inayoonekana kwenye mabano; ferrous sulphate (2), misoprostol (4) na oxytocin (3).

Alisema kwa mujibu wa utaratibu uliopo, dawa inayopatikana kwa kipindi cha kuanzia miezi mitatu inatosha kwa mahitaji miezi minne kwa MSD na miezi mitatu kwa kituo cha afya.

Dk. Bujari alisema katika kipindi cha Juni mwaka huu, upatikanaji dawa huo ulikuwa ferrous sulphate (3), misoprostol (3) na oxytocin (1). Dk Bujari alisema HDT kupitia ofisi zake za mikoani, imeshuhudia hali ya upatikanaji wa miongoni mwa dawa hizo kuwa sio mzuri na unatia shaka kuhusu wajawazito wanaojifungua huko.

Alivitaja vituo vya afya Nyakahura, Ngarambe, Lusahunga na Kalenge katika wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera, kwamba wamekuwa hali ya upatikanaji wa baadhi ya dawa hizo hauiridhishi.

Pia alivitaja vituo vya Kirushya, Murusagamba, Bukiriro na Keza mkoani humo kuwa ni miongoni mwa vituo vinavyokabiliwa na ukosefu ama upungufu wa dawa hizo kwa kipindi cha Februari na Juni, mwaka huu.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**GARI INAUZWA,** Toyota Land Cruiser Amazon Vx DIESEL AUTOMATIC no 'C' safi sana Bei 27 milion. Leyland DAf Tank ya maji Diesel Lita elfu 10 inatembea safi sana Reg. namba D bei ni Sh. 28 milion. Mawasiliano: 0713 227788/ 0713 469480

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311

Nipashe

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

**NEWSPAPER**

**CLASSFIED ADVERTISEMENT**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MOURINHO

## ASIFIA UKUTA WA MAGUIRE

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amemsifia Harry Maguire baada ya nyota huyo mpya wa Manchester United aliyetua hapo kwa pauni milioni 80 kufurahia mwanzo wake mzuri kwa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Chelsea katika mchezo wa Ligi Kuu England juzi.

Siku ambayo Maguire alianza kucheza pale Old Trafford Jumapili naye Mourinho mshidi mara tatu wa kombe la Ligi Kuu ya England alianza kuwa mchambuzi kwenye kituo cha televisheni cha Sky Sports.

Maguire, ambaye ndiye beki ghali zaidi duniani kwa sasa aliibuka kuwa nyota wa mchezo baada ya kucheza vizuri zaidi katika nafasi ya beki wa kati kwa Man United, jambo lililomuibua Mourinho.

"Kwa hakika alistahili tuzo ya kuwa nyota wa mchezo, aliweka ukuta mgumu kama jiwe," alisema Mourinho.

"Kwa upande wangu, Man United walikuwa wanahitaji beki kama Maguire kwa muda mrefu zaidi, na leo (juzi) alithibitisha kwamba yeye ni beki bora kabisa," alisema Mourinho.

Mouirnho wakati akiinoa Man United aliomba mara kadhaa kupatiwa beki wa kati kwa ajii ya kuimarisha kikosi chake, lakini hadi anafukuzwa Desemba mwaka jana hakuweza kufanikisha hilo.

Lakini kipindi hiki cha majira ya joto, Man United walifanikiwa kumtwaa beki huyo kutoka Leicester City kwa ada ambayo iliweka rekodi ya dunia.

# MANGALA WA MAN CITY KUTUA VALENCIA

**MANCHESTER, England**

BEKI wa Manchester City, Eliaquim Mangala yupo kwenye uwezekano wa kutua Valencia ya Hispania kwa mkopo kwa ajili ya kujiimarisha zaidi.

Raia huyo wa Ufaransa alikuwa beki ghali zaidi wa pili katika historia ya usajili kwenye Ligi Kuu ya England wakati alipotua hapo Etihad kwa dau la pauni milioni 31.8 akitokea Porto mwaka 2014.

Lakini baada ya kucheza mara kwa mara katika misimu yake miwili ya mwanzo, akajikuta anakosa nafasi na msimu wa 2016-17 na alipelekwa kwa mkopo Valencia na kipindi cha pili cha msimu wa 2017-18 alicheza pale Everton.



Mangala hajacheza mchezo wowote wa mashindano tangu Februari 2018, wakati akiwa kwa mkopo pale Goodison Park, kwa sababu ya kuumia goti.

Hata hivyo, baaada ya kupona sasa, Mangala atarudishwa tena Valencia kucheza kwa mkopo ili aweze kuimarika zaidi, kwa mujibu wa Goal.com

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Mangala hayupo kwenye mipango ya kocha, Pep Guardiola

# UNAI ARIDHISHWA NA KIWANGO CHA ARSENAL

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery anaamini timu yake itaimarika zaidi baada ya kupata ushindi wake wa kwanza kwenye mchezo wake wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Newcastle juzi Jumapili.

Arsenal ilipata ushindi huo wa bao la Pierre-Emerick Aubameyang na kuwafanya kuanza msimu wakiwa na pointi tatu mkononi.

Na sasa Emery anaona kwamba, watakwenda kwenye mchezo wao wa pili wa Ligi kuu wakiwa wanajiamini na ana matumaini ya kuimarika zaidi kwa kiwango chao kuliko kile walichokionyesha pale kwenye uwanja wa St James' Park.

"Ni pointi tatu nzuri zaidi," alisema kocha Emery ambaye ni raia wa Hispania akiiambia Sky Sports.

"Tulicheza mchezo mzuri na mgumu na tuliutawala, lakini tunaweza kuimarika zaidi, kwa sababu katika kipindi cha kwanza kwa mfano tulipoteza mipira mingi katikati na kuwazawadia wao nafasi.

"Kipindi cha pili kilifanana na kile cha kwanza, lakini jambo la msingi tulipata bao na ushindi ule umetufanya tuzidi kujiamini.

"Kiwango tulichokionyesha tuna nafasi ya kuimarika zaidi, maana tutakwenda kwenye mchezo wa pili tukiwa tunajiamini na kutaka kuendelea kupata ushindi," alisema.

Arsenal iliwatumia wachezajichipukuzi, Reiss Nelson na Joe Willock ambao ni raia wa Uingereza na walionekana kucheza vizuri.

Kuwajumuisha Nelson na Willock kwenye mchezo huo inamaana kwamba ni mara ya kwanza kwa Arsenal kuwaanzisha makinda wawili wa Uingereza kwenye kikosi cha kwanza katika mchezo wa Ligi Kuu tangu Februari mwaka 1998, wakati Paolo Vernazza na Matthew Upson walipochezea dhidi ya Crystal Palace, wakati ambao Willock na Nelson walikuwa bado hawajazaliwa.



HABARI MICHEZO



# LAMPARD

## ASEMA CHELSEA HAIKUWA NA BAHATI

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anaamini kikosi chake hakikuwa na bahati na kujikuta kikifungwa mabao 4-0 na Manchester United kwenye mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu ya England juzi Jumapili.

Blues hao walicheza vizuri na kuonekana kuelewana zaidi katika dakika za mwanzo za mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Old Trafford, lakini mabao mawili ya Marcus Rashford na mengine mawili kutoka kwa Anthony Martial na Daniel James yakawafanya waondoke vichwa chini.

Na Lampard anaamini kwamba matokeo hayo yalikuwa mabaya kwao na kwamba hawakua na bahati.

"Tulifanya makosa yaliyozalisha mabao," alisema Lampard akiiambia Sky Sports baada ya mchezo huo.

"Tulitawala kwa muda mwingi wa kipindi cha kwanza. Pengine maamuzi mabovu yalitugharimu.

"Katika kipindi cha kwanza tulitakiwa kuwa mbele kwa mabao. Ilikuwa rahisi zaidi kwao wakati walipokuwa mbele kwa mabao 3-0. Hasa kwa timu inayotumia mbinu ya kufanya mashambulizi ya kushitukiza.

"Walikuwa na kasi hivyo walipopata mpira walitumia mashambulizi ya kushitukiza. Sisi ndio tulioku-wa na mpira. Tumejifunza somo kubwa namna ya kujifunza. Haikuwa na kuepuka kichapo cha mabao 4-0."

# Pogba: Bado kuna swali kuhusu mimi kubaki Utd

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba amebainisha kwamba bado kuna "alama ya kuuliza" kuhusu majaliwa yake hapo Manchester United lakini ameahidi kwamba "atajitolea kila kitu" wakati huu akiwa amebakia Old Trafford.

Mfaransa huyo amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Real Madrid na Juventus baada ya kusema anataka "changamoto mpya" mapema mwanzoni mwa kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa ESPN FC mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 hatauzwa licha ya soko la usajili kwa ligi nyingine Ulaya bado halijafungwa hadi Septemba 2 mwaka huu.


Baada ya kuiongoza United wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Chelsea juzi Jumapili, Pogba ameacha mlango wazi kwa uhamisho wake.

"Mara zote nakuwa vizuri ninapocheza soka," amesema kiungo huyo wa Ufaransa wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Hicho ndio kitu ninachokitaka, ni kazi yangu. Najitoa kwa asilimia zote kila wakati nikiwa kwenye dimba la kijani.

"Kwa kawaida kuna mambo yanazungumza, lakini muda utaongeza. Hii alama ya kuuliza itabakia.

"Hata hivyo, kama nilivyosema, nipo hapa Manchester. Nafurahia kucheza na wachezaji wenzangu na mara zote nataka kushinda kila mchezo. Nitajitolea kila kitu."



## Hazard ajiona anacheza mbingu ya saba Real Madrid

**MADRID, Hispania**

EDEN Hazard amejifunza mengi kutoka kwa makocha wa zamani, Antonio Conte na Maurizio Sarri lakini amebainisha yupo "kwenye mbingu ya saba" kucheza chini ya mtu aliyemvutia katika soka, Zinedine Zidane.

Baada ya kusajiliwa kutoka Chelsea kipindi hiki cha majira ya joto alifunga bao lake la kwanza kwa Los Blancos wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Salzburg Jumatano iliyopita na pia alicheza dhidi ya AS Roma Jumapili.

Madrid itaanza msimu mpya wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, baadae wiki hii dhidi ya Celta Vigo na Hazard ana matarajio chanya kwa kuelekea ufunguzi wa ligi hiyo huku akitoa maneno ya kumsifu kocha huyo.

"Nikiwa mtoto nilikuwa na ndoto ya kuvaa jezi ya Real Madrid," amesema Hazard akiiambia Corriere della.

"Wakati Real Madrid wanapogonga mlango wako, kitu pekee unachoweza kufanya ni kitu kimoja tu: Fungua.

"Nikiwa Chelsea nilitumia miaka ambayo haitasaulika, lakini nipo hapa nikiwa katika mbingu ya saba. Mmoja walionihamasisha wakati nikiwa mtoto ni Zinedine Zidane. Nilikuwa na bango chumbani kwangu na sasa nimepata nafasi ya kufundishwa na yeye."

Wakati Hazard akianza ukurasa mpya pale Santiago Bernabeu, kocha wake wa zamani Conte atakuwa Inter Milan pamoja na mchezaji mwenzake wa Ubelgiji, Romelu Lukaku.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE : PSG HAIWEZI KUWA SAWA BILA NEYMAR

Lazima pia tuone nini kitakachotokea, lakini tutajaribu kulifanya hilo kwa mashabiki, mengine tuiachie bodi ili...

**PARIS, Ufaransa**

Kylian Mbappe amekiri kuwa mabingwa wa Ligue 1, Paris Saint-Germain haiwezi kuwa sawa bila Neymar wakati huu tetesi zikizidi kuongezeka kuhusu majaliwa yake ya baadaye klabuni hapo.

Neymar amekuwa akihusishwa na kurejea klabu yake ya zamani ya Barcelona sambamba pia na kujiunga na miamba ya La Liga, Real Madrid, na hakuwapo dimbani katika kikosi cha PSG kilichofungua pazia la kuanza kutetea ubingwa wao kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Nimes juzi, Jumapili.

Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo alifunguka kuwa Neymar - ambaye aliigharimu uhamisho wa rekodi ya dunia kiasi cha euro milioni 222 wakati akitokea Barca mwaka 2017 - anaweza kuwa amekaribia kuondoka kwa matajiri hao jiji la Ufaransa.

Alipoulizwa endapo PSG inaweza kujizatiti msimu huu, nyota mwenzake, Mbappe aliiambia Canal+: "Inategemea, tutajaribu.

"Lakini hatutadanganya; lazima pia tuone nini kitakachotokea na Neymar. Si timu moja bila Neymar kama ilivyo kwake. Lakini tutajaribu kulifanya hilo kwa mashabiki."

Neymar amefunga mabao 34 katika mechi 37 za Ligue 1 alizocheza ingawa katika misimu yake yote PSG amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mguu.

Mchezaji mwenza wa PSG na Brazil, Marquinhos alikanusha tetesi hizo wakati akiendelea kuzingatia kuelekeza mtazamo wake katika soka.

"Kila mtu anaangazia mchezo wetu, na falsafa yetu," Marquinhos aliongeza kupitia Canal+. "Mengine tunayaacha kwa bodi na Neymar.

"Wanajua vizuri sana nini cha kufanya. Ukweli tunapaswa kufikiri kuhusu uwanjani, na si uhamisho."

## KWA UFUPI

**LAMPARD AMTAKA CHILWELL**
KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anataka kuipata saini ya beki wa Leicester City, Ben Chilwell wakati kifungo chao cha kusajili kitakapomalizika. Nyota huyo wa kimataifa wa England, 22, anathaminishwa na pauni milioni 70. ***(Sun)***

**POGBA AFUNGUKA UNITED**
KIUNGO wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba, 26, amesema mara zote "kumekuwa na ulizo" kuhusu mustakabali wake wa baadaye hapo Manchester United. ***(RMC - in French)***

**COUTINHO HATAONDOKA- BARCA**
Barcelona amesema winga wa Brazil, Philippe Coutinho hataondoka klabuni hapo majira haya ya joto. ***(Marca)***

**OZIL ANUKIA DC UNITED**
WAWAKILISHI wa kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil, 30, watakwea pipa kwenda Marekani kufanya mazungumzo na DC United kuhusu uwezekano wa nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani kujiunga na timu hiyo. ***(Express)***

**MOURINHO AANZA SHOMBO ZAKE**
KOCHA wa zamani wa Manchester United na Chelsea, Jose Mourinho, amesema timu ya Manchester City B inaweza kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mbele ya ama klabu zake hizo za zamani au Arsenal. ***(Telegraph)***

**MANGALA KURUDI TENA VALENCIA**
BEKI wa kati wa Manchester City na Ufaransa, Eliaquim Mangala, 28, anaonekana kujiandaa kutua kwa mkopo Valencia kwa kipindi cha pili. ***(Goal)***

**CHADLI AMFUATA KOMPANY**
KIUNGO wa zamani wa Tottenham na West Brom, Mbelgiji Nacer Chadli, 30, amejiunga na Vincent Kompany katika klabu ya Anderlecht kwa mkopo akitokea Monaco. ***(Anderlecht official website)***

**SARRI: DYBALA ONDOKA**
KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri amesema mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Paulo Dybala, 25, ambaye alikuwa akihusishwa na Manchester United na Tottenham majira haya ya joto, anapaswa kuondoka kwa mabingwa hao wa Serie A ama kujitia majaribuni kwa kutemwa katika kikosi cha kwanza cha mabingwa hao wa Italia. ***(Mirror)***

**NAPOLI KUMPOTEZEA RODRIGUEZ**
Napoli ipo tayari kunyosha mikono juu kuhusu kujaribu kuipata saini ya kiungo mshambuliaji wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez, 28, na badala yake kujaribu kuipata saini ya winga wa PSV Eindhoven na Mexico, Hirving Lozano, 24. ***(Gazzetta dello Sport, via Marca)***

**RAFINHA KUACHWA BARCA**
Barcelona itamruhusu Rafinha - ambaye alikuwa akihusishwa na Liverpool na Arsenal - kuachana na klabu hiyo majira haya ya joto wakati huu Valencia ikipewa nafasi ya kumnasa kiungo huyo Mbrazil mwenye umri wa miaka 26. ***(Sport)***

**LUKAKU AANZA NA NNE INTER**
Romelu Lukaku, 26, amefunga mabao manne katika mechi yake ya kwanza kuichezea Inter Milan katika ushindi wa mabao 8-0 dhidi ya klabu ya Daraja la Nne ya Virtus Bergamo. Straika huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alikamilisha uhamisho wake wa kujiunga na klabu hiyo ya Italia akitokea Manchester United dakika za mwisho kabla ya dirisha la usajili England kufugwa. ***(Manchester Evening News)***

**LOVREN BADO LULU ROMA**
Roma bado inahitaji saini ya beki wa kati wa Liverpool na Croatia, Dejan Lovren, 30. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

HABARI MICHEZO

# AZAM FC KUWAMALIZIA WAETHIOPIA CHAMAZI

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Fasil Kenema kwenye mchezo wa kwanza wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC imeahidi kufanya kweli katika mechi ya marudiano itakayopigwa jijini Dar es Salaam Agosti 24, mwaka huu.

Azam imekuwa timu pekee iliyopoteza kati ya nne zinazopeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa Tanzania Bara.

Azam FC inayonolewa na Mrundi Etienne Ndayiragije ikiwa ugenini nchini Ethiopia juzi, ilikubali kipigo cha bao 1-0 katika mchezo uliokuwa na presha kali kutokana na wenyeji kupata sapoti kubwa kutoka kwa mashabiki wao walioujaza uwanja wao unaokadiriwa kuchukua watazamaji 55,000 kutokana na kuruhusiwa kuingia bure.

KMC ambayo inashiriki michuano ya Kombe la Shirikisho yenyewe Jumamosi ilifanikiwa kupata sare tasa ugenini Kigali dhidi ya AS Kigali, wakati Simba na Yanga zinazopeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika nazo zikitoka sare katika mechi zao za awali.

Simba ikiwa ugenini Msumbiji, ilitoka sare tasa dhidi ya UD Songo wakati Yanga ikilazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani katika Uwanja wa Taifa dhidi ya Township Rollers ya Botswana.

Afisa Habari wa Azam FC, Jaffary Maganga akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika juzi, alisema dakika 90 za mwanzo zimekamilika kwa kupoteza, hivyo hesabu zao ni kujipanga kupata matokeo chanya mechi ya nyumbani.

"Tumemaliza dakika 90 za awali ugenini, baada ya kumaliza kwa kufungwa bao 1-0, sasa mipango yetu ni mchezo wa marudio na sisi tutatumia vema uwanja wa nyumbani ili kusonga mbele," alisema.

Azam sasa itabidi kuhamasisha mashabiki wengi kwenda uwanjani kuipa sapoti itakaporudiana na timu hiyo katika Uwanja wa Azam Complex Agosti 24 ili kuweza kupata matokeo. Mshindi wa jumla katika mechi hiyo atamenyana na mshindi kati ya Triangle FC ya Zimbabwe na Rukinzo FC ya Burundi, anapotokea kocha Ndayiragije.




Mabingwa wa Cosafa U-20, Timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania chini ya miaka 20 (Tanzanite), wakisherehekea na kombe lao baada ya kulitwaa nchini Afrika Kusini kwa kuifunga Zambia 2-1 kwenye mechi ya fainali juzi. **PICHA: TFF**



# Minziro kuipaisha Singida United

**Na Mwandidhi Wetu**

WAKATI zikiwa zimebaki siku 10 kabla ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara kuanza, Kocha Mkuu wa Singida United, Felix Minziro, amesema kikosi chake kimefanya maandalizi mazuri na ana uhakika wa kufanya vizuri msimu huu.

Singida United ambao huu utakuwa ni msimu wa tatu kwao kushiririki Ligi Kuu Bara tangu ilipopanda msimu wa 2017/18, msimu uliopita imaliza katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20.

Ilishinda mechi 11, ikapoteza 13 na kutoka sare 14 huku safu yake ya ulinzi ikiruhusu mabao 39 na ile ya ushambuliaji ikifumania nyavu mara 30 tu.

Hata hivyo, Minziro aliyeanza kukinoa kikosi hicho wakati msimu ukielekea ukingoni, amepania kuuanza vema msimu huu, unaotarajiwa kuanza kufurukuta Agosti 23, mwaka huu.

"Wachezaji wanaendelea kupambana na wana kazi kubwa ya kufanya kwa ajili ya msimu ujao.

"Tunatarajia ushindani utakuwa mkubwa nasi pia tumejipanga kufanya vizuri kikubwa tunahitaji sapoti kutoka kwa mashabiki na wadau wote," alisema Minziro ambaye amekuwa akiziokoa timu nyingi za Ligi Kuu zinazochungulia kushuka daraja, huku pia akiwa na rekodi nzuri ya kupandishi timu Ligi Kuu Bara.

# Shime atoa siri ya mafanikio Tanzanite

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wapya wa michuano ya Cosafa U-20 kwa upande wa wanawake, timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania chini ya miaka 20 (Tanzanite), wamerejea jana jijini Dar es Salaam na kombe hilo huku wakianika siri kubwa ya mafanikio yao.

Tanzanite ambayo katika mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Wolfson juzi ililipa kisasi kwa kuifunga Zambia mabao 2-1, idadi kama iliyofungwa awali na Wazambia hao kwenye hatua ya makundi, imetwaa ubingwa huo huku ikiwa imepoteza mchezo mmoja tu katika mashindano hayo.

Kocha Mkuu wa Tanzanite, Bakari Shime, aliliambia Nipashe kuwa siri kubwa ya mafanikio hayo ni kujiamini na kucheza soka la kushambulia mwanzo mwisho.

"Kazi ilikuwa moja tu, kutafuta matokeo na kulipa kisasi kwa wapinzani wetu kwa kuwa tuliingia uwanjani na kumbukumbu ya kufungwa mabao 2-1 mchezo wa hatua ya makundi.

"Wachezaji walionyesha juhudi na mbinu kubwa ilikuwa ni kushambulia mwanzo mwisho jambo ambalo limesaidia timu kutwaa ubingwa, shukrani kwa mashabiki kwa sapoti kubwa," alisema Shime.

Tanzanite imerejea nchini ikitokea Port Elizabeth, Afrika Kusini ilipokua ikishiriki mashindano hayo ambapo imefanikiwa kutwaa ubingwa huo kwa kuonyesha soka la kuvutia na kiushindani.

Katika hatua ya makundi, Tanzanite ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Botswana, 8-0 dhidi ya Eswatini na kupoteza mchezo mmoja dhidi ya Zambia kwa kuchapwa 2-1.

Baada ya hapo ilipata ushindi wa mabao 2-0 kwenye nusu fainali dhidi ya Afrika Kusini kabla ya kuifunga Zambia 2-1 katika mchezo wa fainali iliochezwa juzi.

Mbali na Tanzanite kutwaa kombe hilo na medali za dhahabu, nahodha wa kikosi hicho, Enekia Kasonga alitangazwa kuwa mchezaji Bora wa Mashindano.

# Michezo

Jumanne Agosti 13, 2019

Nipashe




Mbappe : PSG haiwezi kuwa sawa bila Neymar HABARI UK 30

TOBO, BAO...



Mshambuliaji wa Manchester United, Mfaransa Anthony Martial, akizamisha mpira kimyani kwa kumpiga 'tobo' kipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi. **HABARI UK. 29**

# YANGA YAITIA HOFU TOWNSHIP ROLLERS

●●● Kocha wao akiri vijana hao wa Jangwani wanakimbiza sana na wana njaa ya matokeo, Zahera afunguka...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kuwa na faida ya bao la ugenini walilolipata katika sare ya 1-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita, Kocha Mkuu wa Township Rollers, Tomas Trucha mzaliwa wa Jamhuri ya Czech, ameshindwa kujiamini kwa asilimia zote kuibuka na ushindi ama kulinda matokeo hayo ili kuweza kusonga mbele, imefahamika.

Kutokana na matokeo hayo, mechi ya marudiano itakayopigwa Jumamosi ya Agosti 24, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa mjini Gaborone, Botswana, Yanga itakuwa ikihitaji ushindi ama sare ya kuanzia mabao mawili ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Hata hivyo, kuelekea mechi hiyo ya marudiano, Kocha Mkuu wa Township Rollers, Trucha amesema bado wana kazi kubwa ya kufanya mbele ya Yanga baada ya kuruhusu wenyeji wao kusawazisha na kufanya matokeo kuwa bao 1-1 katika Uwanja wa Taifa.

Township Rollers ambayo ilipata bao dakika ya saba tu tangu mechi hiyo ilipoanza Jumamosi iliyopita, kabla ya Ptrick Sibomana kuisawazishia Yanga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 86, sasa itahitaji ushindi ama sare tasa ili kusonga katika michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Pamoja na kwamba sina hofu kubwa sana, tunapaswa kujipanga vema kwa kuwa tunacheza na timu ambayo ina wachezaji wenye kiu ya kupata matokeo, hivyo hatupaswi kuwabeza hata tukiwa uwanja wa nyumbani.

"Tayari tumefahamu namna wapinzani wetu wanavyocheza na mbinu wanazotumia, si watu wa kukata tamaa, licha ya kwamba tuliwabana mwanzo kwa kuwafunga mapema, waliendelea kutuandama na mwisho wa siku wakapata bao," Trucha alifunguka.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, ambaye atakuwa na mechi mbili za kirafiki dhidi ya Polisi Tanzania itakayopigwa mjini Moshi na FC Leopards ya Kenya itakayopigwa jijini Arusha, lengo likiwa ni kurekebisha makosa aliyoyabaini kabla ya kuwafuata wenyeji wao, Township Rollers, atakachokifanya ni kuhakikisha anaifanyia kazi safu ya ushambuliaji ambayo ilifanya makosa mengi.

"Kuna makosa mengi yaliyofanywa na wachezaji wangu hususan safu ya ushambuliaji huku muunganiko wa timu bado ukionekana haujakaa sawa, tulitarajia kushinda nyumbani, lakini hilo halikuwezekana.

"Tunatambua katika michuano hii ni muhimu kushinda nyumbani, lakini tunaweza kuingiza mabao hata mawili kwao, hasa tukizingatia tuna mechi moja yakutupa tiketi ya kusonga mbele, wao wamepata bao kwetu na sisi tunaweza kufanya hivyo kwao," alisema.

Katika mechi hiyo ya marudiano, Yanga itapaswa kuma makini hususani kwa nyota aliyeanza kuwaliza dakika ya saba, Phenyo Serameng.

Mshindi wa jumla kati ya Yanga na Township Rollers atakutana na mshindi wa jumla wa mechi kati ya Green Mamba ya Eswatini (zamani Swaziland) na Zesco ya Zambia.

## Kuziona Simba, Azam FC buku 5

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba imerejea leo katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Bara (Ngao Jamii) dhidi ya Azam FC baada ya mapumziko ya siku moja, jana kupisha Sikukuu ya Eid, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limeanika viingilio vya kuiona mechi hiyo itakayopigwa Jumamosi ijayo majira saa moja usiku.

Simba na Azam FC zitashuka katika Uwanja wa Taifa Jumamosi kuwania Ngao ya Jamii ambayo ni ishara ya kufunguliwa kwa msimu mpya wa 2019/20 unaotarajiwa kuanza Agosti 23, mwaka huu ambapo kwa mujibu wa ratiba mchezo wa kwanza utakuwa kati ya mabingwa watetezi, Simba na JKT Tanzania kwenye dimba hilo.

**Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari kupitia kwa Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, imeeleza kuwa kiingilio cha chini kwenye mchezo huo kwa jukwaa la mzunguko ni Sh. 5,000 na Jukwaa la VIP B na C itakuwa Sh. 10,000.**

Mechi ya Ngao ya Jamii huwakutanisha mabingwa wa Ligi Kuu Bara, ambao kwa sasa ni Simba pamoja na mabingwa wa Kombe la Shirikisho, linaloshikiliwa na Azam FC kwa sasa.

Timu hizo pia zitautumia mchezo huo kujiandaa na mechi ya kimataifa, ambapo Simba inatarajia kuialika UD Songo ya Msumbiji kati ya Agosti 23-25, kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa baada ya kutoka sare tasa ugenini, wakati Azam yenyewe ikijiandaa kupindua matokeo ya bao 1-0 itakapoikaribisha Fasil Ketema ya Ethiopia katika Uwanja wa Chamazi Agosti 24, mwaka huu katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >